# Nipashe

Jumatatu Juni 24, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0579952

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper




## THRDC yaainisha mambo hatari kwa uhai wa Azaki

UKURASA 3




UKURASA 13

# Lipumba aishauri serikali kukopa BoT

*Endelea uk. 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 4


**DC AWATEGA POLISI KUACHIA HURU MTUHUMIWA WA MAUAJI**

MKUU wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, ameiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) mkoani humo, kuwachunguza askari polisi wa kituo cha Tinde, Shinyanga Vijijini ...

UKURASA WA 26

**LUGOLA ASHANGAA MAHABUSI KUKAA MIEZI 6 KITUO POLISI**

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, ameshangazwa kuona mahabusi 11 waliofutiwa kesi mahakamani kuwekwa katika Kituo cha Polisi...



Prof. Ibrahim Lipumba

Dk. Philip Mpango

## WALENGWA UBORESHAJI DAFTARI LA MPIGAKURA

UK. 2

## Hoja 10 zinazosubiri majibu ya Mpango mjadala bajeti

UK. 2

**MICHEZO** OKWI AIWEKA KIPORO SIMBA UK.32

MAONI, KATUNI UK.6

## HABARI KITAIFA

## Walengwa uboreshaji wa Daftari Mpigakura

**Na Romana Mallya**

UBORESHAJI wa Daftari la Kudumu la Mpigakura linalotarajia kuanza mwezi ujao, litahusu kurekebisha taarifa za wapigakura, kuhamisha taarifa za waliohama, kuwaondoa waliopoteza sifa na kutoa kadi mpya kwa waliozipoteza na zilizoharibika.

Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Dk. Athuman Kihamia, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa semina waliyoitoa kwa wahariri na waandishi wa habari.

Akizungumza kuhusu uboreshaji wa daftari hilo, Dk. Kihamia alisema uboreshaji utahusu raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 na zaidi na wale ambao watakuwa wametimiza umri wa miaka 18 siku ya uchaguzi mkuu unaotarajia kufanyika mwakani.

"Kumefanyika uhakiki wa vituo vya kuandikisha wapigakura baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2015. Uhakiki huo ulilenga kuweka vituo katika maeneo yaliyokubalika pamoja na kuweka angalau kituo kimoja katika kila mtaa au kijiji kwa kuzingatia umbali na idadi ya watu eneo husika," alisema.

Alisema maeneo yaliyokubalika kwa mujibu wa Kanuni ya 12(2) ya Kanuni za Uboreshaji wa Daftari nchini ya Sheria ya Uchaguzi, sura ya 343 na Kanuni ya 15(2) ya Kanuni za Uboreshaji wa Daftari chini ya Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa sura ya 292 ni majengo ya umma na yale ya wazi yanayofikika kwa urahisi.

Maeneo yasiyokubalika kuwa ni kambi za jeshi, nyumba za ibada, ofisi za vyama vya siasa, kambi na makazi ya polisi.

Dk. Kihamia alisema mpigakura ambaye hatakuwa na kadi yake ya awali, taarifa zake zitatafutwa ndani ya mfumo.

"Endapo taarifa zake hazitapatikana, mpigakura ataandikishwa upya kwa kujaza

INAENDELEA UK. 8

# Lipumba aishauri serikali kukopa BoT

**Na Enock Charles**

MWENYEKITI wa Chama cha Wananchi (CUF), Prof. Ibrahimu Lipumba, ameishauri serikali kukopa fedha Benki Kuu ya Tanzania (BoT), kwa lengo la kuongeza ujazi wa fedha kwenye mzunguko wa fedha nchini, ili kutatua changamoto ya hali ngumu ya kibiashara kwa wananchi.

Akizungumza juzi kwenye kongamano la Haki na Furaha kwa Wote katika uzinduzi wa sera ya furaha kwa wananchi wote, Prof. Lipumba alisema hali ngumu ya kibiashara wanayokutana nayo wafanyabiashara wengi nchini

inatokana na kupungua kwa ujazi wa fedha katika mzunguko wa fedha nchini.

"Moja ya tatizo ni kwamba mzunguko wa fedha katika uchumi umepungua, ujazi wa fedha mwaka 2015 ulikuwa kwa asilimia 14.5, mwaka 2016 ukuaji wa ujazi wa fedha ukapungua chini ya asilimia moja, mwaka 2017 ukawa kama asilimia 1.3, mwaka 2018 ukawa chini ya asilimia moja kwa wastani wa miaka mitatu iliyopita," alisema na kuongeza:

"Ujazi wa fedha za msingi ukuaji wake upo chini ya asilimia moja wakati hatuna tatizo la mfumuko wa bei."

Kwa mujibu wa Prof. Lipumba, miaka mitatu ya mwisho ya uongozi wa awamu iliyopita, ujazi wa fedha ulikuwa kwa asilimia 15 na kwamba kwa sasa umeporomoka na kufikia chini ya asilimia moja.

"Wananchi wanalalamika kwamba vyuma vimekaza, lakini ukitazama takwimu hali ni nzuri, Mheshimiwa

Jakaya Kikwete alikuwa mzee wa kutumia ujazi wa fedha wakati wake ulikuwa unaongezeka kwa asilimia 15 kipindi cha miaka mitatu iliyopita umeporomoka chini ya asilimia moja, lazima patakuwa na tatizo katika mzunguko wa fedha," alisema Lipumba ambaye ni profesa wa uchumi.

Prof. Lipumba pia alishauri serikali kuwekeza katika sekta ya kilimo, akieleza

INAENDELEA UK. 8



Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi (CUF), Ibrahimu Lipumba, akizungumza na wanachama kwenye kongamano la Sauti ya Haki na Furaha kwa Wote lililofanyika jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MIRAJI. MSALA**


## alkhalij enterprises Limited

### JOB OPENING
### SALES EXECUTIVE

**Roles and Responsibilities:**

- Present and sell the Company's products and solutions to new and existing accounts
- Accountable for ensuring timely communication and customer satisfaction at assigned accounts
- Understand each customer's business and technical applications, anticipating their needs for products and solutions
- Establish and strengthen individual relationships within purchase, maintenance, and operations departments at assigned accounts
- Identify and analyze key opportunities and threats as it relates to products, markets, and competitors
- Prepare weekly and monthly reports on customer visits, significant quotations, and overall sales activity
- Achieve the allocated sales target for assigned accounts and new business

**Requirements:**

- A degree from a reputable academic institution
- Minimum 2-3 years' sales experience related to products
- Effective communication skills and an ability to build and sustain strong customer relationships
- English proficiency is a must
- Willing to work in Dar es Salaam, Tanzania and travel to other cities

To apply, please send your CV to careers@alkhalij.com

115289902


# Hoja 10 zinazosubiri majibu ya Mpango mjadala bajeti

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

HOJA takribani 10 za mjadala wa bajeti kuu ya serikali ya mwaka wa fedha 2019/20, zinasubiri majibu ya Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, kwa wabunge, ambazo walizoeleza katika michango yao wiki iliyopita.

Ziko hoja kadhaa ikiwamo sera ya mwaka jana iliyoruhusu msamaha wa kodi kwa taulo za kike kufutwa na serikali kuja na pendekezo la kurejesha kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwenye taulo za kike.

Masuala mengine yaliyoibuka katika bajeti hiyo ya Sh. trilioni 33.1 ni mazingira ya uendeshaji wa biashara nchini, utitiri wa kodi na tozo zilizovyochangia kuua soko la kimataifa la Kariakoo, kupandishwa kwa kodi kwenye nywele za bandia hasa mawigi na rasta za bei mbaya.

Hoja nyingine ni kukua kwa hali ya uchumi visiwani Zanzibar, huku gharama za maisha visiwani humo zikidaiwa kuongezeka kutokana na tozo za kodi za bidhaa zinazoingia kutoka Bara.

Limo pia pendekezo la serikali la kuongeza kodi kwenye mafuta ghafi yanayotoka nje ya nchi ili kulinda wazalishaji wa mbegu za mafuta hapa nchini.

Pia, suala la serikali kutenga fedha nyingi katika miradi mikubwa ya maendeleo na kuacha kutazama sekta ya kilimo inayogusa moja kwa moja maisha ya kila siku ya Mtanzania.

Kwa mujibu wa ratiba ya mkutano wa 15 wa Bunge

(mkutano wa bajeti), Waziri Dk. Mpango anapaswa kujibu hoja za wabunge zilizochomoza katika mjadala kuhusu taarifa ya hali ya uchumi, hotuba ya bajeti ya serikali na kuhitimisha mjadala huo leo au kesho ukifuatiwa na upigaji wa kura ya wazi.

Mkutano huo wa Bunge la Bajeti, ulianza Aprili 2, mwaka huu na linatarajiwa kumalizika 28 Juni, 2019 ambapo Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa atatoa hoja ya kuahirisha Bunge.

**KUFA KWA SOKO LA KARIAKOO**

Pia suala la kupotea katika ramani ya biashara soko la kimataifa la Kariakoo, nalo lilichukua mjadala mpana huku, wabunge wakitaka Waziri Mpango kukaa pamoja na Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa na kutafuta ufumbuzi wa kulirejesha kuwa imara.

Aliyeibua hoja hiyo alikuwa ni Mbunge wa Mvomero (CCM), Sadiq Murad, aliyedai kuwa soko la Kariakoo limepotea katika ramani ya biashara, licha ya kuwa Tanzania ilishafanikiwa kuziteka kibiashara nchi za Burundi, Rwanda, Malawi, Uganda na Kongo.

**KUHUSU KILIMO**

Katika mjadala huo baadhi ya wabunge, walieleza kuwa kilimo ni sekta inayotakiwa kuguswa kikamilifu ili kupambana na umaskini wa watu, hivyo haikuwa vyema

INAENDELEA UK. 8

## HABARI KITAIFA



Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, akisikiliza na kutatua kero za wananchi wa Kijiji cha Buchama, Kata ya Tinde, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga Vijijini kwenye mkutano wa hadhara na kuwataka pia wajitume kuchangia shughuli za maendeleo. **PICHA: MARCO MADUHU**

# THRDC yaainisha mambo 10 hatari kwa uhai wa Azaki

**Na Salome Kitomari**

MTANDAO wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), umeainisha mambo 10 hatarishi kwa uhai wa Azaki katika muswada wa marekebisho ya sheria zinazosimamia mashirika ya kiraia nchini (NGO).

Aidha, umeshangazwa na dharura ya serikali kupeleka rasimu ya marekebisho iliyotengenezwa kwa siku 50, lakini siku mbili kabla ya kupelekwa bungeni yaliwekwa kwa Azaki na kunyimwa haki ya kushiriki mchakato mzima wa utengenezaji.

Kwa mujibu wa uchambuzi huo uliotolewa

**INAENDELEA UK. 26**

# Bandari kavu Vigwaza kuanza kazi mwezi ujao

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isack Kamwelwe, amesema bandari kavu ya Kwala iliyopo Vigwaza mkoani Pwani, inatarajiwa kuanza kupokea makontena kutoka Bandari ya Dar es Salaam kuanzia Julai, mwaka huu.

Amesema kuanza kufanya kazi kwa bandari hiyo kutasaidia kupunguza msongamano wa mizigo iliyopo katika Bandari ya Dar es Salaam.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki akiwa kwenye mkutano uliowakutanisha wadau mbalimbali wanaohusika na huduma za bandari uliofanyika katika eneo la bandari hiyo.

"Serikali tumejipanga kuhakikisha huduma za bandari hii zinakuwa bora na zenye tija mara zitakapoanza, kikubwa ni wadau wote kutoa ushirikiano ili mipango yote iliyowekwa iweze kufikiwa kama ilivyotarajiwa," alisema Kamwelwe.

Alisema ujenzi wa bandari hiyo ni mikakati inayofanywa na serikali kuondoa msongamano wa mizigo inayoshushwa bandarini na kusafirishwa kwenda katika nchi jirani zinazotumia bandari hiyo.

Waziri Kamwelwe aliongeza kuwa kuanzia Julai, bandari hiyo ambayo ujenzi wake unaendelea kwa hatua ya uwekaji wa tabaka la zege ardhini, itakamilika rasmi katika kipindi cha miezi mitatu ijayo ikihusisha huduma mbalimbali zikiwamo ulipiaji wa mizigo.

Aliongeza kuwa bandari hiyo itaunganishwa na huduma za reli ikiwamo ya Kampuni ya Reli ya TRC pamoja na Tazara, pia itakuwa mkombozi kwa kupunguza foleni ya malori katika Jiji la Dar es Salaam.

Kadhalika, Waziri Kamwelwe aliwaagiza watoa huduma wote wakiwamo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Tume ya Mionzi, TRC, TAZARA, Dawasa, Wakala wa Meli (TASAC), kuweka ofisi zao katika eneo hilo haraka ili kurahisisha utoaji wa huduma.

Aidha, alimtaka Mkurugenzi wa Wakala wa Ujenzi wa Barabara (Tanroads), kujenga barabara kutoka eneo la Vigwaza hadi katika bandari hiyo yenye urefu wa kilomita 18, akitoa ahadi ya kuwasiliana na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, ili kuwezesha kujengwa kituo kikubwa cha polisi katika eneo hilo.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) Deusdedit Kakoko, alisema ujenzi wa bandari hiyo umefikia pazuri na kwamba agizo la waziri alilotaka bandari hiyo kuanza huduma Julai litatekelezeka kwa ushirikiano baina ya TPA na Suma JKT.

Mkurugenzi wa TRC Masanja Kadogosa, alisema katika kuitikia wito wa ujenzi wa bandari hiyo, TRC tayari imeanza utandazaji wa reli kwenda katika eneo hilo, huku akiahidi kuwa hadi kufikia Julai Mosi, reli hiyo itakuwa imekamilika.

# Askofu KKKT aomba JPM aombewe

**Na Danny Tweve,** SONGWE

ASKOFU mstaafu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri (KKKT), Dayosisi ya Konde, Dk. Israel Mwakyolile, amewataka Watanzania waendelee kumwombea Rais John Magufuli kutokana na watu wachache kuanza kutafuta namna ya kujinasua hata kwa kutumia mbinu chafu.

Akizungumza kwenye ibada ya kutimiza miaka 33 kwa Kanisa la KKKT Usharika wa Vwawa, makao makuu ya Mkoa wa Songwe, Askofu Mwakyolile amesema, ni muhimu kuliko wakati mwingine kwa Watanzania kumwombea Rais wao kwa yale anayoyasimamia.

Alisema katika kipindi hiki, kuna watu wanapata tabu sana kutokana na mtazamo wa serikali na fursa kwa wanyonge zikifunguliwa huku wachache walafi wakibanwa.

Alisema wapo wanaotafuta njia chafu za kuzima jitihada hizo jambo ambalo Watanzania wanapaswa kufanya maombi kwa kadiri wawezavyo.

Katika ibada hiyo aliyekuwa Meneja wa TRA Mkoa wa Songwe, Paul Walalaze, aliwekewa mikono ya baraka yeye na mkewe wakati wa kuaga, kufuatia kuhamishiwa Mkoa wa Temeke, huku akiwa ameupandisha Mkoa wa Songwe katika makusanyo ya TRA kwa mwaka wa pili mfululizo.

Aidha, katika ibada hiyo zaidi ya waumini 50 walibariki ndoa zao katika ibada hiyo kutokana na utaratibu wa Kiongozi wa Usharika Mchungaji John Mwasakilali, kutenga siku ya maadhimisho ya kanisa kuwa sehemu pia ya kuunganisha ndoa za waumini wake, zoezi ambalo limepokewa pia na watu waliofikisha umri wa miaka 60 kwenye ndoa zao kupata baraka.

Kanisa hilo linaadhimisha miaka 33 tangu usharika wa Vwawa kuanzishwa likiwa limetekeleza shughuli za kijamii ikiwamo uanzishaji wa shule ya watoto, miradi ya usindikaji nafaka na upandaji miti.


twiga cement
HEIDELBERGCEMENT Group

**TENDER INVITATION**

Tanzania Portland Cement Public Limited Company (TPCPLC) invites tenders from eligible, reputable and competent tenderers for **Provision Plant Sweeping services**

**TENDER INSTRUCTIONS AND CONDITIONS**

1. Tender documents in English language shall be collected from Procurement Offices from 9AM to 4PM, between 26th June 2019 and 28th June 2019. Tender documents are issued free of charge.

   Or Request tender through **Saphiness.kikwesha@heidelbergcement.com**. Telephone number 0785 670 641

2. TPCPLC is not responsible for any costs related to printing of the bids to be submitted by the tenderers.

3. Tenderers must submit well printed bids in a properly sealed envelope by hand and presented in ONE COPY addressed to:

   **Head of Procurement Cluster III,**
   **Tanzania Portland Cement Company Limited,**
   **P.O. Box 1950,**
   **Dar es Salaam.**

4. Deadline for tender submission shall be 5Th July 2019 before 4PM. late bids shall not be accepted.

5. Tender envelopes must be clearly marked with the relevant tender.

6. Bids MUST be in Tanzania Shillings.

7. Bids should be valid for a period of 90 working days from the date of submission deadline.

8. TPCPLC in not bound to accept the lowest bid or any bid.

9. Sites visits are MANDATORY for all interested tenderers.

10. Documents to be submitted with tender documents include;
    i. Copies of Certificate of Incorporation/Registration/TIN/VRN and valid Business License.
    ii. Copy of tax clearance certificate from Tanzania Revenue Authority
    iii. Letters of recommendation from 3 current major clients.
    iv. Certified bank statement for the month of April 2019 **(1st to 31st May 2019)**
    v. Only short listed Companies will be contacted

215289502

# Vituo vinne vyaanzishwa kutoa huduma za Ukimwi

**Na Mwandishi Wetu**

TUME ya Kudhibiti Ukimwi nchini kwa kushirikiana na Kampuni ya Geita Gold Mine (GGM) imeanzisha vituo vinne vya utoaji huduma za Ukimwi na maarifa kwa lengo la kupunguza kasi ya maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi (VVU) hasa kwa madereva wa masafa marefu.

Vituo hivyo vimeanzishwa kwa kupitia kampeni ya Kilimanjaro Challenge ambayo imelenga kukusanya fedha za kutunisha mfuko wa Ukimwi (ATF) na kutokomeza VVU na Ukimwi.

Akizungumza na waandishi wa habari katika hafla ya kuwapokea watu zaidi ya 80 walioshuka Mlima Kilimanjaro baada ya kupanda kwa muda wa siku saba, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kupambana na Ukimwi (Tacaids), Jumanne Issango, alisema kampeni hiyo pia imesaidia baadhi ya vikundi vya kinamama wanaoishi na VVU kupewa mafunzo ya ujasiriamali.

Aidha, alivitaji vituo hivyo vilivyojengwa kwa kupitia kampeni hiyo ya Kilimanjaro Challenge kuwa ni Michungwani Handeni- Tanga, Manyoni Singida, Geita – Geita na Dumila- Kilosa Morogoro ambako ujenzi wake unaendelea.

Alisema vituo hivyo vitasaidia kuongeza kasi ya upimaji, upatikanaji wa matumizi sahihi ya dawa ni muhimu katika kufikia malengo ya kufikia 90-90-90 ifikapo mwaka 2020.

"Tatizo la Ukimwi kwa Tanzania bado ni kubwa kwani kutokana na takwimu zilizopo zinaonyesha kwa kila mwaka takribani watu

INAENDELEA UK. 8

# DC awatega polisi mtuhumiwa wa mauaji waliyemwachia huru

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

MKUU wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, ameiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) mkoani Shinyanga, kuwachunguza askari polisi wa kituo cha Tinde, Shinyanga Vijijini, kwa tuhuma ya kupokea rushwa kutoka kwa mganga wa kienyeji anayetuhumiwa kwa mauaji na kumwachia huru.

Mboneko alitoa agizo hilo juzi kwenye mkutano wa hadhara wa kusikiliza kero za wananchi na kuzitatua kwenye Kijiji cha Buchama, Kata ya Tinde, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga Vijijini, kufuatia malalamiko yaliyotolewa na wananchi kwa askari polisi wa kituo hicho kumwachia huru mtuhumiwa huyo wa mauaji.

Wananchi wakitoa malalamiko yao mbele ya mkuu huyo wa wilaya, walisema mganga huyo ambaye anafahamika kwa jina la Juma Dwale, wanamtuhumu kuhusika na tukio la mauaji ya mwanamke kwa kumkata mapanga na kisha kutoa nyeti zake, ambaye alikamatwa na Jeshi la Polisi, lakini ndani ya siku mbili akaachiwa.

Mmoja wa wananchi hao, Maganga Mhamila, alisema siku chache kabla ya kuachiwa mganga huyo huru, familia yake iliuza ng'ombe zaidi ya 20 na kuwaona watu wakienda nyumbani kwake na siku iliyofuata walimuona mitaani na kuanza kutamba kuwa mwenye pesa hawezi kufanywa chochote.

"Sasa hivi kwenye kijiji hiki hakuna amani kabisa, mganga huyu anatamba sana na kutishia kuwamaliza wale wote ambao walitoa taarifa juu ya yeye kuhusika na mauaji ya mwanamke huyo, yaani tunakosa usingizi kabisa, wanaume wazima tunajisaidia ndani kwenye makopo nyakati za usiku kwa kuogopa kuuawa," alisema Mhamila. Naye Mwenyekiti wa kijiji hicho cha Buchama, Rahel Kinga, alionyesha kusikitishwa na kitendo cha askari polisi wa kituo hicho, kumwachia huru mtuhumiwa huyo bila kufanya uchunguzi wa tuhuma zinazomkabili, na kurudi uraiani kuanza kutishia maisha ya wananchi.

Mkuu Wilaya licha ya kuiagiza Takukuru kuchunguza tuhuma hizo, pia alimwagiza Mkuu wa Kituo cha Polisi Tinde kuhakikisha mganga huyo anasakwa popote alipo na kukamatwa mara moja, ili uchuguzi wa tuhuma zinazomkabili uanze.

Alitoa wito kwa wananchi kutoa ushirikiano wa ushahidi kwa vyombo hivyo vya dola pale vitakapokuwa vikifanya kazi dhidi ya tuhuma zote walizozitoa ikiwamo ya rushwa na mauaji badala ya kukimbia ili haki iweze kutendeka, ikiwa mtuhumiwa hawezi kupewa hukumu kama hakuna ushahidi wa kutosha.

Mkuu wa Kituo hicho cha Polisi Tinde, Patrick Mkude, alikiri kumkamata mganga huyo wa kienyeji na kumwachia, huku akiahidi kutii agizo hilo la Mkuu wa Wilaya la kumsaka na kumkamata tena.



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, akisalimiana na baadhi ya watoto wenye matatizo ya moyo katika Hospitali ya Jakaya Kikwete iliyopo jijini humo juzi. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**


***Jipatie Maji ya Kunywa ya Kilimanjaro kwa Bei Elekezi za Rejareja kama Ifuatavyo:-***

- ***Nusu Lita (500ml) – TSHS. 500/=***
- ***Lita Moja na Nusu (1.5L) – TSHS. 1,000/=***
- ***Bei Hizi Elekezi ni Kwa Nchi Nzima***
- ***Maji ya Kunywa ya Kilimanjaro ni Maji ya Kuaminika Kila Siku***

215227501



## HABARI KITAIFA

# Ujangili meno ya tembo wadhibitiwa kaskazini

**Na Salome Kitomari**

UJANGILI wa meno ya tembo ukanda wa kaskazini umekwisha, na sasa wanaokufa hukutwa na meno yao tofauti na miaka ya nyuma ambako ujangili ulishamiri.

Hayo yalibainika mwishoni mwa wiki wakati wa ziara ya waandishi wa habari 10 wa Tanzania na Thailand, walioko kwenye programu maalum ya kuandika habari za ujangili na uhifadhi, chini ya Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania, kwa ufadhili wa Shirika la Misaada la Marekani (USAID).

Akiwasilisha mada ya hali ya ujangili na namna wanavyokabiliana na ujangili kwa mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Manyara na Tanga, Kamanda wa Kikosi dhidi ya Ujangili Kanda ya Kaskazini-Arusha, Peter Mbonjoko, alisema jitihada za serikali ya awamu ya tano zimezaa matunda hayo.

Alisema data za mwaka 2018 zinaonyesha kuwa tembo 12 walikufa kwa sababu mbalimbali, ikiwa ni wasiojulikana chanzo cha kifo inawezekana kuwa ni umri mkubwa (7), aliyeuawa kutokana na kuua mtu (1) na ugonjwa wa kimeta (4).

Aidha, tembo 22 waliokolewa kwa kupewa tiba mbalimbali na kwamba kwa wote mizoga yao ilikutwa ikiwa na meno yake yote, jambo ambalo ni kiashiria kuwa kwa sasa hakuna ujangili.

"Miaka mitatu iliyopita ilikuwa ni ngumu sana tembo afe alafu ukute meno yake, na ujangili ulishika kasi sana kiasi cha mamia ya tembo kuuawa huku mtandao ukihusisha watu wa ngazi ya chini hadi taifa," alibainisha.

Alisema takwimu za mwaka 2012 zinaonyesha tembo 64 waliuawa, lakini baada ya serikali kuimarisha vikosi na kuhakikisha taasisi zote zinashirikiana ujangili umeisha.

Kwa mujibu wa Mbanjoko, Julai 2018 hadi mwaka huu, jumla ya watuhumiwa 113 walikamatwa kwa makosa ya kuwinda wanyamapori kwa ajili ya kitoweo na biashara.

Alisema ujangili huo mpya

INAENDELEA UK. 8

# TPSF yaainisha mambo 7 muhimu miradi mikubwa

**Na Romana Mallya**

TAASISI ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), imeainisha mambo saba muhimu kwenye miradi mikubwa kama wa kufua umeme wa maji Bonde la Mto Rufiji.

Pia imeiomba serikali ihakikishe sekta binafsi inapewa kipaumbele wakati wa kuibuni na utayarishaji ili kuondokana na wazawa kuomba kazi kampuni za nje badala ya wao ndio wawe waajiri.

Mwenyekiti wa TPSF, Salum Shamte, aliyasema hayo Jumamosi katika warsha iliyoandaliwa na taasisi hiyo kujadili fursa za kibiashara kwa kampuni za ndani zinazotokana na mradi huo wa Mto Rufiji.

Shamte aliiomba serikali, itungwe sheria ya kuhakikisha miradi mikubwa wanapewa makandarasi wazawa sekta binafsi halafu wao kwa kushirikiana na serikali ndipo waite kampuni kutoka nje na kuwaajiri katika maeneo yenye upungufu wa wataalamu na siyo kama inavyofanyika sasa, Watanzania ndio wanaoomba kazi hizo.

"Ikibidi sheria hii wapewe makandarasi wa nje, iwe ni lazima waingie ubia na kampuni za ndani kwenye mradi. Hatuna uhakika kama mkataba mradi wa Mto Rufiji unamwajibisha kivipi kuhusu kutumia kampuni na huduma za Tanzania," alisema.

Shamte alitaja jambo jingine kuwa inasemekana Watanzania hawatumii nguvu kubwa na ujasiri katika kutafuta kazi kwenye miradi mikubwa ikilinganishwa na kampuni za nchi za jirani.

Lingine alilolisema ni haki ya kila Mtanzania hususan sekta binafsi kupewa taarifa za wazi namna ambavyo mkandarasi atakuwa anatoa kazi kwa kampuni za wazawa ili kusiwe na upendeleo.

"Suala la mitaji na utendaji kazi ni changamoto kubwa inayoondoa kampuni za wazawa kwenye ushindani, inabidi hili liangaliwe kwa jicho la uwekezaji ikibidi kuanzisha mpango wa kutoa dhamana ya serikali au kuwe na mfumo maalum wa kuwezesha dhamana hiyo kupatikana," alisema.

Shamte alisema uwajibikaji, umahiri, nidhamu, uaminifu wa kampuni za wazawa wakati wanapopata fursa kushiriki katika miradi mikubwa ni muhimu kwa sababu kumekuwa na malalamiko ya utendaji usioridhisha kwa baadhi yao.

Pia alisema pamoja na kwamba wanajadili fursa za mradi wa Mto Rufiji, lazima wazitazame kwa mapana yake kwa sababu mbali ya ujenzi wa bwawa, zipo fursa za kudumu zinazoibuliwa na mradi huo.

"Zipo fursa za kilimo, ufugaji na uvuvi kwa sababu bonde la mto Rufiji ni kubwa kupita mabonde yote Afrika Mashariki, moja ya changamoto ya kuliendeleza ni mafuriko kila mwaka, mradi huu wa umeme utayazuia, hivyo wakulima wataweza kulitumia kwa kilimo cha umwagiliaji wa kisasa, ufugaji wa kisasa na uvuvi kutakuwa na bwawa la takribani kilometa za mraba 1500," alisema.

Alitaja jambo lingine ni ushirikishaji wa Watanzania katika miradi mikubwa ni suala la wao kuomba kwa makandarasi kuja na kuwatangazia fursa bali liwe ni jukumu la serikali kuhakikisha maslahi ya sekta binafsi yanapewa kipaumbele

INAENDELEA UK. 8







Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Usajili huu Simba, Yanga uzingatie michuano Caf

**JUMAPILI** wiki hii Juni 30, ndiyo siku ambayo klabu zinazowakilisha nchi zao kwenye michuano ya kimataifa, Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika zinatakiwa ziwe zimekamilisha usajili wao.

Hiyo ni kwa mujibu wa Shirikisho la Soka Afrika (Caf), na tayari klabu husika hususan hapa nchini, Simba, Yanga, Azam FC na KMC zimekuwa katika mchakato wa kuimarisha vikosi vyao kuelekea michuano hiyo.

Ikumbukwe, Simba na Yanga zitaiwakilisha nchi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa wakati Azam na KMC zenyewe zikitakiwa kuhakikisha bendera ya Tanzania kwa upande Bara inapepea vema kwenye kitimtimu cha Kombe la Shirikisho Afrika.

Hii ni mara ya kwanza katika historia ya soka la Tanzania Bara, kuwakilishwa na timu nne kwenye michuano hiyo yenye utajiri mkubwa kwa ngazi ya klabu Afrika. Hivyo ni matarajio ya Nipashe kuona wawakilishi hao wa Tanzania Bara wakifanya usajili makini utakaowawezesha kufika mbali kwenye michuano hiyo na kuwa sehemu ya zitakazonufaika na utajiri huo.

Kama inavyofahamika, bingwa wa michuano hiyo huibuka na dola za Kimarekani milioni 2.5 (Sh. bilioni 5.7), huku mshindi wa pili akizawadiwa dola milioni 1.25 (Sh. bilioni 2.8 za Tanzania). Na si bingwa na mshindi wa pili tu ambaye huibuka na donge hilo nono, bali pia timu inayotinga nusu fainali huibuka dola 800,000 (Sh. bilioni 1.8) na robo fainali huzawadiwa dola 650,000 (Sh. bilioni 1.5), huku timu zinazoshika nafasi ya tatu na ya nne kwenye hatua ya makundi zikinufaika na utajiri huo wa Caf kwa kupewa dola 550,000 (Sh. bilioni 1.2).

Ndiyo maana tunatamani kuona wawakilishi wetu wakiongeza umakini zaidi katika kusainisha wachezaji kwa kutazama wenye sifa na viwango vya kutoa ushindani kwenye michuano hiyo.

Kwa miaka mingi Simba na Yanga zimekuwa na utamaduni wa kusainisha wachezaji kwa sifa ama kukomoana zenyewe kwa zenyewe, huku zikiwa hazizingatii mapendekezo ya makocha wao na matokeo ya usajili kama huo ni kocha kuchukua muda mrefu katika kukiandaa kikosi chake kwa kuweza kupata 'kombinesheni' inayoweza kumpa ushindi.

Aidha, wasiwasi wetu pia ni namna klabu mfano Yanga inavyosainisha wachezaji wengi, hiyo ikiwa ni dalili ya mabadiliko makubwa ambayo pia yatamchukua kocha muda mrefu kuweza kupata kikosi imara cha kwanza.

Nipashe tukiwa kama wadau na wazoefu wa michezo hususan soka, tulitarajia kuona wawakilishi wetu hao wakiziba mapengo na kuimarisha idara ambazo zilipwaya msimu uliopita na si kusainisha karibu kikosi kizima cha kwanza. Wawakilishi wetu hawana budi kutambua kuwa michuano wanayokwenda kushiriki ni mikubwa na migumu na inahitaji ubora wa mchezaji mmoja mmoja, lakini pia kucheza kitimu.


Simba msimu uliomalizika ilifanikiwa kufika robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika na kilichoisaidia ni kuweza kucheza kitimu zaidi kwani wapinzani wao licha ya kucheza kitimu walikuwa bora zaidi kwa upande wa uwezo binafsi wa mchezaji mmoja mmoja.

Ni wazi kwa klabu zetu hazina uwezo kifedha kushindana sokoni katika kuwania wachezaji bora na klabu kama Al Ahly, Esperance ama TP Mazembe, hivyo kinachoweza kuzibeba katika michuano hiyo ni kucheza kitimu zaidi, jambo ambalo linahitaji wachezaji kucheza kwa pamoja muda mrefu ili kuzoeana.

Pamoja na hilo, basi usajili huo hauna budi kumulikwa kwa kutazama wachezaji ambao wanaweza kuzibeba timu kwa uwezo wao binafsi badala ya kufanyika kwa mihemko zaidi kama tunavyoshuhudia kwa sasa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Stars iungwe mkono kwa matokeo yoyote inayopata

Na Adam Fungamwango

**JANA** Taifa Stars ilitupa karata yake ya kwanza kwenye michuano ya fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) 2019, dhidi ya Senegal katika mechi iliyochezwa saa 2:00 usiku kwa saa za Afrika Mashariki.

Timu hiyo ya Tanzania itakuwa na mechi zingine mbili dhidi ya Algeria na Kenya kwenye fainali hizo za Afcon zinazoendelea nchini Misri.

Na kama Stars ikifanya vizuri kwenye mechi hizo, basi itafuzu hatua ya robo fainali ya michuano hiyo mikubwa kabisa ngazi ya timu za taifa barani Afrika.

Wala nisipepese macho kusema kuwa Watanzania wengi hasa unapopita mitaani na kwenye mitandao ya kijamii wamegawanyika kuhusu timu yao ya taifa. Wa kwanza ni wale wazalendo ambao wao hawajali kama timu inapewa kipaumbele kushinda au la.

Wao ni Tanzania kwanza, wanachoishangilia ni timu yao ya taifa kwa hali na mali, na kwa matokeo yoyote yale yatakayotokea wao wako na timu yao tu. Ikifuzu watashangilia na kama haikufuzu wala hawatoona vibaya kwa sababu ni timu yao.

Kundi la pili ni wale wenye nongwa. Hawa wanachotaka au kuombea ni Stars kufungwa ili waanze kumnanga kocha Emmanuel Amunike kwa sababu zao tu za kuacha wachezaji ambao wao waliona wanafaa kuichezea, au wachezaji wanaowapenda wao.

Kundi la tatu ni wale ambao hawana uhakika na timu ya Tanzania kama inaweza kufanya vizuri au la.

Wanachofanya kwanza ni kuangalia kama itashinda na ikiwa hivyo basi watashangilia na kujifanya wao ndiyo mashabiki namba moja. Lakini kama timu ikipoteza basi wao ndiyo watakaoanza kutoa lawama kwa makocha, wachezaji na kila mtu ambaye wanaona anahusika kwenye kikosi hicho cha Taifa Stars. Hata hivyo makundi haya yote ni mashabiki wa timu ya taifa na ni Watanzania.

Ukiangalia katika makundi haya matatu, kundi linalotakiwa kuwa mfano wa kuigwa ni lile la kwanza. Kundi la pili na la tatu, wote wanatakiwa kuiga mfano wa kundi la kwanza la kuwa Watanzania kwanza.

Kama ni Mtanzania huwezi kuwa chochote kile zaidi ya hicho. Hata kama timu haitofanya vema basi kinachotakiwa ni kusikitika, lakini ukiendelea kuwa Mtanzania na si kuanza kulaumu na kutupia lawama watu.

Nasema hili kwa sababu mara nyingi kuna mazoea yamejengeka kuwa Stars ikishinda timu inakuwa ni ya wote. Ni ya Watanzania wote, huku kila mmoja akijiona ni mhusika wa mafanikio hayo.

Pongezi kwenda kwa wachezaji, makocha na hata Shirikisho la Soka nchini (TFF), zinakuwa hafifu, badala yake watu wanashangilia tu kana kwamba ushindi umeletwa hivi hivi. Inapokuwa kinyume chake sasa, mzigo anatupiwa kocha, wachezaji wa TFF.

Si kama kusiwe na ukosoaji kama timu inafanya vibaya. Ni lazima watu waseme tatizo liko wapi. Tatizo ni pale ukosoaji huo hauwi wa kujenga, bali ni kama kusuta, kushutumu na kuhukumu.

Binafsi, kwa hapa Stars ilipofikia ni mafanikio makubwa kwenye soka la nchi yetu, kwani baada ya miaka 39, timu hiyo imefuzu na inacheza michuano hiyo baada ya miaka 40.

Kwa maana hiyo naona kuingia kwa mara ya kwanza baada ya miaka hiyo ni kwenda kusaka uzoefu na si kuwaweka wachezaji roho juu na kujiaminisha kuwa wanatakiwa kulitwaa kombe hilo au kufika nusu fainali.

Ni kama Klabu ya Simba ilivyofanya mwaka huu kuwa lengo lake ilikuwa ni kutinga makundi, hivyo kufika hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa ilikuwa ni kuvuka malengo waliyojiwekea.

Stars nayo ni hivyo hivyo, lengo lilikuwa ni kufuzu AFCON na tayari imefanya hivyo, hivyo hakuna sababu ya kuihukumu pale kwa bahati mbaya itakaposhindwa kufuzu kwenda hatua inayofuata.

Na kama ikifanikiwa basi itakuwa imevuka malengo na hakuna haja ya kumshika mtu uchawi.

Kwa sasa Watanzania wote wapenzi wa soka wanatakiwa kuungana na kuwa kitu kimoja kuiombea Taifa Stars ifanye vema, lakini pia kukubali matokeo yoyote yale yatakayotokea bila kushusha lawama zisizo na msingi. Ikishinda tufurahi wote na ikifungwa tuhuzunike wote.

## MJADALA/BARUA

# *Mamlaka zikiangalie kituo cha daladala Basihaya*

***Mhariri,***

*NINALIPONGEZA sana gazeti lenu kwa kuandika habari ambazo zinagusa sana maisha ya wananchi, hususan kero mbalimbali zinazotokea katika jamii yetu hii ya Kitanzania.*

*Baada ya pongezi hizi, ninawasilisha kwako kero kubwa inayotusumbua watumiaji wengi wa Barabara ya Bagamoyo. Katika siku za karibuni, eneo la Boko Basihaya limekuwa likisababisha foleni, kutokana na kituo cha daladala.*

*Hali hiyo imekuwa ikisababisha magari yanayotoka Tegeta kukumbwa na foleni kuanzia Namanga au Nyaishozi.*

*Kwa magari yanayotoka Bunju na Mbweni kwenda Tegeta yamekuwa yakikwama kuanzia Chama, hivyo abiria kutumia muda mrefu kutokana na usumbufu huo.*

*Kimsingi, foleni hiyo inasababishwa na kituo cha daladala cha Basihaya kuwa katika eneo lisilofaa kabisa. Ninasema hivyo kwa sababu kimeingia kabisa ndani ya barabara na kusababisha magari mengine kushindwa kupishana.*


*Hali hiyo ilichangiwa zaidi baada ya kuongezeka kwa idadi ya magari hususan mabasi makubwa ya mikoani yalipoanza kutumia njia hiyo kwenda mikoa ya Kanda ya Kaskazini.*

*Pia kituo hicho ni njia panda, kwa kuwa kuna barabara inayotokea Ununio na maeneo mengine ya Tegeta na nyingine inaingia eneo la chuo binafsi.*

*Ninaziomba mamlaka husika zifuatilie kero hii na kuitafutia ufumbuzi ili kuwapunguzia watumiaji wa barabara hiyo usumbufu wa kupoteza muda mrefu wa kukaa katika foleni.*

*Ushauri wangu ni kuwa kero hii inaweza kupatiwa ufumbuzi wa kudumu iwapo kituo cha daladala cha Basihaya kitaondolewa na kuwekwa eneo zuri ambalo ni rahisi magari kupishana bila ya usumbufu wowote.*

# KMC waulizeni Mtibwa shughuli ya Shirikisho




**Na Adam Fungamwango**

BAHATI ya mtende kuota jangwani iliwaangulia vijana wa KMC, klabu inayomilikiwa na Manispaa ya Kinondoni kupata tiketi ya kucheza Kombe la Shirikisho Afrika msimu ujao.

Kikosi cha KMC kilikamata nafasi ya nne, na kikiwa hakina hili wala lile, kikajikuta kinatakiwa kucheza Kombe la Shrikisho.

Ni baada ya Shirikisho la Soka Afrika (Caf) kulijulisha Shirikisho la Soka nchini (TFF) kuwa msimu ujao Tanzania inatakiwa iwe na timu nne; mbili Ligi ya Mabingwa na idadi kama hiyo Kombe la Shirikisho, badala ya zamani ambako kulikuwa na timu moja kwenye kila michuano hiyo miwili.

TFF haikuumiza kichwa sana, ilichofanya ni kumchukua bingwa ambaye ni Simba na mshindi wa pili, Yanga kuiwakilisha nchi kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika.

Nafasi ya mshindi wa tatu ilichukuliwa na Azam FC ambayo ilipaswa moja kwa moja icheze Kombe la Shirikisho, lakini kwa bahati nzuri kwao ilikuwa tayari imeshakata tiketi hiyo ilipitia mgongo mwingine wa kuwa bingwa wa Kombe la FA ambao hutoa nafasi ya kushiriki moja kwa moja michuano hiyo.

Ilichofanya TFF ni kuichukua timu iliyokamata nafasi ya nne ili ichukue nafasi ya Azam FC ambayo ina tiketi kupitia FA.

Hapo ndipo KMC ikapata nafasi hiyo ya kushiriki michuano hiyo mikubwa barani Afrika kwa ngazi ya klabu. Timu hiyo ilipanda na kuanza kucheza Ligi Kuu kwa mara ya kwanza msimu huu.

Kwa ninavyoona ni kama vile KMC ilishtukizwa na haijajipanga kwa dhati haswa kucheza Kombe la Shirikisho. Naona kama hata usajili wake ni ule ule kama wa kutaka kucheza Ligi Kuu tu msimu ujao na si kwenda kucheza mechi za kimataifa.

Ni kweli imefanikiwa kuwasainisha au kuwabakisha wachezaji wake wengi waliocheza msimu uliopita ambao walikuwa wanawaniwa na klabu mbalimbali kubwa nchini, akiwamo kipa mkongwe na mzoefu nchini, Juma Kaseja.

Kwa sasa imebaki wiki moja tu kumalizika kwa usajili wa michuano hiyo ya kimataifa, Juni 30, mpaka sasa bado sijaona jina, au mchezaji ambaye kweli unaweza kusema kuwa huyu anaisaidia timu hiyo kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho zaidi ya kipa Kaseja ambaye ni mzoefu.

Sijaona mchezaji kutoka nje ya nchi ambaye wamemsainisha unayeweza kusema kuwa KMC ni kweli imedhamiria kwenda kupambana kimataifa.

Unaweza ukaona jinsi Klabu za Simba, Yanga na hata Azam zinavyosainisha wachezaji bora na hivyo kuonekana wamejiandaa kwenda kukambiliana na mechi za kimataifa.

Pamoja na kusaini wachezaji wapya, lakini pia bado timu hizo zina wachezaji ambao ni wazoefu na wameshacheza michuano hiyo kuanzia msimu ulioisha na hata mingine iliyopita.

Hata Azam ina wachezaji kama Obrey Chirwa, Donald Ngoma na wengine ambao wameshakumbana na misukosuko ya michuano ya Ligi ya Mabingwa na Shirikisho.

Kama viongozi wa KMC wanaona wanaweza kwenda kupambana na timu zingine wakiwa na aina hiyo ya wachezaji basi wanajidanganya.

Kombe la Shirikisho halitofautiani kabisa na Ligi ya Mabingwa kwa sababu kuna timu bora, nzuri na ngumu zinapata bahati mbaya ya kutolewa na kuangukia huko. Ugumu wa michuano unakuwa ni ule ule.

Msimu uliomalizika tuliona timu ngumu kama Nkana FC ikitolewa na Simba na kushuka kwenye Kombe la Shirikisho, Gor Mahia, Zamaleki ambao ndiyo mabingwa, Asante Kotoko, Al Hilal na timu nyingine nyingi.

KMC iiulize Mtibwa Sugar ilichokipata msimu uliopita kwani pamoja na kuwa na wachezaji wazuri, lakini ilijikuta ikitolewa kwenye raundi ya kwanza na KCCA ya Uganda kwa kuchapwa mechi zote mbili ilipochapwa mabao 2-1 nyumbani, kabla ya kutandikwa 3-0 ugenini.

Kilichowaondoa Mtibwa si tu kwamba hawakuwa na wachezaji wazuri wa kigeni, lakini pia haikuwa na wachezaji wazoefu wa kiwango cha michuano hiyo.

Kama kweli KMC inataka kufanya vizuri kwenye michuano hiyo na si kusindikiza, basi kwa kipindi hiki kilichosalia cha usajili itafute wachezaji wa kigeni angalau hata watatu wenye viwango vya juu, lakini pia wachezaji wengine wa ndani wenye uzoefu wa mechi za kimataifa. Vinginevyo itaingia kwenye michuano hiyo na kucheza kwa kubahatisha kama ilivyokuwa kwa Mtibwa Sugar msimu uliomalizika.

## KABWELA NA FADHIL MOHAMMED




## WASILIANA NASI:

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz

# Walengwa uboreshaji wa Daftari Mpigakura

INATOKA UK. 2

fomu namba moja na uchukuaji alama za vidole, picha na saini litaendelea na atapatiwa kadi mpya," alisema.

Kuhusu wale waliopoteza kadi au wale zilizoharibika, Dk. Kihamia alisema watajaza fomu namba 5A na kuipeleka kwa BVR (kit operator) ili kupatiwa kadi mpya.

"Katika uboreshaji wa daftari, wapigakura ambao watakuwa wamepoteza sifa za kuendelea kuwapo kwenye daftari mfano waliofariki, wanatakiwa kuondolewa, watu wenye taarifa kuhusu watu hao wanatakiwa kuzipeleka katika vituo vya uandikishaji kipindi cha uboreshaji na kujaza fomu namba 5B," alisema.

Alisema Ofisa Mwandikishaji atazi-wasilisha fomu hizo tume kwa sababu ndiyo yenye jukumu la kuwaondoa watu hao waliopoteza sifa.

Alisema baada ya uboreshaji kukamilika, NEC itaandaa Daftari la Wapigakura ambalo litatumika katika uchaguzi.

"Tume itakuwa na utaratibu wa kutoa nakala ya Daftari la Wapigakura kwa vyama vya siasa kabla ya uchaguzi mkuu, baada ya kukamilisha kila chama cha siasa kitapewa nakala yake," alisema.

# Vituo vinne vyaanzishwa

INATOKA UK. 4

72,000 hupata maambukizi mapya ya VVU kila mwaka, ambapo takriban watu milioni 1.5 wameambukizwa na VVU huku wastani wa hali ya maambukizi ikiwa ni asilimia 4.7 kwa Tanzania Bara," alisema.

Aidha, alisema wakati maambukizo hayo yakipungua kwa ujumla wake kwa Watanzania yapo makundi ambayo maambukizi yamekuwa yakiongezeka husasan kwa vijana kati ya miaka 15 hadi 24.

"Makundi mengine yaliyoko kwenye mazingira hatarishi ni kama vile wasafirishaji wa masafa marefu, watu wanaotumia dawa za kulevya, wanaofanya mapenzi kinyume na maumbile, wanawake wanaofanya biashara ya ngono, wafanyakazi kwenye migodi, wavuvi, wafanyakazi kwenye mashamba makubwa.

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira, alisema jukumu lililoko ni kuwapo kwa ushiriki mpana wa wadau katika sekta zote ikiwamo sekta binafsi ndiyo maana serikali ikaanzisha Mfuko wa Ukimwi. "Mfuko huo unalenga kuokoa kizazi chetu, kulihakikishia Taifa upatikanaji wa dawa za kufubaza VVU na kuweka mkazo ili watu wote wapime na wanaobainika kuwa wameambukizwa waanze kutumia dawa mapema na kuwa na ufuasi mzuri ili kuendelea kuishi maisha ya kawaida na kutumikia taifa," alisema.

Makamu wa Rais wa GGM, Simon Shayo, alisema GGM itaendelea kushirikiana na TACAIDS kwa kuwashirikisha wadau wa Ukimwi kutoka ndani na nje ya nchi ili washiriki kikamilifu kwenye afua mbalimbali za udhibiti wa Ukimwi zikiwemo za kinga, kufanya utafiti mbalimbali, matunzo kwa wagonjwa Ukimwi, WaVVU, watoto yatima na kuweka mazingira wezeshi.

"Ndiyo maana GGM tulianzisha programu ya Kilimanjaro Challenge Against HIV and AIDS miaka 17 iliyopita ambayo sasa imekusanya zaidi ya Sh. bilioni 13 ambazo zimenufaisha taasisi mbalimbali 40 zinazotoa huduma za VVU na Ukimwi pamoja na Mfuko wa Ukimwi (ATF).

"Pia imesaidia uendelezaji na uendeshaji wa kituo cha watoto yatima Geita (Moyo wa Huruma Orphanage Centre), Utoaji huduma za Ukimwi kwa wasafirishaji wa masafa marefu na jamii zinazoishi kwenye maegesho hatarishi na misaada kwa kupunguza athari za ugonjwa huo kwa wajane na watoto yatima kuwapatia vifaa vya elimu," alisema.

Timu ya wapandaji 31 wa Kili Challenge iliyoongozwa na Kapteni Moses Rusasa ilifika kileleni, 32 walitumia baiskeli waliongozwa na Kapteni Masolwa Bukelebe kupitia milima na mabonde.

# TPSF yaainisha mambo 7

INATOKA UK. 5

wakati wa kubuni na kuitayarisha.

Jambo lingine ni lazima kuwapo ufuatiliaji wa tathmini unaofanywa kwa pamoja na serikali, sekta ya umma kama Tanesco au Ewura na sekta binafsi kuhusu ushirikishwaji wao katika utekelezaji wa miradi mikubwa.

Mhandisi Edward Ishengoma kutoka Wizara ya Nishati, alizitaka kampuni za kizawa zitakazopata fursa kwenye mradi huo zihakikishe zinatoa huduma nzuri zenye kuridhisha.

Alisema mradi huo ambao utatekelezwa kwa miaka mitatu unatarajia kutoa ajira kwa watu 6,000, ambapo fursa zilizopo kwa wazawa ni huduma mbalimbali za kibinadamu ikiwamo chakula, sehemu za kulala na vifaa vya ujenzi.

Mratibu wa mradi huo wa Mto Rufiji, Justus Mtolera, akizungumzia kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme (Tanesco), Dk. Tito Mwinuka, alizitaka kampuni za wazawa zihakikishe kuwa zipo vizuri kivifaa, ziwe na wafanyakazi wa kutosha na ziwe zimesajiliwa.

# Ujangili meno ya tembo

INATOKA UK. 5

kwa sasa unashika kasi baada ya ujangili wa tembo na faru kupigwa mafuruku na kubomoa mtandao, na sasa watu wanaua wanyama kwa ajili ya kusafirisha nyama nje ya nchi.

Kamanda huyo alisema jitihada zinazofanywa na kikosi kwa kushirikiana na wasamaria wema, ni kumaliza mtandao wa biashara hiyo ikiwa ni pamoja na kesi zote kushughulikiwa ipasavyo.

Alitaja vifaa walivyokamatwa navyo watuhumiwa hao kuwa ni pikipiki (40, nyaya (117), mishale (6), tochi (24), visu (25) na nyara mbalimbali (306) na kesi mbalimbali zinaendelea mahakamani na nyingine zimeshaamuliwa.

# Lipumba aishauri serikali kukopa BoT

INATOKA UK. 2

kuwa kilimo ndio tegemeo la wananchi wengi na kuwa bila kuwekeza katika kilimo ni vigumu kupiga hatua katika sekta ya viwanda.

"Nimekuwa napitia kitabu cha hali ya uchumi wa taifa kuna jedwali humu la 24 ukilifanyia kazi unakuta mwaka wa fedha 2017/2018 huwezi ukaamini kwenye kila Sh. 100 iliyotumiwa na serikali fedha iliyokwenda kwenye sekta ya kilimo ni

Sh. 1, huwezi ukaamini mpaka nikadhani labda walikosea nikafanya hesabu napata hiyo hiyo asilimia moja," alisema.

**JIBU LA BoT**

Gazeti lilimtafuta Gavana wa BoT, Prof. Florens Luoga, ili kutoa ufafanuzi wa hoja ya Prof. Lipumba, alitaka atafutwe Meneja msaidizi wa Benki hiyo ili atoe ufafanuzi na alipotafutwa Meneja Msaidizi, Zalia Mbeo, akisema hoja hiyo inaihusu serikali na kuwa ndio inayoweza kutoa ufafanuzi wa suala hilo.

"Kwa kuwa ameishauri serikali basi ungeitafuta serikali ndio inaweza kuwa na majibu mazuri," Zalia alisema.

**UCHAGUZI WA MWAKANI**

Kuhusu Uchaguzi Mkuu wa 2020, Prof. Lipumba alisema chama hicho kitaendelea kudai demokrasia ya kweli na kuwa Malengo ya

Maendeleo Endelevu (SDGs) yatakuwa sehemu ya sera na pia ilani ya uchaguzi ya chama hicho.

"Kama kuna demokrasia ya kweli uko salama wakati unatoka madarakani, lakini pakiwa hakuna demokrasia ya kweli, mambo yanaweza kugeuza kibao, uliyokuwa unayafanya mazuri ya kutetea rasilimali ili zitumiwe kwa manufaa ya Watanzania mambo hayo yakageuzwa," alisema.

**WAPOKEA CHADEMA, ACT**

Katika mkutano huo pia chama hicho kilipokea wanachama kutoka vyama viwili vya upinzani wengi wao kutoka Chama cha ACT-Wazalendo na wengine kutoka Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema).

# Hoja 10 zinazosubiri majibu ya Mpango mjadala bajeti

INATOKA UK. 2

kuitengea kiasi kidogo cha fedha.

Mbunge wa Mtama (CCM), Nape Nnauye aliyeeleza: "Kilimo kinazalisha ajira asilimia 65 na asilimia 85 ya bidhaa tunazouza nje zinatokana na kilimo. Kilimo kinachangia pato la taifa kwa asilimia 29 na asilimia zaidi ya 100 chakula nchini kinategemea kilimo,"

"Lakini ukiangalia mtiririko wa bajeti mwaka 2016/17 bajeti ya maendeleo katika kilimo tulitenga asilimia 1.38, mwaka 2017/18 tukatenga asilimia 1.25 na 2018/19 tukatenga asilimia 0.81 na 2019/2020 tumetenga asilimia 1.17 na hizi fedha zimetengwa tu bado hazijapelekwa."

**TAULO ZA KIKE**

Uamuzi wa serikali kurejesha Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwenye taulo za kike ni moja ya hoja iliyowagusa wabunge karibu wote, lakini kubwa ni Mbunge wa Kigoma Mjini (ACT-Wazalendo), Zitto Kabwe, kupinga pendekezo la serikali la kurejesha kodi, akiamini ni uamuzi wa haraka na unaharibu sifa ya Tanzania.

Katika mapendekezo hayo ya bajeti ya Sh. trilioni 33.1, serikali imeweka wazi kuwa ina mpango wa kurejesha VAT kwenye taulo za kike iliyoifuta mwaka jana kwa kuwa uamuzi wake huo haukufanikiwa kupunguza bei ya bidhaa hiyo muhimu.

Baadhi ya wabunge wamedai kuwa serikali ilikuja na pendekezo kwenye Bunge ili kuweza kuleta unafuu kwa wanawake milioni 13 katika matumizi ya taulo za kike kwa kila mwezi na kwa mwaka huu, wanashangaa ni kwa nini serikali imeona kwamba pendekezo lile halijaleta yale matokeo ambayo ilikuwa inayataka.

Kwa upande wake, Mbunge wa Mtwara Vijijini (CCM), Hawa Ghasia, alisema njia pekee ya kumsaidia mwanamke na mtoto wa kike kwenye bidhaa hizo ni serikali kuhakikisha inasimamia viwanda vya ndani ili taulo hizo zizalishwe kwa wingi na kwa bei nafuu.

**MAFUTA YA KULA**

Kuhusu pendekezo la serikali la kuongeza kodi kwenye mafuta ghafi yanayotoka nje ya nchi ili kulinda wazalishaji wa mbegu za mafuta hapa nchini, baadhi ya wabunge waliochangia mjadala huo wa bajeti wameeleza kuwa bado uzalishaji unashuka na kuna haja serikali ikafanya mapinduzi zaidi ya kulinda soko.

**GHARAMA ZA MAISHA ZANZIBAR**

Katika mjadala huo, baadhi ya wabunge akiwamo Mbunge wa Welezo Zanzibar, Saada Mkuya (CCM) alieleza masikitiko yake kwamba bidhaa zinazoingia kutoka Bara kwenda Zanzibar zinatozwa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) na zikifika tena Zanzibar zinatozwa kodi na Mamlaka ya Mapato Zanzibar, jambo linawakwaza wafanyabiashara na kutikisa mitaji yao.

**SUALA LA PPP**

Hoja kuhusu ushirikiano kati ya serikali na sekta binafsi lilikuwa miongoni mwa mambo yaliyoguswagusswa na baadhi ya wabunge akiwamo Mbunge wa Momba (Chadema), David Silinde, aliyetaka serikali kutambua kuwa maendeleo ya nchi hayategemei kukusanya kodi.

Alisema maendeleo hutegemea kuboresha uwekezaji wa moja kwa moja na ushirikiano wa sekta binafsi na umma (PPP).

"Duniani kote maendeleo ya nchi hayategemei kodi pekee, nasema hivi kwa sababu wimbo humu ndani (bungeni) ni kodi tu. Nchi nyingi hutumia kodi kwa matumizi mengineyo na kulipa mishahara," ameeleza Silinde.

**TAASISI ZENYE MAJUKUMU YANAYOFANANA**

Pamoja na mambo mengine, wakati wa mjadala huo, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti ilitoa mapendekezo yake yaliyogusa wabunge wengi ambao wameitaka serikali iharakishe mchakato wa kuziunganisha taasisi zote zenye majukumu yanayofanana ya ukaguzi kwenye bidhaa, kampuni, taasisi na maeneo ya viwanda nchini ili kuondoa kero na usumbufu unaojitokeza.

Taasisi ambazo Bunge limeekeleza serikali kuziunganisha ni Shirika la Viwango nchini (TBS), Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA), Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) na Jeshi la Zimamoto na Uokozi.

# TBS yatoa matakwa ya msingi kwa wazalishaji mifuko mbadala

**Na Felix Andrew**

SERIKALI imetoa matakwa ya msingi ambayo wazalishaji, wasambazaji na wauzaji wa mifuko mbadala wanatakiwa kuyafuata ili kuwawezesha kufanya shughuli zao.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Dk. Yusuf Ngenya, alitaja matakwa kwa bidhaa hiyo kuwa ni uzito usiopungua GSM 70.

Matakwa mengine ni kuwa yenye kurejelewesha (recyclable), kuwa na anuani ya mzalishaji au nembo ya biashara (trademark).

Alisema kuwa mifuko inatakiwa kuonyesha uwezo wake wa kubeba na iwe imethibitishwa ubora wake na Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

Dk. Ngenya alisema hakuna mfuko wowote utakaoruhusiwa kuingia au kuzalishwa nchini kama hautakidhi matakwa yalioyotajwa.

Alitoa onyo kwa watakaoendelea kuzalisha, kusambaza na kuagiza mifuko hiyo kinyume cha utaratibu ulioainishwa kuwa hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

Aliwaasa wazalishaji , wasambazaji na waagizaji wa vifungashio na vibebeo ambavyo vimeruhusiwa kisheria kuwasiliana na shirika hilo ili kuthibitisha bidhaa zao na kupata leseni ya ubora wa mifuko ambayo italinda afya ya mtumiaji na mazingira ya Tanzania.

Hivi karibuni shirika hilo lilitangaza kuanza kutumika kwa kiwango kipya cha lazima cha mifuko mbadala.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Lazaro Msasalaga, alikaririwa akisema kiwango hicho ni TZS 2292: 2018 na TZS 2130: 2018.

Aliwataka wazalishaji wa mifuko mbadala nchini kuanza kupeleka maombi kwa ajili ya leseni za kazi zao.

Alisema shirika bado halijapokea maombi juu ya utengenezaji wa vifugashio na mifuko mbadala tangu katazo la mifuko ya plastiki lilipoanza kutumika wiki iliyopita.

Msasalaga alisema katika kuungana na serikali wao kama Shirika la Viwango limechukua hatua tatu muhimu kwa wazalishaji wa vifungashio vilivyopigwa marufuku.

"TBS limesitisha uhuishaji wa ubora kwa wazalishaji wa aina hiyo ya bidhaa ya vifungashio, kutopokea maombi mapya ya uzalishaji wa vifungashio pamoja na kuondoa katika matumizi kwa kiwango kilichokuwa kinatumika cha plastiki," alisema.

Aidha, Msasalaga ambaye pia ni Kaimu Mkurugenzi Udhibiti Ubora, aliwatahadharisha wote wanaotumia vibaya nembo ya shirika hilo endapo watakutwa sheria kali itachukuliwa.

Mifuko ya plastiki ilipigwa marufuku kuanzia Juni mosi mwaka huu ambapo sheria kali zitachukuliwa endapo yoyote atakayekutwa anatumia au kuuza bidhaa hizo atapigwa faini au jela au vyote kwa pamoja.

Kifungu au kanuni namba 8 ya sheria ya kuzuia matumizi ya mifuko plastiki ya mwaka 2019 kinatanabaisha juu ya makosa yatokanayo na uingizaji, kusafirisha nje ya nchi, kuagiza, kuhifadhi na kuagiza, kifungu hiki kinakataza uingizaji wa bidhaa hizo.



Kaimu Mkurugenzi Mkuu, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Vupe Ligate (kulia), akimuhudumia mstaafu na mwanachama wa mfuko huo, Shayo, wakati wa Wiki ya Utumishi wa Umma jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TPB yapiga jeki shule

**Restuta Damian,** KARAGWE

JUMLA ya wanafunzi 120 wa Shule ya Msingi Rumanyika Kata ya Kayanga, Wilaya ya Karagwe mkoani Kagera, husomea katika chumba kimoja kutokana na ukosefu wa vyumba vya madarasa.

Hayo yalisemwa na mkuu wa shule hiyo, Ebearth Kasenene, wakati wa mapokezi ya vifaa vya ujenzi vyenye thamani ya Sh. milioni nne, saruji mifuko 100 na bati 60 kutoka Benki ya TPB, ili kuendeleza ujenzi wa vyumba vya madarasa mawili ili kupunguza mrundikano wa wanafunzi.

Kasenene alisema uongozi wa shule umelazimika kufanya hivyo kutokana na wingi wa wanafunzi katika Shule ya Msingi Kambarage na Rumanyika, ambazo kila moja ina zaidi ya wanafunzi 1,000.

Alisema ili kukabiliana na changamoto, uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe umeamua kujenga shule ambayo itasaidia kupunguza idadi kubwa ya wanafunzi madarasani.

Alisema kwa hali hiyo uelewa wa wanafunzi unakuwa mdogo kutokana na walimu kushindwa kumfikia kila mwanafunzi.

Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Godwin Kitonka, alisema shule hiyo iko katika mazingira magumu ya wanafunzi 180 walitolewa katika shule za Kambarage na Rumanyika kusoma katika mrundikano.

Kitonka alisema hatua zinazofanywa na halmashauri ni kutafuta wahisani ambao watashirikiana kusaidia jamii kama kuunga mkono shughuli za ujenzi wa miundombinu.

Alisema fedha za mapato ya ndani hazikidhi mahitaji ya sekta za elimu na afya.

Mwenyekiti wa Bodi ya TPB, Edmundi Mndolwa, alisema kwa kutambua umuhimu wa elimu na afya, ndiyo maana wameamua kusaidia jamii.

# WMA yaendelea uhakiki, elimu ya mizani

**Na Mwandishi Wetu,** TABORA

WAKALA wa Vipimo (WMA) mkoani Tabora, unaendelea kufanya uhakiki wa mizani kwa vyama vya ushirika vya msingi (AMCOS) sambamba na elimu ya matumizi sahihi ya mizani nchini.

Hatua hiyo imelenga kuwalinda wakulima wa pamba waweze kupata faida kwa kuuza mazao yao kupitia vipimo na mizani sahihi iliyohakikiwa na WMA.

Hayo yalielezwa na Meneja wa WMA Mkoa wa Tabora, Mrisho Mandari, mwishoni mwa wiki, ambapo alisema wamefanya uhakiki wa mizani ya AMCOS katika wilaya tano za Igunga, Nzega, Uyui, Urambo pamoja na Kaliua.

Mbali na uhakiki, alisema wanatoa elimu ya matumizi sahihi ya vipimo kwa wakulima wa pamba na wananchi wote waweze kutambua mambo muhimu ya kuzingatia wanapokwenda kuuza pamba katika vituo maalum.

"Niwaase wakulima wawe makini pindi wanapokwenda kuuza pamba kwa kuhakiksha mizani unasoma sifuri kabla ya kuanza upimaji kwa ile mizani ya digitali.

"Baada ya kupima furushi la pamba mizani inatakiwa kurudi katika sifuri na wahakikishe mizani haisomi hasi (-) baada ya kutoa mzigo na ikitokea hivyo wamwambie karani anayesimamia mizani kuizima na kuiwasha tena ksha upimaji uendelee," alisisitiza Mandari.

Meneja huyo aliongeza kuwa ili kuboresha ulinzi wa mizani iliyohakikiwa na kukidhi vigezo vya kutumika katika ununuzi wa pamba, wanaweka stika maalum ya WMA pamoja na kufunga lakiri katika maeneo muhimu ya mizani kuzuia kuchakachuliwa na wafanyabiashara wasiokuwa waaminifu.

Mandari alisema katika wilaya zote walizofanyia uhakiki, mizani 158 imehakikiwa na kusambazwa kwenye vituo vyote vya kununulia pamba mkoani Tabora.

Alisema kati ya mizani 158 iliyohakikiwa, 130 haikubainika na tatizo lolote, na 18 ilikutwa na hitilafu ndogo ndogo ambazo zilirekebishwa, huku 16 zilifikia viwango vya usahihi. Aisha aliongeza kuwa mizani miwili ilikataliwa kabisa kutumika kutokana na kuwa na matatizo makubwa, na kuwaonya wanunuzi wa pamba kujiepusha na vitendo vya dhuluma kwa wakulima kwa kutumia mizani ambazo hazijahakikiwa na kupata idhini ya kutumika katika msimu husika.

"Niwakumbushe wanunuzi wa pamba kwamba kwa sasa sheria ya vipimo sura Na.340 na mapitio yake ya mwaka 2002 imefanyiwa marekebisho na adhabu zimekuwa kali, ambapo ukikutwa na kosa la kuchezea mizani na ukakiri kosa faini yake ni kati ya Sh. milioni 20 kwa kosa la kwanza na Sh. milioni 50 kwa mkosaji wa kosa la kujirudia," alisema Mandari.

Uhakiki wa mizani na utoaji elimu kwa wakulima wa pamba ni zoezi endelevu ambalo hufanywa mara kwa mara, ili kuwalinda wakulima na hufanyika kabla ya msimu wa ununuzi wa pamba na hufanywa na maofisa wa WMA kwa kupita katika vituo mbalimbali vinavyotumika kununulia pamba na mazao mengine kama tumbaku, ufuta, kahawa na korosho.

# Onyo kwa wanaochakachua tumbaku

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

SERIKALI imesema kuwa, itawachukulia hatua za kisheria wakulima wa tumbaku ambao wamekuwa na tabia ya kuchanganya tumbakusafi na chafu kwa ajili ya kujipatia kipatao ambacho sio halali kwao.

Onyo hilo ilitokana na mkulima wa zao hilo, Majaliwa Joseph Masaluta, kutoka chama cha msingi cha Mweli, aliyekuwa na marobota 50 ya tumbaku yenye kilo 500 ya zao hilo na kubainika akiwa amechanganya tumbakusafi na chafu kisha kuyapeleka sokoni.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Mkuu wa Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga, Anamringi Macha, wakati akizungumza na vyombo vya habari, na kusema kuwa hali hiyo imekuwa ikiharibu taswira ya Tanzania kuwa tumbaku chafu inayozalishwa inatoka katika mkoa wa kitumbaku Kahama.

Aidha, Macha alizitaka mamlaka zinazosimamia zao hilo ikiwamo Bodi ya Tumbaku kuwachukulia hatua za kisheri wakulima ambao wamekuwa na tabia ya kufanya udanganyifu kwa kufunga tumbakusafi na chafu sehemu moja kwa lengo la kujinufaisha kwa maslahi yao binafsi.

“Wakulima ambao walilima tumbaku walikuwa 4,670 na walelima hekta 5,888 na wamezalisha zaidi ya kilo milioni 8.1, lakini baadhi yao wamekuwa wakichanganya tumbakusafi na chafu kwenye belo moja, hali ambayo imekuwa ikichafua taswira ya nchi kuwa tumbaku chafu inatoka mkoa wa kitumbaku Kahama,” alisema.

Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika KACU wilayani hapa, Emmanuel Charahani, alikiri kuwapo kwa vitendo hivyo, ambavyo vimekuwa vikijitokeza kila msimu wa uuzaji wa tumbaku nakuongeza mwaka huu wamemkamata mkulima mmoja kutoka chama cha msingi.

Alisema alikuwa na tumbaku mabelo 50 yenye zaidi ya kilo 500 ambayo yalibainika kuwa na mchanganyiko wa tumbakusafi na chafu na kwa hatua ya awali tumbaku hizo zimeondolewa kwenye soko kwa ajili ya ukaguzi wa kina na ikibaika ni mabelo yote atafutiwa kibali cha uzalishaji wa zao hilo.

Charahani alisema chama cha msingi ambacho kilikuwa kinamsimamia kimetozwa faini ya Sh. 300,000 kwa kushindwa kumsimamia vema katika ufungaji wa mabelo hayo pamoja na kuandika barua ya kujielekeza.



Mfanyakazi wa Airtel akimuhudumia Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, ili kuhakiki usajili wa laini yake ya Airtel kwa kutumia alama za vidole ofisini kwake jijini Dar es salaam mwishoni mwa wiki, ambapo Airtel inaendelea na zoezi la usajili na uhakiki wa laini za simu kwa kutumia alama za vidole kama ilivyoagizwa na Mamlaka ya Mawasiliano TCRA kuwa hadi kufikia Desemba 2019 laini zisizohakikiwa kwa mfumo wa alama za vidole (Biometria) zitafungwa. Kulia ni Meneja Matukio Airtel Tanzania, Dangio Kaniki. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Wadau wafagilia uanzishwaji mabaraza ya ujuzi ya kisekta

**Na Elizabeth Zaya**

WADAU kutoka sekta za uchumi nchini wamepongeza hatua ya serikali na taasisi ya sekta binafsi kuanzisha mabaraza ya kisekta ya ujuzi kwani hiyo ni ishara njema kwa ujenzi wa sekta ya viwanda.

Wamesema hatua ya kuanzisha mabaraza hayo ni chanya na itawasaidia wahitimu kuwa na uwezo wa kujiamini na kutoa mchango mkubwa wanapokuwa katika ajira.

Mkuu wa Chuo cha Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), Prof.

Preksedis Ndomba, alisema, kuanzishwa kwa mabaraza hayo ni fursa pekee kwa chuo chake kunufaika na huduma ya mabaraza hayo.

“Serikali ya awamu ya tano chini ya Rais John Magufuli kwa kushirikiana bega kwa bega na sekta binafsi imeonyesha njia, hivyo ni jukumu la wadau kutoka sekta mbalimbali kuunga mkono jitihada hizo, ili kutimiza azma ya serikali ya viwanda ifikapo 2025,” alisema.

Mwekezaji wa ndani katika sekta ya nishati mbadala, Hilary Biduga, alisema yeye kama mwekezaji anahitaji wafanyakazi wenye ujuzi ili kufanikisha azma yake, hivyo mabaraza hayo yatachochea ukuaji na maendeleo ya sekta mbalimbali.

“Nikiwa kama mdau wa maendeleo na mwekezaji wa ndani, hatua iliyofikiwa na serikali na sekta binafsi kuanzisha mabaraza ina lengo jema kwa nchi, kwani kupitia mabaraza haya vijana wataleta ushindani katika soko la ajira,” alisema Biduga.

Mkurugenzi Mtendaji wa TPSF, Godfrey Simbeye, alisema TPSF kama msimamizi na mratibu mkuu wa mabaraza hayo watahakikisha malengo ya kuanzishwa kwa mabaraza hayo yanatekelezwa kama ilivyokusudiwa.

“Mabaraza haya ndiyo daraja la kuwavusha vijana kuelekea katika fursa mbalimbali hivyo kuwa na mchango mkubwa katika kufikia azma ya serikali ya kujenga uchumi wa kati na viwanda ifikapo mwaka 2025,” alisema.

Simbeye alipongeza ushirikiano uliopo kati ya sekta binafsi na serikali katika kutimiza azma ya kuanzishwa kwa mabaraza.

“Niipongeze serikali na TPSF kwa kuafikiana na hatimaye kuanzishwa kwa Mabaraza, ambapo inaonyesha ishara nzuri ya kiushirikiano kati ya serikali na TPSF katika kutatua changamoto mbalimbali ili kuendelea kuwa na mazingira mazuri ya kibiashara, uchumi na uwekezaji,” alisema.

Simbeye alisema elimu zaidi itatolewa nchi nzima kuhusiana na umuhimu wa mabaraza hayo na namna TPSF ilivyojipanga kufanikisha utekelezaji ikiwamo kuwawezesha vijana wanaomaliza vyuo vya kati na vikuu kuingia kwenye ushindani wa soko la ajira ndani na kimataifa.

# Elimu waathirika dawa za kulevya

**Na Dege Masoli,** TANGA

MAMLAKA ya Kudhibiti Dawa za Kulevya imepanga kueneza elimu ya athari ya dawa hizo kupitia klabu zitakazoanzishwa katika shule za msingi na vyuo nchini, ili kuwalinda vijana ambao hawajaanza kuzitumia.

Hayo yalielezwa na Kamishna wa Kinga na Tiba wa Mamlaka ya Kudhibiti Dawa za Kulevya nchini, Dk. Peter Mfisi kwenye mkutano wake na waandishi wa habari jijini hapa alipokuwa akielezea maadhimisho ya Siku ya Dawa za Kulevya yatayofanyika kitaifa jijini hapa Juni 26, mwaka huu.

Dk. Mfisi alieleza kuwa mamlaka hiyo inatambua uwapo wa makundi matatu ya waathirika wa dawa za kulevya, watumiaji ambao hawajaathirika na kundi lile la watu ambao hawajaanza kujiingiza katika matumizi ya dawa za kulevya.

Alisema kutokana na hali hiyo tayari mpango mahususi wa kutoa elimu hiyo katika shule umeshaandaliwa kwa ajili ya kunusuru kundi la tatu ambalo halijaingia kwenye matumizi ya dawa hizo kutambua athari zake.

“Mpango huu tumeanza Mkoa wa Dar es Salaam kwa kufundisha shuleni athari za matumizi ya dawa za kulevya lengo ni kumfanya mtoto atambue tatizo hilo tangu akiwa mdogo na aweze kujihami kwa kutoshawishika kutumia dawa vya kulevya,” alieleza Dk. Mfisi.

Hata hivyo, alieleza kuwa mpango wa kuwapo kwa klabu za vijana zinazopinga matumizi ya dawa za kulevya shuleni ni wa kitaifa na kwamba utakuwa kwa kila shule nchi nzima, lengo ni kuwajenga vijana hao waliyoshuleni na kupata matokeo tarajiwa.

Kuhusu maadhimisho hayo, Dk. Mfisi alisema yatafungwa Juni 26 jijini hapa na Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, na kuwataka wakazi wa Mkoa wa Tanga kushiriki kikamilifu katika shughuli hiyo ili wanufaike na elimu itakayotolewa kuhusiana na janga hilo la taifa.

# Zaidi ya 2,000 wasajili laini za simu

**Na Allan Isack,** ARUSHA

JUMLA ya wananchi 2,073 katika Jiji la Arusha wamesajili laini za simu kwa mfumo wa kielektroniki unaotumia dole gumba, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Utumishi wa Umma.

Akizungumza wakati wa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Utumishi wa Umma mwishoni mwa wiki, Kaimu Meneja wa Mamlaka ya Mawasiliano nchini (TCRA), Mhandisi Imelda Salum, alisema mamlaka hiyo, kwa kushirikiana na kampuni za mawasiliano nchini, Ofisi ya Vitambulisho vya Taifa (Nida) na Ofisi ya Uhamiaji, wamefanikiwa kusajili laini 2,073 hadi kufikia siku ya kilele cha maadhimisho hayo.

Alisema katika maadhimisho hayo, wananchi wapya waliojaza fomu kwa ajili ya kupata vitambulisho vya taifa ni 4,757.

Aidha, alisema wananchi walionunua laini mpya na kuzisajili ni watu 417.

Alisema zoezi hilo lilifanyika kwa mafanikio makubwa kwa wananchi kujitokeza kwa wingi kuchukua namba za vitambulisho, kusajili laini zao pamoja na kuhakiki taarifa za vitambulisho.

Hata hivyo, alisema wakati wa kuhitimisha zoezi hilo wananchi waliendelea kujitokeza kwa wingi hali inayoonyesha bado kuna uhitaji mkubwa wa huduma hiyo kuendelea kutolewa kwa wananchi.

"Mwitikio wa zoezi hili ni kubwa kwani tumefanya kazi kwa mafanikio makubwa na wananchi walijitokeza kwa wingi, pia walituomba tuendelee kutoa huduma hii katika Soko la Kilombero, ili kuwafikia wananchi wengi zaidi ya hawa waliopata huduma," alisema Imelda.

Alisema changamoto kubwa inayowakabili wananchi ni kutokuwa na elimu ya kufahamu utaratibu wa kupata vitambulisho vyao pamoja na namba za vitambulisho kwa ajili ya kukamilisha usajili wa laini.

Awali zoezi hilo lilifanyika kwa muda wa siku mbili kwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Uhasibu Arusha (IAA) na kuhitimishwa kwa siku tatu katika soko la Kilombero.

Ofisa Usajili wa Vitambulisho vya Taifa kutoka Mamlaka ya Nida, Julieth Raymond, alisema kwa wananchi ambao hawakufanikiwa kupata huduma hiyo, wakati zoezi lilipokuwa likiendelea kwenye maeneo hayo, wafikie katika ofisi za Nida kwa ajili ya kupatiwa huduma husika.



Ofisa Madini Mkazi Mkoa wa Kimadini wa Simanjiro, Daud Ntalima (kushoto), akikagua madini ya viwandani katika mgodi wa Mwajanga uliokuwa na mgogoro wa watu watatu na kuutatua. **PICHA: GIFT THADEY**

# DC aonya kinamama kujifungulia nyumbani

**Na Zanura Mollel,** ARUSHA

MKUU wa Wilaya ya Longido mkoani Arusha, Frank Mwaisumbe, amezindua kampeni ya jiongeze tuwavushe salama wilayani hapa na kuwataka wajawazito kuacha tabia ya kujifungulia nyumbani, ili kuepuka madhara wakati wa kujifungua.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Mwaisumbe alisema kampeni hiyo ina dhamira ya kuokoa maisha ya mama na mtoto, kabla na baada ya kujifungua na kuwataka wajawazito kujali afya zao kwa kwenda vituo vya afya.

Mwaisumbe alisema kaulimbiu katika kampeni hiyo ni "Kila mmoja wetu ana wajibu wa kuzuia vifo vitokanavyo na uzazi, na vya watoto wachanga, maneno basi, sasa vitendo".

Alisema ili taifa liweze kufikia malengo yake asilimia 80 ya kupunguza vifo vya mama na mtoto, kuna umuhimu wa kutoa elimu kwa jamii pamoja na kuhakikisha vifaa tiba vinapatikana katika vituo vya afya.

"Tuhakikishe tuna wakunga wa kutosha kwenye vituo, wahudumu wa afya pamoja na madaktari vikiambatana na vitendea kazi," alisema Mwaisumbe.

Alifafanua kuwa serikali imetoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya wilaya na inaelekea kukamilika, hivyo usumbufu wa kusafirisha wajawazito zaidi ya kilomita 80 hadi 100, unaelekea kuisha na kuwataka wakazi wa wilaya hiyo kuvitumia vituo vya afya vilivyopo kwa sasa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Longido, Wakili Juma Mhina (PJ), alisema Wilaya ya Longido ni kubwa yenye kilomita za mraba 7,782 na wakazi 143,613 kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012, lakini Idara ya Afya inajitahidi kuwafikia wakazi hao kwa huduma zaidi licha ya makazi kuwa mbalimbali.

Alisema kumekuwa na changamoto ya kinamama kujifungulia nyumbani, hali ambayo husababisha kukosekana kwa taarifa sahihi ya takwimu za kinamama waliojifungua na hiyo inatokana na mila na tamaduni za baadhi ya makabila nchini.

"Awamu ya tano imetoa fedha zaidi ya Sh. bilioni 2.6 kwa ajili ya kitengo cha afya, vituo vya afya vimejengwa, kupitia kampeni hii ya Jiongeze Tuwavushe Salama ni wakati wa kuhakikisha kinamama wanajifungulia vituo vya afya," alisema Mhina.

Mratibu kitengo cha afya ya uzazi, mama na mtoto wilayani hapa, Joshua Mruve, alisema kiwango cha kinamama kujifungulia katika vituo vya afya, kimeongezeka kutoka asilimia 27 mwaka 2017 hadi asilimia 51.3 mwaka 2019.

"Lakini pia kumekuwa na ongezeka la wanaume kuhudhuria kliniki na wake zao kwa asilimia 59.2 tofauti na miaka ya nyuma hii ni dhahiri wamekuwa na uelewa juu ya afya ya uzazi," alisema.

Hata hivyo, alisema kinamama waliohudhuria kliniki wakiwa na mimba chini ya wiki 12 mwezi Oktoba_ hadi Desemba 2018, ilikuwa asilimia 38, lakini kwa sasa imepanda hadi asilimia 43.6 na hiyo ikiwa ni miongoni mwa viashiria vya ngazi ya kitaifa kuhusu afya ya uzazi.

Kwa upande wa utoaji wa dawa za SP kwa ajili ya tiba kinga ya malaria kwa mjamzito kwa mwezi Januari hadi Machi mwaka 2019, ni asilimia 99.4, huku utoaji wa vyandarua ikiwa ni kwa asilimia 100 kwa wajawazito wote waliohudhuria kliniki.

Aidha, alisema kumekuwa na changomoto ya lishe kwa watoto, huku utapiamlo ukionekana kushika kasi wilayani hapo na kuwataka viongozi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kuhakikisha taswira hiyo, inapotea ili kufikia malengo ya kitaifa.

Mruve alisema wajawazito waliohudhuria kliniki walipimwa maambukizi ya VVU (Ukimwi) kwa asilimia 99.5 na kiwango cha waliobainika kuambukizwa ilikuwa asilimia 0.4 na wote walianzishiwa dawa za kufubaza virusi hivyo.

Sinyati Ngayoni mkazi wa Eworendeke, Kata ya Kimokouwa alisema mila na desturi za jamii ya kifugaji zimekuwa kandamizi kwa wajawazito, wakati mwingine wanakatazwa kula vyakula vyenye ubora kwa makuzi ya mtoto.

"Kuna wengine tunatamani kujifungulia hospitali na hata kuhudhuria kliniki, lakini waume zetu hawana uelewa," aliomba Sinyati.

# NEMC yatoa elimu kwa wafanyabiashara vibebeo

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

BARAZA la Usimamizi na Hifadhi ya Mazingira (NEMC) Kanda ya Kaskazini, limefanya ukaguzi na kuwapa elimu katika masoko ya mkoa huo wajasiriamali wadogo ili waondokane na kugeuza vifungashio vya plastiki kuwa vibebeo vya bidhaa sokoni.

Baraza hilo limefanya ukaguzi katika soko la Kilombero pamoja Mbauda na kuwapa elimu wafanyabiashara wa masoko hayo, pamoja na kupiga marufuku utumiaji wa vifungashio hivyo kama vibebeo.

Meneja wa NEMC Kanda ya Kaskazini, Lewis Mzari, alisema walifanya ukaguzi wakagundua kuwa wafanyabiashara wadogo baada ya kunyimwa kutumia mifuko ya plastiki (malboro), wameamua kutumia vifungashio vya plastiki kubebea vitu.

"Hili halikubaliki kwani nalo ni kwenda kinyume cha sheria, hivyo tumetumia muda mwingi kuwaelimisha wafanyabiashara waache kutumia vifungashio kama vya kubebea bidhaa," alisema.

Naye Mkaguzi wa Mazingira, Novatus Mushi, alisema maeneo mengi waliyopita ya sokoni wamekutana na vituko vya wafanyabiashara hao kugeuza vifungashio kama vibebeo.

"Kweli kunavituko tumepita huku sokoni na kufanya ukaguzi tukakuta wafanyabiashara wamegeuza vifungashio kuwa vibebeo, sasa kitu tulichofanya tumeamua kuwapa elimu na wameelewa na tumetoa onyo kuwa kuanzia kesho tukija tusikute wanaendelea kutumia vifungashio hivyo kama vibebeo na tukikuta mtu anafanya hivyo tutamchukulia hatua kali za kisheria," alisema Mushi.

Alisema kwa kuwa wamegundua tatizo hilo wataendelea kupita katika masoko mengine yote kwa ajili ya kukagua na kutoa elimu kuhusiana na suala hilo.

Mushi alisema wananchi wataelimishwa kuhusu aina za mifuko mbadala yenye ubora unaotakiwa kwa kushirikiana na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) kwa miongozo.

Alifafanua kuwa katika kwenda sambamba na sera ya viwanda wananchi watapata muda wa kufahamu tathmini ya athari kwa mazingira ili kuhakikisha sera ya Tanzania ya viwanda inafanikiwa.

Aidha, wakitoa maoni wafanyabiashara hao, waliomba serikali kuwatafutia vifungashio mbadala vya kuweka vimiminika kama, barafu na nyama ili kupunguza usumbufu wanaoupata.



Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Rombo (DED), Magreth John (watatu kutoka kushoto), akiwa pamoja na watu mbalimbali wenye ulemavu wa viungo baada ya kukabidhiwa baiskeli maalumu za magurudumu matatu (tricycle), zilitolewa na Rotary Club ya Mkuu Rombo. Jumla ya baiskeli 20 zenye thamani ya Sh. milioni 10, zilitolewa na klabu hiyo, kutoka Rotary International. **PICHA: JAMES LANKA**

## Tanroad yashiriki usafi wa mazingira

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WAFANYAKAZI wa Wakala wa Barabara mkoani Kilimanjaro (Tanroad), wameshiriki kufanya usafi wa mazingira katika maeneo mbalimbali yenye vichaka na madimbwi ya maji mjini Moshi yenye mazalia ya mbu, ili kuzuia uwezekano wa kuwapo na mlipuko wa magonjwa ikiwamo kipindupindu, dengue na malaria.

Wakizungumza kando ya ujenzi wa jengo jipya la mama na mtoto katika Hospitali ya Mawenzi ambako pia walifanya usafi, wafanyakazi hao Mhandisi Nicodemus Kalenzo na Kiango-Tupa, walisema, usafi huo umefanyika kuadhimisha Wiki ya Utumishi wa Umma na utakuwa wa kudumu katika maeneo mbalimbali mkoani hapa.

"Katika maadhimisho haya, taasisi yetu pia tumejitokeza kufanya usafi katika maeneo mbalimbali ya mji huu, ili kuonyesha wananchi kuwa jambo hili tunapaswa kufanya wote na si Tanroad pekee," alisema Mhandisi Kalenzo.

Meneja wa Tanroad Mkoa, Mhandisi Nkolenta Ntije, alisema walipokea maelekezo ya kila taasisi kufanya usafi wiki ya utumishi ndani ya taasisi yake na kupeleka taarifa, hivyo yametumia nafasi hiyo kukutana na wadau mbalimbali wakiwamo makandarasi ambao walijadili changamoto ya mashimo katika barabara kuu na namna ya kuzitatua.

"Mbali na mazungumzo na wadau hao pia tumeweza kukutana na watumishi wa hapa kwetu na kuzungumzia changamoto wanazokabiliana nazo na zile zinazohusu uongozi tumezichukua na tunazifanyia kazi, ili kuhakikisha zinaisha na tunaendelea kutoa huduma iliyo bora kwa wanaotutegemea," alisema.

Aidha, Katibu wa hospitali hiyo, Rehema Nyongele, alikiri wafanya kazi hao kufanya usafi katika maeneo ya hospitali hiyo na kuiomba jamii kuwa na moyo wa kujitokeza mara kwa mara kufanya usafi kwa kushirikiana na watendaji wa hospitali hiyo.

"Sisi kama hospitali pamoja na usafi wa mazingira ndani na nje, lakini pia huwa wanapulizia dawa za kuua wadudu wa aina mbalimbali ili wasilete madhara kwa wagonjwa," alisema.

Rachael Josefu ni mfanyabiashara katika jengo kuu la maegesho ya magari ya mjini Moshi, aliipongeza serikali kwa utaratibu mpya wa kusherehekea Wiki ya Utumishi wa Umma, huku akisema itawasaidia kupokea kero za watumishi na kufanyiwa kazi kwa wakati.

"Utaratibu uliofanyika mwaka huu, umeleta tija kwa taasisi zenyewe na wadau wanaohudumiwa na taasisi hizo...lakini tunaiomba serikali kuhakikisha inapokea kero hizo na kuzifanyia kazi kwa wakati ili tuweze kusonga mbele kwa maendeleo," alisema Musa Swalehe, mkazi wa Moshi.

# GGM yakusanya bil. 2/- kupambana VVU

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MGODI wa dhahabu wa Geita (GGM) kwa kushirikiana na wafadhili mbalimbali umekusanya zaidi ya Sh. bilioni mbili katika kampeni ya mapambano dhidi ya virusi vya Ukimwi.

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira, aliyasema mwishoni mwa wiki wakati akiwapokea wapandaji wa Mlima Kilimanjaro 32 na waendeshaji wa baiskeli 32 ambao walizunguka mlima huo kwa lengo la kuhamasisha uchangishaji wa fedha hizo.

Alisema kupitia mfuko maalumu wa kusaidia kampeni ya mapambano dhidi ya virusi vya Ukimwi kwa mwaka huu 2019 wamefanikiwa kukusanya zaidi ya Sh. bilioni mbili fedha ambazo zinatokana na wafadhili pamoja na wadau wengine wanaopambana na Ukimwi.

"Katika kipindi cha miaka 17 tangu GGM wameanzisha kampeni hii, wamefanikiwa kukusanya zaidi ya Sh. bilioni 13, mbali na fedha hizo kwa mwaka huu kupitia kampeni hii wamechangisha zaidi ya Sh. bilioni mbili ambazo zinatokana na wafadhili na wadau wengine," alisema.

Aidha, alisema lengo la serikali ni kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka 2030 inafikia lengo la sifuri tatu na kwamba kwa kupitia kampeni hiyo ya GGM imekuwa na manufaa makubwa kwa mkoa huo kutokana na hali ya maambukizi ya virusi vya Ukimwi kupungua kwa asilimia tano hadi kufikia asilimia 2.6.

Naye Makamu wa Rais wa GGM, Simon Shao, alisema kupitia kampeni hiyo zaidi ya taasisi 50 zinazojihusisha na masuala ya Ukimwi zimenufaika kupitia fedha hizo ikiwamo kituo cha kulelea watoto yatima cha Mtoto wa Huruma.

"Tumekuwa tukichangisha fedha hizi za mapambano dhidi ya virusi vya Ukimwi kwa miaka 17, fedha zinazopatika tunazitumia kusaidia mapambano haya.. toka tumeanza zaidi ya watu 800 wamepanda Mlima Kilimanjaro na leo zaidi ya asilimia 99 wamefika kileleni," alisema.

Alisema GGM itaendelea kushirikiana na serikali katika masuala mbalimbali ya maendeleo ikiwamo mapambano dhidi ya Ukimwi na kwamba ni vema taasisi nyingine zikashiriki katika kampeni hiyo na kuacha kuitegemea serikali pekee.

Kwa upande wake, Kaimu Mkurugenzi wa Tume ya Kudhibiti Ukimwi (Tacaids), Jumanne Issango, alisema tume hiyo itahakikisha fedha zote zinazochangishwa zinatumika kwa uwazi kwa lengo lililokusudiwa.

## Wahudumu afya watakiwa kuacha ubaguzi

**Na Mary Mosha,** HAI

KIONGOZI wa Mbio za Mwenge wa Uhuru 2019, Mzee Mkongea Ali, amewataka wahudumu wa afya katika Hospitali ya Wilaya ya Hai, kuendelea kuwajibika katika huduma ya afya bila ubaguzi na chuki kwa wagonjwa. Aliyasema hayojana wakati alipotembelea duka la dawa hospitalini hapo, ili kujionea utoaji wa huduma zinazoendelea na kuwataka wananchi kutumia vyandarua kwa njia sahihi, wajawazito kuhudhuria kliniki na kuwataka watoaji wa huduma za afya kuzingatia weledi wa kazi zao.

"Watoa huduma endeleeni kutoa huduma kwa kuzingatia sheria taratibu na kanuni za misingi ya umma...serikali ya awamu ya tano haitamvumilia mtu yeyote atakayekaidi kwa makusudi au kuzembea kumnyima mwananchi huduma," alisema.

Awali akitoa ujumbe wa Mwenge kitaifa, alisema serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itahakikisha ifikapo mwaka 2020 wananchi wanaoishi vijijini wanapata huduma ya majisafi na salama kwa asilimia 85 na mjini asilimia 95.

"Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, itaendelea kupambana na wabadhirifu wa mali za umma pamoja na vitendo vya biashara na matumizi ya dawa za kulevya ili kunusuru vijana wanaotegemewa na taifa," alisema.

Mwenge wa Uhuru umezindua na kutembelea miradi mitano yenye thamani ya Sh. 11,240,840,094 na ujumbe wa Mwenge kwa mwaka huu ni "Maji ni haki ya kila mtu, tutunze vyanzo vyake na tukumbuke kushiriki uchaguzi wa serikali za mitaa".

Nao baadhi ya wananchi wa wilaya hiyo, Anna Moleli, alipongeza zoezi la Mwenge kupitia kila eneo la nchi katika kukagua miradi ya maendeleo kwa kuwa inatoa changamoto kwa watendaji kwa ngazi za wilaya na mkoa.

"Tunaomba serikali watazame zoezi hili kwa upya ... ikiwa wanakagua miradi ya maendeleo, wakague iliyokamilika pamoja na kupanga idadi ya miradi ambayo watakagua kila wilaya, kwa kila mwaka itasukuma juhudi za maendeleo kwa kila mwaka," alisema Samwel Moleli.

Nipashe

# Spotika



USAJILI WA NDANI LIGI KUU BARA 2019/20 UK.18



# PATASHIKA...

Mshambuliaji wa Brazil, Gabriel Jesus (kushoto), akipata upinzani mkali kutoka kwa mabeki wa Peru wakati akitaka kuwatoka kwenye mechi ya Copa America iliyopigwa juzi na wenyeji hao kushinda 5-0, hivyo kufuzu hatua ya robo fainali. **HABARI UK. 28**

## ISIKUPITE

MWANADADA Marta ameweka rekodi ya kuwa mchezaji wa kwanza kufunga mabao 17 kwenye Kombe la Dunia kwa upande wa wanawake na wanaume, kufuatia bao lake aliloifungia Brazil dhidi ya Italia Jumanne kwenye fainali za Kombe la Dunia kwa Wanawake. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, sasa ameipiku rekodi iliyokuwa ikishikiliwa na Mjerumani Miroslav Klose ya mabao 16 kwenye michuano hiyo.



SOKA

# NYOTA WANAOSUBIRIWA KUTUA ARSENAL 2019/20



Praet

**LONDON, England**

DIRISHA la usajili si kitu ambacho mashabiki wa Arsenal wanakifurahia, hasa ukizingatia kiwango chao kibovu katika misimu ya hivi karibuni. Utawala mbovu limekuwa jambo la kawaida pale, hasa linapokuja suala la kusimamia mikataba ya wachezaji.

'Washika bunduki' hao walitarajiwa kumaliza kwenye nne bora ya Ligi Kuu England, na walishindwa kutwaa taji la Ligi ya Europa kwa kufungwa kwenye fainali. Kwa bahati mbaya majeruhi na kutokuwa na kiwango kilichoimarika na maamuzi ya uchaguzi wa wachezaji kutoka kwa kocha, Unai Emery yote hayo yamekuwa mambo ambayo yamechangia timu hiyo kufungwa kwenye fainali ya Ligi ya Europa mabao 4-1 na wapinzani wao wa jiji moja la London, Chelsea kule Baku na pia wakishindwa kumaliza kwenye nne bora.

Kushindwa kwao kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao, ndiko kumesababisha Arsenal kushindwa kuwapata wachezaji waliokuwa wanawawania kama vile Samuel Umtiti (Barcelona) na Nicolas Pepe (Lille), ambao wameona ni afadhali wakacheze sehemu nyingine ambako watakuwa na nafasi ya kucheza kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. Ukiangalia bajeti yao ya usajili ya kupenda kununua wachezaji kwa bei rahisi, hilo nalo ni tatizo jingine.

Huku msimu wa 2019/20 ukiwa umebakiza mwezi mmoja kuanza, Washika Bunduki hao wapo kwenye harakati za kuimarisha kikosi chao kwa kujaribu kutafuta wachezaji wa maana ili kuwasainisha. Hapa tunawaangalia wachezaji wanne ambao Arsenal inatakiwa kuwania saini zao kipindi hiki cha majira ya joto, teremka nayo...

**4, 3. JOACHIM ANDERSON NA DENNIS PRAET (SAMPDORIA)**

Kipaumbele cha usajili wa Arsenal msimu huu cha kutafuta mabeki wa kati wenye uwezo wa kumiliki mpira na pia kumtafuta kiungo ambaye ataweza kuvaa vizuri viatu vya Aaron Ramsey. Wachezaji hawa wa Sampdoria, Joachim Anderson na Dennis Praet wanaonekana kufiti nafasi hiyo na wameonyesha nia kubwa ya kutaka kuwasainisha mikataba.

Emery anatazamiwa kukijenga kikosi chake kwa kusaini wachezaji wenye uwezo mkubwa wa kiungo kwa ajili ya kutengeneza mashambulizi, hawa wawili wanaonekana kuwa kwenye rada zao.

Anderson mwenye umri wa miaka 23, raia wa Denmark, anacheza nafasi ya beki wa kati. Staili yake ya uchezaji ndiyo iliyomvutia Emery na benchi la ufundi limekuwa na uhakika mkubwa wa kuweza kumpata. Akiwa na uwiano wa asilimia 88.1% wa kupiga pasi kwa usahihi, ndiye mtu sahihi ambaye anaweza kufiti kwenye staili ya kocha Emery.

Wakati huo huo, mchezaji mwenzake, Praet ni kiungo mbunifu ambaye anapenda zaidi kucheza namba nane na hivyo ana uwezo mkubwa wa kumrithi Ramsey aliyetimkia Juventus. Kwa ada inayotajwa kuwa ni pauni milioni 15, anaweza kuwa muhimu zaidi kwao.

Kwa mujibu wa Gazeti la Gazzetta dello Sport, Sampdoria imepanga kiasi cha pauni milioni 49 kwa wachezaji wote wawili baada ya kukataa ofa ya awali ya pauni milioni 43 iliyotolewa wiki iliyopita. Kama wataweza kukamilisha mpango huo ni suala la muda.

**2. ALEXIS CLAUDE-MAURICE (LORIENT FC)**

Alexis Claude-Maurice anaweza kufuata nyayo za Matteo Guendouzi na kuwa na mafanikio pale kwenye dimba la Emirates.

Huku Danny Welbeck akiwa anaondoka hapo, Arsenal wanahitaji kupata mchezaji bora wa kuimarisha kikosi hicho na kuwa cha ushindani hasa kwenye safu ya ushambuliaji. Pierre-Emerick Aubameyang na Alexandre Lacazette kwa namna yoyote hawawezi kutumika kwa mzunguko, hasa ikizingatiwa kwamba upatina wao umekuwa na matokeo mazuri zaidi. Hivyo kwa kuzingatia hilo, Alexis Claude-Maurice anaonekana atafaa kuwa mshambuliaji nyuma yao.

Gazeti la Ufaransa la Soccerlink, limeripoti kwamba ofa zimezidi kumiminika kwa nyota huyo wa Ligue 2. Arsenal wenyewe wameripotiwa kwamba wameshatoa ofa ya pauni milioni nane kwa ajili ya mchezaji huyo, ingawa pia West Ham, Lyon, AS Monaco, Lille na Borussia Moncheng-ladbach pia zimekuwa zikimwania mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21.

Msimu uliopita alifunga mabao 14 na kutoa pasi za mwisho nne. Hivyo kama Arsenal wataweza kuipata saini yake atakuwa na faida kubwa zaidi kwa upande wao.

**1. YANNICK CARRASCO (DALIAN YIFANG)**

Kwa mujibu wa taarifa mbalimbali, Arsenal wanaongoza kwenye mbio za kuipata huduma ya winga Yannick Carrasco wakati mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji akiwa anapanga kurudi kucheza barani Ulaya. Ukizingatia kwamba, hawana winga wa kutosha, mashabiki wengi wamekuwa wakimtaka Carrasco kutua kwenye dimba hilo la Emirates.

Huku jezi za klabu hiyo za Adidas zikitarajiwa kutambulishwa Julai Mosi, ni wazi kwamba kuna uwezekano mkubwa mmoja wa wachezaji wake watakuwapo kwenye jezi hizo. Carrasco anaonekana kwamba yupo kwenye nafasi nzuri zaidi ya kujiunga na kikosi hicho, huku ada yake ikitajwa kuwa kati ya pauni milioni 25 hadi 30.

Hata hivyo, kwa mujibu wa Gazeti la Ujerumani la Bild, miamba wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, Bayern Munich watarudi kwenye mpango wa kuanza mazungumzo ya kumsainisha mkataba mchezaji huyo wa Ubelgiji baada ya kumkosa winga wa Manchester City, Leroy Sane. Hivyo Washika Bunduki hao kwa sasa wapo kwenye mazungumzo na klabu yake ya China ya Dalian Yifang kwa ajili ya kuipata saini ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25.

**JE, WAJUA?**



HII ni mara ya 15 kwa Senegal kushiriki michuano ya Mataifa ya Afrika (Afcon), rekodi yao ya kufanya vizuri ni mwaka 2002, ilipotinga fainali na kupoteza kwa penalti dhidi ya Cameroon wakati huo kocha wa kikosi hicho kwa sasa, Aliou Cisse akiwa nahodha.

## MICHEZO



# KIKOSI BORA CHA MAPRO LIGI KUU BARA 2018/19

Clatous Chama wa Simba, mmoja wa mapro waliotisha Ligi Kuu msimu uliomalizika.

**Na Mwandishi Wetu**

UKWELI lazima usemwe kuwa mashabiki wa soka nchini walikuwa wakimiminika katika viwanja mbalimbali nchini na hata kwenye vibandaumiza kuangalia wachezaji kadhaa wa kigeni nchini ambao wamefanya kazi kubwa ya kutoa burudani kwao na kuzisaidia klabu zao kufanya vema.

Kwa msimu wa 2018/19, kumekuwa na wachezaji wa kigeni wengine wakicheza ligi kwa mara ya kwanza na wengine wakiwa wazoefu wa ligi ya Tanzania, waliokuwa wakiwapagawisha mashabiki wa soka kutokana na uwezo wao mkubwa wa kusakata kabumbu, vipaji, lakini uwezo wa kufunga mabao pia.

Tayari Ligi Kuu imemalizika, na katika mfululizo wa makala haya, tuliwaletea wachezaji bora wa jumla ambao ni mchanganyiko wa kigeni na wazawa, pia tuliwaletea wachezaji bora wa Kitanzania wa msimu, leo tunamalizia mfululizo wa makala haya kwa kuwaangazia wachezaji bora wa kigeni kutoka nchi mbalimbali, waliofanya vema kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliomalizika, twende pamoja...

**1. JONATHAN NAHIMANA- KMC**

Mafanikio na KMC kukamata nafasi ya nne na kupata tiketi ya kucheza Kombe la Shirikisho hayawezi kuzungumziwa, bila kumwelezea kipa namba moja kwa sasa wa timu hiyo, Jonathan Nahimana. Huyu amewaweka benchi makipa wote wa klabu hiyo, akiwamo kipa maarufu nchini Juma Kaseja.

Ni kipa wa timu ya Taifa ya Burundi na sasa yupo Afcon akiiwakilisha nchi yake kwenye michuano hiyo na shughuli yake ilionekana dhidi ya Nigeria wakati wakipoteza kwa bao 1-0. Amefanya kazi kubwa sana hadi KMC kuwa hapo ilipo.

**2. NICOLAUS WADADA- AZAM FC**

Ni beki wa pembeni wa Azam FC na timu ya Taifa ya Uganda. Huyu pia kwa sasa yupo nchini Misri kwenye michuano ya Afcon, akiiwakilisha nchi yake kwenye michuano hiyo.

Pamoja na kuifikisha timu yake ya Azam FC, nafasi ya tatu kwenye ligi, lakini pia amewezesha timu hiyo kupata tiketi ya kucheza Kombe la Shirikisho msimu ujao. Ni mmoja wa wachezaji waliofanya vizuri sana msimu huu kutokana na kasi yake, kuzuia na krosi za hatari.

**3. BRUCE KANGWA- AZAM FC**

Huyu pia alikuwamo katika kikosi cha wachezaji bora wa jumla ya msimu uliomalizika kwenye Ligi Kuu. Anastahili kuendelea kuwamo pia kwenye kikosi cha ma-pro wenzake kutokana na sababu au sifa tulizozieleza. Ni raia wa Zimbabwe mwenye uwezo mkubwa wa kukaba na kupeleka mashambulizi mbele. Kikubwa ni wepesi wake na kasi kubwa, ikiwamo uwezo wa kutoa pasi za mabao.

**4. PASCHAL WAWA- SIMBA**

Ni mmoja wa wachezaji wa kigeni waliowezesha Simba kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, lakini pia kuiwezesha kutinga hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Wawa, raia wa Ivory Coast, amekuwa mhimili mkubwa kwenye ngome ya timu hiyo na hata asipokuwapo, safu ya beki wa kati huteteреka.

**5. YAKUBU MOHAMED- AZAM FC**

Beki huyu wa kati kutoka Ghana ni mmoja kati ya wachezaji mahiri na muhimu kwenye kikosi cha Azam FC. Anapokuwa uwanjani akicheza sambamba na Mbongo Aggrey Moris, ngome ya timu hiyo huwa haitikisiki. Ni beki mwenye kutumia nguvu inapobidi, lakini kwa asilimia kubwa hutumia akili. Naweza nikampa unahodha wa kikosi hiki.

**6. PAPY TSHISHIMBI- YANGA**

Ni Mkongomani alifika nchini na kujiunga na Yanga misimu miwili iliyopita. Alifanya makubwa, lakini mwanzoni mwa msimu huu hakuwa kwenye kiwango chake cha kawaida. Hata hivyo, kuelekea kumalizika msimu, alirejea kwenye kiwango chake na kuifungia timu yake mabao muhimu, hivyo anastahili kuwamo kwenye kikosi cha wageni.

**7. HARUNA NIYONZIMA- SIMBA**

Mnyarwanda Haruna Niyonzima alianza vibaya, lakini amemaliza vizuri. Hakuwa na msimu mzuri tangu alipojiunga na Simba akitokea Yanga. Lakini kuelekea kumaliza mkataba wake wa miaka miwili, ameibuka na kuwa muhimu kwenye kikosi cha timu hiyo.

Mechi dhidi ya SC Vita ya DRC, ndiyo iliyomwondoa kuwa mchezaji wa akiba hadi wa kutegemewa. Na baada ya kuisaidia Simba kushinda mabao 2-1, akaanza kuwa tegemeo hadi kwenye Ligi Kuu.

**8. CLEOTUS CHAMA- SIMBA**

Wenyewe wanamwita 'Mwamba wa Lusaka.' Ni mmoja wa kiungo ambaye ni kivutio kikubwa akiwa uwanjani, si tu kwa wanachama na mashabiki wa Simba, bali hata kwa wapinzani wanavutiwa na kabumbu lake. Ni mmoja wa wachezaji wachache wa kigeni kwenye Ligi Kuu ya Tanzania mwenye uwezo wa kuuchezea mpira anavyotaka, chenga za maudhi, pamoja na uwezo wa kufunga mabao.

Ameipa Simba ubingwa, lakini pia kuifikisha kwenye hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

**9. MEDDIE KAGERE- SIMBA**

Raia huyu wa Rwanda, ndiye mfungaji bora wa Ligi Kuu ya Tanzania Bara akiwa na mabao 23.

Kwa msimu mmoja tu aliocheza Ligi Kuu ya Tanzania, ametokea kuwa maarufu si kwa mashabiki wa soka pekee, hata kwa watoto wadogo kutokana na uwezo wake mkubwa wa kupachika mabao.

Kikubwa kinachompa uwezo Kagere ni nguvu, akifanana na aina ya mastraika asilia wa kizamani waliokuwapo Bongo, lakini kwa sasa ni nadra kuwapata.

**10. HERITIER MAKAMBO- YANGA**

Kwa bahati mbaya msimu ujao hatutokuwa naye straika huyu kutoka DRC kwani ameshasajiliwa na klabu ya Horoya ya Guinea, lakini kwa msimu mmoja tu aliocheza Tanzania ameotokea kuwa kipenzi cha wanachama na mashabiki wa Yanga na wapenda soka kwa ujumla. Alimaliza ligi akiwa na mabao 17.

**11. EMMANUEL OKWI- SIMBA**

Kwa sasa yupo na timu ya Taifa ya Uganda kwenye michuano ya Afcon nchini Misri na ndiye aliyefunga bao moja kati ya mawili wakati wakiichapa DR Congo 2-0 juzi. Okwi ni mchezaji mkongwe zaidi wa kigeni kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, pia hata nchini. Alianza kucheza msimu wa 2009/10. Pamoja kutoka nje ya nchi na kurejea, lakini anabaki na rekodi yake hiyo hadi leo. Bado ana uwezo mkubwa wa kucheza soka kutokana na kuwa na nidhamu, lakini pia amekuwa kama ni nembo na alama ya Klabu ya Simba.

## NJE YA UWANJA

### Wanawake Marekani na rekodi Kombe la Dunia

MAREKANI imeweka rekodi kwenye fainali za Kombe la Dunia kwa upande wa wanawake na wanaume kwa kuweza kufunga mabao 18 katika hatua ya makundi. Mabao hayo iliyapata kwa kuifunga Sweden 2-0, kisha Chile 3-0 kabla ya kuifurumusha Thailand 13-0 kipigo ambacho pia ni rekodi ya ushindi mkubwa kuwahi kupatikana kwenye mechi moja ya michuano hiyo kwa wanawake na hata wanaume. Ni Hungary (mwaka 1954) na Norway (1995) pekee zilizokuwa zikishikilia rekodi ya kuweza kufunga mabao 17 katika hatua ya makundi.



# WANASOKA 10 WANAOINGIZA MKWANJA MREFU DUNIANI



LEO MESSI

**LONDON, England**

TANGU kuanza kwa mchezo wa soka, umepitia mabadiliko mengi. Leo hii klabu zinatumia kitita kikubwa cha fedha kwa ajili ya kutafuta wachezaji bora kutoka kote duniani. Wachezaji hao wanalipwa mamilioni ya fedha kwa wiki ili kuendelea kubaki kwenye klabu zao. Ukiacha hilo, hata nafasi yao nje ya uwanja inawafanya walipwe, hasa kwa kutangaza bidhaa mbalimbali na kujikuta wakiwa kwenye soko kubwa mno.

Orodha hii hapa chini ni kwa mujibu wa jarida la Forbes, ambapo limewataja wanasoka wanaolipwa zaidi duniani kwa sasa. Kiasi hicho kimejumuishwa na zawadi za fedha, mishahara, bonasi pamoja matangazo kwa kipindi cha Juni 2018 na Juni 2019.

Hii ndio orodha kamili ya wanasoka 10 wanaolipwa fedha nyingi zaidi duniani kwa sasa, tiririka nayo sasa...

### 10. ANTOINE GRIEZMANN

Antoine Griezmann kwa muda sasa amekuwa akihusishwa na mpango wa kutua pale Barcelona. Kipindi cha majira ya joto kilichopita, Barcelona ilituma ofa ya maana kwa ajili ya kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28. Hata hivyo, mambo hayakwenda sawa kwa 'La Blaugrana' hao tena wakamkosa dakika za mwisho.

Mchezaji huyu wa kimataifa wa Ufaransa amethibitisha kwamba anaondoka Atletico Madrid kipindi hiki cha majira ya joto na Ofisa Mtendaji wa Atletico, Angel Gil Marin hivi karibuni alibainisha kwamba, Griezmann ataichezea Barcelona msimu ujao.

Mfaransa huyu ni mmoja wa washambuliaji waliokamilika kiufundi, mara nyingi akitumika kucheza namba tisa, na wakati mwingine kama winga wa kulia pale inapohitajika. Uwezo wake huo ndio unamfanya kuwa mchezaji hatari zaidi kwenye lango la adui na ni ngumu kumkabili kirahisi.

Kwa mujibu wa Forbes, anaingiza kiasi cha dola milioni 27.7, huku dola milioni 23.2 zikiwa ni mshahara wake na dola milioni 4.5 ni kutokana na matangazo na bonasi. Anastaili yake ya kushangilia akifunga bao inayoitwa 'Fortnite dance'. Griezmann anadhaminiwa na Kampuni ya vifaa vya michezo ya Puma na Kampuni ya Huawei ya nchini China.

### 9. OSCAR

Kwa wengi, bado inawashangaza mchezaji mwenye kipaji cha ukweli kama Oscar kuamua kuachana na soka la ushindani la barani Ulaya na kuamua kuhamia China tena wakati akiwa kwenye kilele bora kabisa cha uchezaji soka. Hata hivyo, hilo linabaki kuwa ni la kwake binafsi, kama ilivyo kwa mchezaji mwingine yeyote.

Hadi sasa, mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil anaonekana kuwa na furaha zaidi kuendelea kuichezea Klabu ya Shanghai SIPG. Anaendelea kuonyesha kipaji chake nchini China, alisaidia klabu yake kumaliza nafasi ya pili kwenye Ligi Kuu ya Super League katika msimu wake wa kwanza na mwaka jana aliiwezesha kutwaa taji la Ligi Kuu, ikiwa ni mara ya kwanza katika historia ya klabu hiyo.

Hata hivyo, uamuzi wake wa kuhamia China umemfanya kutokuwa na nafasi kwenye kikosi cha timu ya Taifa ya Brazil. Awali akiichezea mara kwa mara Brazil, Oscar hadi sasa ameichezea mechi 47 Brazil na mara ya mwisho ilikuwa Novemba mwaka 2015.

Mchezaji huyo wa zamani wa Chelsea, anaingiza kitita cha dola milioni 29, huku dola milioni 27 ni mshahara na nyingine za matangazo na bonasi ni dola milioni mbili.

### 8. MESUT OZIL

Mesut Ozil, mshindi wa Kombe la Dunia mwaka 2014, anatajwa kama mmoja wa kiungo mbunifu zaidi kwenye soka la kisasa. Mwaka 2010 kwenye Kombe la Dunia nchini Afrika Kusini alitajwa kwenye tuzo ya mpira wa dhahabu pamoja na ofa ya kwenda kucheza Real Madrid.

Mchezaji huyu mwenye umri wa miaka 30, alitangaza kuacha kuichezea timu ya Taifa ya Ujerumani baada ya kuwa na matokeo mabaya kwenye michuano ya Kombe la Dunia mwaka 2018 nchini Urusi, huku akitoa madai ya ubaguzi. Na sasa amekuwa kwenye 'kiti cha moto' chini ya Kocha Unai Emery pale Arsenal kwa kuonekana kutokuwa kwenye kiwango.

Mjerumani huyu mwenye asili ya Uturuki, alikubali kuongeza mkataba wake na 'Washika Bunduki' hao ambao ulimfanya achukue mshahara wa dola milioni 24 kwa mwaka. Ozil pia alikuwa mwanzilishi wa Kampuni ya Michezo ya M10 eSports mwaka 2018.

Yeye ni mmoja wa wachezaji anayelipwa zaidi kwenye Ligi Kuu ya England, kwani Ozil mshahara wake ni dola milioni 30.2 kwa mwaka. Na pia mikataba ya matangazo na Kampuni ya magari ya Mercedes Benz, Kampuni ya vifaa vya michezo, Adidas na pia anatangaza spika za masikioni za Beats za Mwanahipop nguli wa Marekani, Dr. Dre.

### 7. KYLIAN MBAPPE

Ndiye mchezaji mwenye umri mdogo zaidi katika orodha hii, Kylian Mbappe amekuwa akichomoza kwa kasi kubwa na anatabiriwa mengi katika soka kwa siku za usoni. Msimu wa 2016/17, akiwa pale AS Monaco ndiko dunia ikamtambua na klabu kadhaa Ulaya zikaanza mbio za kuwania saini yake na mwisho wa siku Paris Saint-Germain wakashinda kwenye mbio hizo.

Hata hivyo, ilikuwa ni michuano ya Kombe la Dunia mwaka 2018 nchini Urusi ndio iliyomtambulisha rasmi Mbappe kama mmoja wa wachezaji bora kabisa. Mfaransa huyo alishinda tuzo ya mchezaji bora kijana wa michuano hiyo na pia ameshinda tuzo ya mchezaji bora wa mwaka wa Ufaransa kutokana na kiwango chake dimbani. Uwezo wake umemfanya kuwa na soko kubwa zaidi duniani kwa sasa.

Kabla ya michuano ya Kombe la Dunia mwaka jana, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20, alikuwa na mdhamini mmoja tu, Nike. Oktoba mwaka jana akaingia mkataba na Kampuni ya Hublot, akichukua nafasi ya mwanariadha Usain Bolt ambaye alikuwa balozi wa bidhaa za Hublot. Akiwa anaingiza kiasi cha dola milioni 26.6 kutoka kwenye mshahara wake, lakini pia anaingiza kiasi cha dola milioni nne kutoka kwenye matangazo na udhamini na hivyo kumfanya aingize mfukoni dola milioni 30.6 kwa mwaka.

### 6. ALEXIS SANCHEZ

Baada ya kujiunga na Arsenal akitokea Barcelona mwaka 2014, Alexis Sanchez haraka aliweza kuzoea mazingira ya Ligi Kuu ya England na kuwa mkali dimba. Wakati wake akicheza pale Arsenal, mchezaji huyu wa kimataifa wa Chile alikuwa akitajwa kama mshambuliaji hatari zaidi. Pamoja na mchango wake wa kufunga mabao kwa Washika Bundi hao, lakini Sanchez hakuweza kuisaidia Arsenal kutwaa taji la Ligi Kuu.

Kutokana na njaa ya kutaka kutwaa mataji, Sanchez akalazimisha uhamisho wa kuondoka Arsenal mwaka jana na akajiunga na Manchester United katika uhamisho ambao pia ulimhusisha Henrikh Mkhitaryan kuondoka pale Old Trafford kwenda Arsenal. Lakini kwa mshangao wa wengi, raia huyu wa Chile alishindwa kabisa kuonyesha uwezo wake kwenye dimba la Old Trafford. Amekuwa na kiwago kibovu zaidi katika historia yake ya uchezaji soka, licha ya kuchukua mshahara mkubwa klabuni hapo.

Mshahara wake kwa mwaka ni dola milioni 28.3 na dola milioni 2.5 zinatokana na matangazo na hivyo kumfanya kuingiza kiasi cha dola milioni 30.8 kwa mwaka. Ana kampuni kadhaa zinazomdhamini kama vile, Pepsi na alitajwa kuwa balozi wa Huawei mwaka 2015. Pia ana mkataba na kampuni ya vifaa vya michezo ya Nike ambayo anavaa viatu vyake.

### 5. ANDRES INIESTA

Andres Iniesta ndiye mchezaji mwenye umri mkubwa zaidi katika orodha hii. Mhispania huyu anabaki kuwa mmoja wa viungo bora zaidi dunia kuwahi kuwashuhudia. Ni kiungo mbunifu mwenye uwezo wa kuichezesha timu, uwezo wa kumiliki mpira na kutengeneza pasi zenye 'macho'. Ilijulikane kwamba wakicheza kwa pamoja, Iniesta, Xavi na Lionel Messi hakuna beki iliyokuwa na uwezo wa kuwazuia duniani.

Akiwa amekulia katika kituo cha kulelea vipaji vya soka pale 'La Masia' katika Klabu ya Barcelona, aliamua kumaliza kipindi chake cha miaka 22 aliyokaa na miamba hiyo ya Catalunya na kujiunga na klabu ya nchini Japan ya Vissel Kobe mwaka jana. Pia amekuwa akidhaminiwa na kampuni ya vifaa vya michezo ya Nike kwa zaidi ya muongo mmoja. Mhispania huyu kwa sasa ameingia mkataba na kampuni ya vifaa vya michezo ya Asics ya nchini Japan.

Pamoja na mshahara na mapato mengine, Iniesta anapata kiasi cha dola milioni 32.5 kwa mwaka. Dola milioni 30 ikiwa ni mshahara na mapato mengine ni dola milioni 2.5.

### 4. PAUL POGBA

Baada ya kuondoka Manchester United, Paul Pogba alifurahia kipindi chake cha uchezaji pale Juventus. Uwezo wake aliounyesha pale kwa 'Kibibi Kizee' cha Turin ukawafanya 'Mashetani Wekundu' kumchukua tena baada ya miaka minne kwa ada iliyoweka rekodi kipindi hicho.

Mfaransa huyo amekuwa wa kubadilika badilika hapo Old Trafford, ilikuwa habari mbaya kwamba Pogba hazikuiva na kocha, Jose Mourinho na mahusiano yao mabaya yakaifanya Man United kutokuwa kwenye kiwango bora. Na msuguano wao wa chinichini ukasababisha Mourinho kufukuzwa pale Manchester United Desemba mwaka jana.

Ukizungumzia kuhusu uhamisho wa Pogba, klabu kadhaa zimekuwa zikimwania ikiwamo timu yake ya zamani ya Juventus na Real Madrid. Kama mpango wake utafanikiwa, basi atabakia kuwa mmoja wa wachezaji ghali zaidi wa wakati wote.

Kwa mwaka Mfaransa huyu anaingiza dola milioni nne kutoka kwenye matangazo na bonasi, huku kwenye mshahara akiingiza dola milioni 29 na hivyo kumfanya aingize kitita cha dola milioni 33 kwa mwaka. Pogba ana mkataba wa miaka 10 na Kampuni ya Adidas. Kampuni hiyo ya vifaa vya michezo ya Ujerumani imekuwa ikimvalisha nyota huyo.

### 3. NEYMAR

Miaka michache nyuma, Neymar alikuwa mchezaji kijana aliyekuwa akitabiriwa kwa mambo mengi zaidi, ambapo alitajwa ndiye atakayekuja kumaliza zama za Lionel Messi na Cristiano Ronaldo. Bahati mbaya mambo yamekwenda tofauti kabisa na dunia ya soka ilivyomtarajia nyota huyo wa kimataifa wa Brazil.

Kwa sasa ndiye mchezaji ghali zaidi wa wakati wote, nyota huyo wa zamani wa Santos aliondoka Barcelona kipindi cha majira ya joto cha mwaka 2017 kwenda kujiunga na PSG kwa ada ya euro milioni 222. Tangu hapo amekuwa akisumbuliwa na majeraha ya mara kwa mara.

Neymar pia hayupo kwenye michuano ya mataifa ya Amerika Kusini, Copa America, kwa sababu ameumia kifundo cha mguu wakati wa mchezo wa kirafiki kati ya Brazil na Qatar. Madai ya kumbaka mrembo, Najila Trindade yameibuliwa hivi karibuni na kumweka kwenye wakati mgumu Neymar.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, nje ya dimba anadhaminiwa na Nike, Red Bull, Gillette, McDonalds na Beats by Dre. Anaingiza kiasi cha dola milioni 105 kwa mwaka.

### 2. CRISTIANO RONALDO

Cristiano Ronaldo kwa mara nyingine tena ameshindwa kuongoza kwenye orodha hii, akitoka kuikosa pia mwaka jana. Raia huyu wa Ureno alijiunga na Juventus baada ya kukaa kwa miaka tisa pale Real Madrid.

Mwanzo wake pale kwenye dimba la Allianz Ronaldo ameisaidia Juventus kutwaa taji la Ligi Kuu ya Italia, Serie A, akifunga mabao 21 na kutoa pasi za mwisho 11 katika mashindano yote. Hivi karibuni alikuwa kwenye kikosi cha timu ya Taifa ya Ureno kilichotwaa Kombe la Ligi ya Mataifa ya UEFA.

Ronaldo alikumbwa na kesi ya kukwepa kodi na hivyo akakubali kulipa kiasi cha dola milioni 21 katika mahakama ya mjini Madrid nchini Hispania. Kwa sasa ana umri wa miaka 34, akiwa ndiye mmoja wa wanamichezo maarufu zaidi kwenye mitandao ya kijamii akiwa na wafuasi karibia milioni 400.

Matangazo na bonasi zinamwingizia kiasi cha dola milioni 44. Anadhaminiwa na Kampuni kama Tag Heuer, Herbalifena Nike. Ukijumlisha na mashahara, kwa mwaka anaingiza kiasi cha dola milioni 109.

### 1. LIONEL MESSI

Lionel Messi kwa sasa ndiye mwanamichezo anayelipwa fedha nyingi zaidi duniani akimpiku bondia wa Marekani, Floyd Mayweather, ambaye alikuwa akishika nafasi hiyo mwaka jana. Raia huyu wa Ujerumani bila shaka yoyote ni mchezaji wa ajabu zaidi katika soka la kisasa duniani.

Kwa sasa Messi anainyatia tuzo ya Ballon d'Or 2019, kwa pamoja na Cristiano Ronaldo na Virgil van Dijk.

Messi mwenye umri wa miaka 31, mkataba wake wa sasa na Barcelona unamalizika mwaka 2021, akiwa analipwa kiasi cha dola milioni 80 kwa mwaka. Na anaingia kiasi cha dola milioni 35 kutoka na matangazo, akiwa anadhaminiwa na Adidas, Gatorade, Pepsi, Huawei na Ooredoo. Hivyo kwa mwaka anaingia kitita cha dola milioni 127.

## Nukuu

"Watu wanazungumza kuhusu wote, lakini Argentina ya Maradona ilikuwa imara na ilikuwa na ubora kuliko ya Messi. Alikuwa na wachezaji wazuri mbele yake, lakini katika kiungo na nyuma amekosa ulinzi. Hilo ndilo tatizo muhimu, Messi ni wa kipekee, anaishi akiwaza kuhusu kucheza na si kuhusu biashara, kama kwa mfano anavyofanya Neymar," **kocha wa zamani wa AC Milan, Real Madrid na England, Fabio Capello akiichambua Argentina enzi za Maradonna ya Messi kwa sasa.**



"Ni nani ambaye hatataka kufurahia wachezaji kama Ney? Mchezaji wa Barca anapaswa kujiandaa kwa mashindano na klabu kuleta mchezaji mnayeelewana ambaye anaweza kukuiga wakati wowote. Wote tunataka kuisaidia klabu, sitasema yupi wa kumleta ama wa kutomleta hapa," **Luis Suarez akionyesha kumkubali zaidi Neymar kuliko Antoine Griezmann**



"Nina kitu muhimu sana cha kutangaza," aliandika katika akaunti yake ya mtandao wa Twitter. "Baada ya miaka 18, muda umefika wa kupumzika soka. Jumapili ijayo (jana) Juni 23 saa 4:00 asubuhi kwa saa za Japan, nitakuwa na mkutano na waandishi wa habari jijini Tokyo kuelezea kila kitu. Tuonane pale," **mshambuliaji wa zamani wa Atletico Madrid, Liverpool na Chelsea (kwa sasa Sagan Tosu ya Japan), Fernando Torres akitangaza nia yake ya kutundika daluga baada ya kuwa dimbani kwa kipindi cha miaka 18.**



## Michezo

# USAJILI WA NDANI LIGI KUU BARA 2019/20




KAKOLANYA

**Na Adam Fungamwango**

HARAKATI za usajili kwa klabu za Tanzania zimepamba moto kwa sasa, huku kila klabu ikipita huku na huko kuangalia wachezaji ambao wanaweza kuwafaa kwenye klabu zao kwa msimu ujao wa Ligi Kuu 2019/20 na michuano mingine mbalimbali, ikiwamo ya kimataifa.

Kwa timu zinazoshiriki michuano ya kimataifa kama vile Simba, Yanga, Azam na KMC usajili wa kimataifa ulianza Juni Mosi na unatarajiwa kumalizika Juni 30, huku kukiwa na wiki mbili za ziada ambazo zitakuwa na faini, wiki ya kwanza ikiwa na faini yake na ya pili faini yake ikiwa juu zaidi, lakini pia ikiwa ni ya mwisho kabla ya dirisha kufungwa.

Kwa upande wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), dirisha lao la usajili lilinza Juni 15 na linatarajia kumalizika Julai 15.

Tayari sura mpya zimeanza kuonekana, baadhi ya wachezaji wakianza kutambulishwa na klabu mbalimbali za Ligi Kuu, wengine wakiwa ni Watanzania, baadhi kutoka nje ya nchi, huku wengine wakiwa wageni, lakini wakiwa wanacheza Ligi Kuu nchini Tanzania.

Kwenye makala haya, tutaorodhesha wachezaji wa Ligi Kuu ya Tanzania tu haijalishi wa kigeni au Kibongo ambao wametoka klabu moja kwenda nyingine, lakini zikiwa ni za humu humu ndani. Hawa ni wachezaji tu ambao wametangaza na kutambulishwa rasmi na klabu zilizowasainisha. Wachezaji walioongeza mikataba na klabu zao hawahusiki na orodha hii, sasa shuka nayo...

**1. BIRIGIMANA BLAISE- NAMUNGO FC, KUTOKA ALLIANCE FC**

Usajili wa kwanza kabisa wa ndani kutangazwa rasmi ulikuwa ni wa Bigirama Blaise ambaye ni raia wa Burundi. Sraika huyo ambaye alimaliza ligi msimu uliomalizika akiwa na Aliiance FC, amesaini kuichezea Namungo FC ambayo imepanda daraja msimu huu na itaanza kwa mara ya kwanza kucheza Ligi Kuu.

Klabu hiyo imetangaza kumpa mkataba wa mwaka mmoja straika huyo ambaye amemaliza ligi akiwa na mabao tisa. Matano aliyafunga akiwa na Alliance ambayo alijiunga nayo kwenye kipindi cha dirisha dogo, huku manne akiyafunga akiwa Stand United aliyoichezea hadi katikati ya msimu.

**2. IDD SULEIMAN 'NADO'- AZAM FC, KUTOKA MBEYA CITY**

Mchezaji huyo zao la Ndondo Cup misimu miwili iliyopita akiichezea Manzese United, amejiunga na Azam FC akitokea Mbeya City.

Idd Suleiman maarufu kama Nado ana uwezo wa kucheza kama kiungo mchezeshaji, lakini pia kama winga wa kulia na kushoto. Kwenye Ligi Kuu msimu uliomalizika akifanikiwa kutupia jumla ya mabao manane, na hiyo ikawa ni usajili mwingine wa klabu ya ndani kwenda klabu ya ndani nchini.

**3. EMMANUEL MVUYEKURE- AZAM FC, KUTOKA KMC**

Azam iliingia tena kwenye soko la ndani la usajili na kumpata straika mmoja matata Emmanuel Mvuyekure raia wa Burundi. Mchezaji huyo alikuwa akiichezea KMC kwenye ligi iliyomalizika na akafunga mabao saba kwa msimu, amepewa mkataba wa mwaka mmoja kwa matumaini ya kuisaidia timu hiyo kwenye michuano ya kimataifa inayoikabili timu hiyo msimu ujao.

**4. BENNO KAKOLANYA- SIMBA, KUTOKA YANGA**

Kakolanya ni golikipa wa zamani wa timu ya taifa, Taifa Stars ambaye kwa muda mrefu alikuwa na mgogoro na klabu yake kiasi cha kutocheza kwa muda mrefu hali iliyosababisha kushindwa kuitwa Stars. Hatimaye Shirikisho la Soka nchini (TFF) lilimtangaza kuwa yuko huru baada ya Ligi Kuu kumalizika na usajili ulipoanza, Simba ilitoa taarifa ya kumsajili kipa huyo kwa miaka miwili kusaidiana na kina Aishi Manula na Deogratius Munishi 'Dida'.

**5. ABDULAZIZ MAKAME- YANGA, KUTOKA MAFUNZO**

Huyu ni kiungo mkabaji kutoka Mafunzo ya Zanzibar ambaye naye amesainishwa na Yanga kwa ajili kuitumikia klabu hiyo kwa msimu ujao kwenye mechi mbalimbali za Ligi Kuu, Ligi ya Mabingwa na michuano mingine mbalimbali.

Abdulaziz Makame ni mmoja wa viungo waliofanya vizuri kwenye Ligi Kuu ya Zanzibar kwenye ligi iliyomalizika.

**6. KENNEDY JUMA- SIMBA, KUTOKA SINGIDA UNITED**

Msimu uliomalizika alikuwa ndiye nahodha wa Kikosi cha Singida United. Msimu huu amesajiliwa na Klabu ya Simba kwa mkataba wa miaka miwili. Ni beki wa kati akiwa na uwezo wa kucheza namba nne na tano. Tayari ameshaanza kuitumikia timu hiyo kwenye mechi ya kirafiki dhidi ya Gwambina, mechi iliyochezwa Ijumaa iliyopita. Alimaliza ligi akiwa ameifungia Singida United bao moja.

**7. ALLY ALLY- YANGA, KUTOKA KMC**

Klabu ya Yanga imemnasa beki wa kati kutoka KMC ya Kinondoni anaitwa Ally Ally. Ni beki ambaye kabla ya timu hiyo alikuwa akiichezea Stand United. Alizua gumzo kubwa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara iliyomalizika alipojifunga bao katika namna iliyoshangaza wengi, Yanga ikicheza dhidi ya KMC. Beki huyo amesaini mkataba wa miaka miwili.

**8. MAPINDUZI BALAMA- YANGA, KUTOKA ALLIANCE FC**

Ni kiungo maridadi aliyekuwa akiichezea Alliance FC msimu uliomalizika. Alikuwa kwenye msimu mzuri kiasi cha kuwavutia viongozi wa Yanga na kuamua kumpa mkataba wa miaka mitatu kuichezea timu hiyo. Kiungo huyo anamudu kucheza nafasi ya kiungo mshambuliaji, mwenye kasi, chenga na uwezo mkubwa wa kutoa pasi za mwisho.

**9. PAUL NGALEMA- NAMUNGO, KUTOKA LIPULI FC**

Katika kuonyesha kuwa imedhamiria kuonyesha makubwa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao, timu ya Namungo imenasa saini ya beki mzoefu Paul Ngalema. Ngalema msimu huu alichezea timu ya Lipuli, alishawahi kuzichezea Klabu za Ndanda na Simba na zingine kabla ya kujiunga na Lipuli ya Iringa ambayo aliisaidia kufanya vema msimu uliomalizika kwa kushika nafasi ya pili kwenye Kombe la FA, na nafasi ya sita kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

**10. MIRAJI ATHUMANI- SIMBA, KUTOKA LIPULI FC**


Huyu ndiye mchezaji pekee ambaye bado hajatambulishwa na viongozi wa klabu kama wenzake wote, lakini amejitangaza mwenyewe.

Kabla viongozi wa Simba hawajamtambulishwa rasmi, mwenyewe akafunguka na kusema tayari ameshamalizana na klabu hiyo, akitokea Lipuli FC.

"Mpaka nimeamua kusaini Simba, ina maana nimeshamalizana na Lipuli na majina makubwa ya wachezaji wa klabu hiyo hayanitii hofu, nitapambana kwa sababu hakuna ambako hakuna changamoto." Alisema winga huyo ambaye alitokea kwenye kikosi cha pili cha Simba.

Na katika kuthibitisha hilo, Ijumaa iliyopita alicheza mechi yake dhidi ya Gwambina FC tangu ajiunge na Simba.

**NAJUA WAJUA**




Mshambuliaji wa Burundi, Mohamed Amissi, amekuwa mchezaji wa kwanza aliyezaliwa mwaka 2000 kuweza kucheza michuano ya Mataifa ya Afrika (Afcon).

SOKA




# MADRID INAVYOJARIBU KUIRUDISHA GALACTICOS

JOVIC

**MADRID, Hispania**

KATIKA miongo kadhaa iliyopita, miamba wa Ligi Kuu ya Hispania, Real Madrid wamejipatia umaarufu wa matumizi ya hali ya juu kuwanunua wachezaji wenye majina makubwa duniani.

Kutoka Luis Figo na David Beckham hadi Christiano Ronaldo na Gareth Bale, rais wa klabu hiyo, Florentino Perez hajutii matumizi anayofanya ili kuwakusanya wachezaji nyota duniani.

Katika miaka ya hivi karibuni, hata hivyo mtazamo huo umesahaulika.

Mbali na kuwasili kwa Thibaut Courtois kutoka Chelsea msimu uliopia, Real Madrid haijajihusisha na usajili wa mchezaji nyota tangu mwaka 2014 wakati Toni Kross na James Rodriguez waliposajiliwa.

Tangu wakati huo, makocha waliofuata kama vile Carlo Ancelotti, Rafale Benitez, Zinedine Zidane, Julen Lopetegui, Santi Solari na sasa Zinedine Zidane tena- wamekuwa wakiwashirikisha wachezajii wale wale kama vile Keylor Navas, Sergio Ramos, Raphael Varane, Dani Carvajal, Marcelo. Kross, Casemiro, Luka Modric, Isco, Bale, Ronaldo na Karim Benzima wakiwa wakitegemewa zaidi na timu hiyo mwaka baada ya mwaka.

Kwa nini mabadiliko hayo ya sera? Je, wachezaji wapya ni kina nani? Je, kutakuwa na wengine zaidi? Na je, hilo linamaanisha nini kwa nyota waliohudumu kwa kipindi kirefu?

Muda tu baada ya kuishinda Liverpool Mei mwaka jana kuibuka mshindi wa Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa msimu wa tatu mfululizo, Zidane alichukua hatua isiyo ya kawaida, alijiuzulu, akidai kwamba hawezi kupata mafanikio na raslimali alizonazo.

Zidane amekuwa akisema kwamba mafanikio katika ligi ya nyumbani ni uthibitisho mzuri wa uwezo wa timu na alihisi ushindi wa Kombe la Ligi ya Mabingwa 2018 ulikuwa unaashiria kushuka kwa kiwango cha klabu hiyo suala ambalo lilijitokeza wakati ilipomaliza katika nafasi ya tatu msimu huu.

Tayari kulikuwa na ishara mbaya baada ya kuuzwa kwa Ronaldo, na Zidane alikuwa akituma ujumbe kwamba iwapo asingewezeshwa kufanya mabadiliko aliyotaka ilikuwa wakati wa kuondoka. Wiki chache tu baada ya Zidane kujiuzulu, ilionekana wazi kwamba alikuwa sawa.

Baada ya Lopetegui na Solari waliohudumu kwa wiki chache katika klabu hiyo, Perez alirudi kwa Zidane na 'mkia katikati ya miguu yake', akikubali maono yake kwamba kikosi hicho kilihitaji kufanyiwa mabadiliko. Zidane alirudi nyuma na kukubali, lakini kwa masharti.

Kiungo muhimu cha mabadiliko ya Real Madrid, msimu ujao ni usajili wa Eden Hazard. Raia huyo wa Ubelgiji alifuatiliwa kwa kipindi cha mwaka mmoja na Perez na kuvutia mashabiki 50,000 katika Uwanja wa Bernabeu wakati alipotambulishwa.

Huku akiuzwa kwa dau la pauni milioni 150, mchezaji huyo wa zamani wa Chelsea atajiunga na mshambuliaji Benzema.

Lakini Hazard siye mchezaji wa pekee katika safu ya ushambuliaji, huku Real pia ikimsajili nyota mwenye talanta inayozidi kuimarika, Luka Jovic.

Mchezaji huyo wa Serbia mwenye umri wa miaka 21, ameifungia Eintracht Frankfurt mabao 27 msimu uliopita na anatarajiwa kuhusishwa katika kikosi cha kwanza baada ya kununuliwa kwa dau la euro milioni 60.

Mchezaji mwingine aliyesajiliwa ni beki wa kushoto, Ferland Mendy ambaye amejipatia umaarufu mkubwa wakati wa kampeni ya Lyon msimu uliopita na anatarajiwa kushindana na mchezaji wa nyumbani, Sergio Reguilon katika upande wa beki ya kulia ili kumrithi Mercelo.

Huku nahodha Sergio Ramos akiwa na umri wa miaka 33, beki wa kati wa siku za usoni tayari amepatikana kupitia kuwasili kwa Eder Militao kwa dau la euro milioni 50 kutoka Porto, huku mchezaji wa mwisho kusainishwa akiwa winga Rodrygo Goes kutoka klabu ya Santos mwenye umri wa miaka 18 akitajwa kuwa uwekezaji wa siku zijazo.

Na usajili huo sio wa mwisho. Walipokuwa wakisubiri kuwasili kwa Hazard katika uzinduzi wake Alhamisi, mashabiki wa Real walijifurahisha wakisema: "Twamtaka Mbappe" na haijulikani iwapo mchezaji huyo wa Ufaransa ambaye hivi karibuni alikiri kwamba hajui kitakachotokea kuhusu hatima yake, ataondoka PSG katika miezi michache ijayo."

Uvumi unaomhusisha Zidane na nyota mwingine wa Manchester United, Paul Pogba hautaki kuisha, huku kiungo wa kati wa Lyon, Tanguy Ndombele akichukuliwa kama mchezaji atakayenunuliwa iwapo Pogba hatoruhusiwa kujiunga na klabu hiyo.

Usajili wa wachezaji wa hivi karibuni, pamoja na kurudi kwa baadhi ya wachezaji waliotolewa kwa mkopo umeongeza idadi ya wachezaji wa kikosi cha Zidane hadi kufikia 37, na kifedha ni wazi kwamba baadhi yao watalazimika kuuzwa ili kuleta mapato.

Mapato madogo kati ya euro milioni 10 hadi 20 kwa wachezaji kama vile Dani Ceballos, Marcos Llorente, Theo Hernandez na Mariano Diaz yanaweza kulipa fedha alizonunuliwa Hazard mbali na kutoa nafasi katika kikosi hicho. Lakini baadhi ya wachezaji nyota pia watauzwa kuanzia Gareth Bale.

Winga huyo wa Wales hana uhusiano mzuri na Zidane, hivyo basi hatua ya kumtafutia klabu nyingine mchezaji huyo wa zamani wa Tottenham ni mpango uliopo wazi kabisa.

Hata hivyo, uwezo wa kumuondoa mchezaji huyo mwenye majeraha yasiyoisha pamoja na mshahara mkubwa uko juu ni mdogo kwa sasa.

Maamuzi kama hayo pia yanamwandama kiungo wa kati wa Colombia, James Rodrigues ambaye hatakiwi na Zidane na kwamba hakuimarika wakati wa mkopo wake katika klabu ya Bayern Munich ili kuweza kusalia.

Marcelo na Navas pia huenda wakaondoka iwapo ombi zuri litawasilishwa, huku hatima ya Isco ikiwa haijulikani licha ya uhusiano wake wa karibu na Zidane huku mchezaji mwingine mwenye kipaji akiwa mshambuliaji Marco Asensio ambaye hajaimarika zaidi ya ilivyotarajiwa.

**NDANI YA 18**




Uganda imepata ushindi kwa mara ya kwanza kwenye mechi za fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) baada ya miaka 41, ni kufuatia juzi kuichapa DR Congo 2-0 katika mechi yao ya Kundi A nchini Misri, mabao yakifungwa na Patrick Kaddu na Emmanuel Okwi.

# Nipashe Spotika



TANGU kuanza kwa mchezo wa soka, umepitia mabadiliko mengi. Leo hii klabu zinatumia kitita kikubwa cha fedha kwa ajili ya kutafuta wachezaji bora kutoka kote duniani. Wachezaji hao wanalipwa mamilioni ya fedha kwa wiki ili ...

**Uk. 16-17**



# SABABU 3 MAN UNITED KUVURUNDA MSIMU UJAO

**MANCHESTER, England**

MANCHESTER United ilimaliza nafasi ya sita kwenye msimu wa 2018-19 wa Ligi Kuu ya England. Timu haikuwa na kiwango cha kuvutia dimbani na kuwaacha maelfu ya mashabiki wake wakiwa wamevunjika mioyo yao.

Ole Gunnar Solskjaer ana wakati mgumu wa kuijenga klabu hiyo na sasa anaingia katika kipindi cha kuhakikisha timu hiyo inakuwa na maendeleo zaidi, kwa kuchukua hatua kadhaa za kuibadilisha. Idadi ya wachezji muhimu kwenye kikosi hicho bado hawajakubali kuongeza mikataba yao, huku wachache wakiwa kwenye kiwango kibovu. Klabu imekosa nafasi ya kucheza kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na hivyo, usajili wa kipindi hiki cha majira ya joto utakuwa mgumu zaidi kwako.

Matarajio ya klabu hiyo hayaonekani kama yatakuwa mazuri kwa msimu ujao na hivyo hapa makala haya yanakuchambulia sababu tatu kwa nini Manchester United inaweza kuwa tena na msimu wa kukatisha tamaa, twende sasa...

**Uzoefu mdogo wa Solskjaer**

Baada ya kuteuliwa kuwa kocha wa muda Desemba mwaka jana, Ole Gunnar Solskjaer alionyesha ari kubwa kwa Manchester United kuwa kwenye kiwango cha kuvutia kwa miezi miwili. Manchester United ilifurahia kiwango bora kwa kipindi cha miezi hiyo miwili na klabu ilionekana ni wazi kwamba ingemaliza katika nafasi zile nne bora kwenye Ligi Kuu. Hata hivyo, Klabu ikarudi tena kwenye matokeo mabaya kwa kuanza kupoteza mechi kiurahisi tu. Hakuna safu yoyote ya kikosi hicho ilionekana kuwa fiti na kuteuliwa kwa Solskjaer kuwa kocha wa kudumu hakuisaidia klabu hiyo.

Manchester United inahitaji kujengwa upya, lakini kwa kocha kijana ambaye hana uzoefu wa kutosha, kutaifanya klabu hiyo ya Old Trafford kuwa tena na matokeo ya kutoridhisha. Kocha huyo ambaye ameshindwa kumaliza tatizo hilo kwa kipindi kifupi alichokaa hapo, hana uwezo wa kuwa suluhisho la matatizo ya Manchester United kwa wakati huu.

**Kukosekana kiongozi kikosini**

Katika matukio mengi msimu uliopita, timu ilionekana kutoelewana dimbani hasa baada ya kuruhusu bao moja au mawili mwanzoni mwa mchezo. Ukiacha ushindi wa kihistoria walioupata dhidi ya PSG kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, uwezo wa kujiamini wa Manchester United umekuwa mdogo mno msimu uliopita.

Na sababu kubwa ni kukosekana kwa mchezaji kiongozi dimbani ambaye anaweza kuwaongoza na kuwahimiza wachezaji wenzake. Kiukweli, nahodha wa timu katika mechi nyingi, Ashley Young, amekuwa mmoja wa wachezaji walionyesha kiwango kibovu zaidi kwa klabu hiyo msimu uliopita. Paul Pogba na David De Gea wangeweza kumaliza tatizo hilo kwa klabu, lakini wachezaji wote wawili bado hawajakubali kusaini mkataba mpya klabuni hapo.

Ander Herrera ameondoka na kuna wachezaji wachache kikosini hapo wenye uwezo wa kuwa viongozi wa kukabiliana na hali ilivyo hivi sasa. Hata hivyo, klabu inaweza kuwa na matumaini na wachezaji wapya wanaojiunga na kikosi hicho.

**Kutokuwa na staili yao ya kucheza**



Zile siku ambazo kiwango cha uchezaji cha Manchester United kilichowahamasisha mashabiki wao kwa kucheza soka la kuvutia na staili ya kupigana mwanzo mwisho, imeshatoweka. Staili yao kubwa ilikuwa ni kucheza kwa nguvu kwa dakika zote bila kuchoka hadi dakika ya mwisho.

Staili hiyo sasa imehamia kwa wapinzani wao, Liverpool na Manchester City ambao wamekuwa wakikimbizana kwenye Ligi Kuu. Na haikuwa bahati mbaya kwa timu hizi kupishana kwa pointi moja tu katika mbio za ubingwa msimu huu na kuwa timu zenye kiwango cha kuvutia zaidi kwenye Ligi Kuu ya England.

Kikosi cha sasa cha Manchester United kimekuwa hakina uwezo wa kusukuma mashambulizi mara kwa mara kwa timu pinzani, wameshindwa kuwa na kasi ile iliyozoeleka na pia imekuwa haina mabeki wa pembeni wenye uwezo wa kusukumiza mashambulizi mbele. Tofauti na mwanzoni kikosi cha Manchester United kilikuwa na uwezo wa kutengeneza mashambulizi kutoka pande zote, lakini kwa sasa morali ile haipo tena.

Na hii imeathiri utambulisho wa klabu hiyo na sasa wakati huu ikijengwa upya inatakiwa kurudisha utambulisho wake. Lakini kama wataendelea kucheza kama ilivyokuwa kwa msimu uliopita, uwezekano wa kuwa na matokeo mazuri dimbani ni mdogo mno. Hivyo, hii ni moja ya sababu itakayoweza kuifanya Man United kuwa na msimu mwingine usiovutia zaidi kwa mashabiki wake.

**USILOLIJUA**



MARA ya mwisho Argentina kushindwa kusonga mbele kutoka hatua ya makundi kwenye michuano ya Copa America ilikuwa mwaka 1983, wakati timu moja tu kutoka kila kundi ilikuwa ikikata tiketi ya kucheza hatua inayofuata.



## HABARI MBEYA

# RC aiagiza TRA kukutana na wafanyabiashara

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ameiagiza Ofisi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) mkoani humo kwa kushirikiana na Makatibu Tawala wa Wilaya kuiitisha mkutano wa pamoja na wafanyabiashara ili kuzitambua na kuzitatua changamoto zinazowakabili.

Chalamila alitoa agizo hilo juzi katika mkutano uliowahusisha watumishi wa idara mbalimbali ikiwamo ya ardhi, makatibu tawala ndani ya Jiji la Mbeya ili kujadili mpango kazi wa kuinua uchumi wa mkoani humo.

Alisema ili kukuza uchumi wa mkoa, lazima viongozi wakutane na wafanyabiashara kwa lengo la kuzitafutia ufumbuzi changamoto zinazowakabili.

"Mbali na kuhimiza viongozi wa serikali kuitisha mikutano pamoja na wafanyabiashara, lakini viongozi hao wana kazi ya kuhakikisha wanatatua migogoro katika jamii ikiwamo migogoro ya ardhi, uvamizi wa maeneo pamoja na migogoro ya mirathi hali ambayo imekuwa ikisababisha baadhi yao kukosa haki zao za msingi," alisema Chalamila.

Katibu Tawala Mkoa wa Mbeya, Mariamu Mtunguja, alisema, ni vyema watumishi wakaungana pamoja kuzitatua changamoto zinazowakabili ili kusimamia vizuri sheria ya ulipaji kodi.

Naye Kamishna wa Ardhi Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Thadei Kabonge, alisema Idara ya Ardhi ni moja ya sekta ambayo imekuwa ikikabiliwa na malalamiko mengi jambo ambalo limewalazimu kuandaa mkakati madhubuti wa kutatua migogoro hiyo ili kuhakikisha kila mmoja anapata haki yake ya msingi.



Watoto wa Kanisa Katoliki Parokia ya Mtakatifu Joseph mjini Zanzibar, wakiandamana kuadhimisha Sikukuu ya Ekaristi Takatifu jana. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# Uchafuzi wa mazingira wakithiri vyanzo vya maji

**Na Grace Mwakalinga,** CHUNYA

SHIRIKA lisilokuwa la kiserikali linalojihusisha na Uhifadhi wa Mazingira la KAEA lililoko katika Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, limesema wananchi wa wilaya hiyo wanachangia kwa kiasi kikubwa uharibifu wa mazingira hasa kwenye vyanzo vya maji.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika hilo, Lucas Malangalila, wakati wa mafunzo ya utunzaji mazingira yaliyofanyika katika Kata ya Lupatingatinga.

Alisema baadhi ya wananchi wanafanya shughuli za kibinadamu kama vile kilimo, ufyatuaji wa matofali na ukataji miti ovyo kando na vyanzo vya maji, hali inayosababisha maji kukauka au kupungua.

Alitaja miongoni mwa sababu zinazochangia uharibifu wa mazingira hasa kwenye vyanzo vya maji kuwa ni wananchi hususani waishio vijijini kukosa fedha ya kumudu nishati mbadala ya kupikia na kulazimika kutumia kuni au mkaa.

Alisema licha ya sababu hiyo, lakini shirika hilo limekuwa likitoa elimu ya faida za kutunza mazingira vikiwamo na vyanzo vya maji ili kujinusuru na ukame.

"Tunawaelimisha wananchi kuhusu athari za uharibifu wa mazingira na kuacha matumizi mabaya ya rasilimali misitu, ili kuhifadhi vyanzo vya maji na kutoathiri mabadiliko ya tabia nchi, lakini bado baadhi ya wananchi wanaendelea kufanya shughuli zao za kibinadamu," alisema Malangalila.

Hata hivyo, Malangalila alisema wanaendelea kutoa elimu ya masuala ya uhifadhi mazingira hususani kwa wanawake ambao ni wadau muhimu wa maji.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Lupatingatinga, Gasper Msomba, alisema mafunzo hayo yatasaidia jamii kuacha kufanya shughuli za uharibifu wa mazingira ambazo zinachangia mabadiliko ya tabia ya nchi.

Naye Diwani wa Viti Maalum katika kata hiyo, Rehema Mwamakula, alisema ataendelea kuwaelimisha wananchi kupitia mikutano ya hadhara umuhimu wa utunzaji mazingira na kusimamia kikamilifu Sheria za Mazingira.

Aliwaomba wadau yakiwamo mashirika ya kiserikali na yasiyo ya kiserikali na vyombo vya habari kuhakikisha mazingira yanalindwa.

# Vitendo ujangili hifadhi za taifa vyapungua

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

KAMISHNA Mwandamizi wa Hifadhi za Wanyama Tanzania kutoka Shirika la Hifadhi la Taifa (Tanapa), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Dk. Christopher Timbuka, amekiri kuwa vitendo vya ujangili katika maeneo mbalimbali ya hifadhi ikiwamo ya Katavi, Kitulo na Ruaha, vimepungua kutokana na ulinzi unaofanywa na askari wa wanyamapori.

Dk. Timbuka aliyasema hayo jana jijini Mbeya wakati wa ufunguzi wa kikao cha wadau wa Idara ya Ulinzi wa Hifadhi ya Taifa Kitulo, alisema licha ya vitendo vya ujangili wa wanyama kupungua pia ujangili wa mmea aina ya chakanda katika Hifadhi ya Kitulo nao umepungua baada ya kutolewa elimu kwa wananchi wanaozunguka hifadhi hiyo.

Alisisitiza kuwa askari wa wanyamapori wataendelea kuzilinda hifadhi zote nchini kwa lengo la kuongeza watalii na kuliletea taifa manufaa ikiwamo kupata fedha na fursa nyingine.

Akizungumzia uvamizi wa mmea wa chitanda katika Hifadhi ya Kitulo, Kamishna Msaidizi wa Hifadhi hiyo, Theodora Aloyce, alisema walipita katika maeneo yote yanayozunguka hifadhi hiyo kutoa elimu ya umuhimu wa kutunza hifadhi na rasilimali zao na ilisaidia kukomesha tabia hiyo.


"Mmea wa chitanda unatumika kama chakula na gharama yake ni kubwa sana sokoni, lakini pia ni adimu kuupata mmea huo, lakini hifadhi ya Kitulo tumebarikiwa hivyo wananchi huvamia ili kuchimba mmea huo kwa kuwa ni rasilimali adimu, tumepiga marufuku ili tuendelee kuutunza kwenye hifadhi yetu," alisema Theodora.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, aliipongeza Tanapa kwa kuendelea kutunza na kuhifadhi hifadhi mbalimbali nchini na kwamba matokeo yake yameliingizia faida kubwa taifa.

Aliwatahadharisha wanasiasa kuacha tabia ya kuingiza siasa kwenye masuala ya uhifadhi pindi wanapokamatwa wahalifu.

Alifafanua kuwa taarifa zinaonyesha kuwa bado baadhi ya wananchi hukamatwa katika maeneo ya hifadhi za wanyamapori na misitu kwa tuhuma za ujangili na katika kipindi cha mwaka 2016/2017 jumla ya watuhumiwa wa ujangili 141 walikamatwa na mwaka 2017/18 watuhumiwa 78, huku mwaka 2018/19 walikamatwa watuhumiwa 57.

Alisema jumla ya watuhumiwa waliokamatwa ni 276 idadi ambayo ni kubwa na kila mwaka inazidi kupungua.





# Kinamama wakumbuka watoto yatima

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

JUMUIYA ya kinamama wa Madrasat Rahim G ya mkoani hapa, imetoa msaada wa mchele, unga wa ugali, mafuta ya kula, nguo, fedha na madaftari kwa watoto yatima 150 katika eneo la Kizota.

Mbali na msaada huo, wameiomba serikali iwasaidie waweze kupata kituo maalum cha kuwalea yatima hao.

Misaada hiyo waliwakabidhi yatima hao mbele ya Mkurugenzi wa Kituo cha Rahim G, Ustadh Abubakari Ally, walezi na wazazi wa watoto hao pamoja na baadhi ya wakazi wa jijini hapa.

Wakizungumza na waandishi wa habari jana baada ya kugawa vitu hivyo, Kiongozi wa Jumuiya hiyo, Mohbouba Sheikhe, alisema kikundi chao waliamua kujichanga kwa kutafuta fedha, chakula na nguo, ili waweze kuwasaidia yatima hao.

"Kizota kumekuwa na watoto wengi wa mitaani ambao hawana wazazi, tukaona huu ndio wakati wa kuwasaidia, tumechanga fedha, nguo pamoja na chakula ...lengo letu ni tuwasaidie hawa yatima, tunafurahi kwa sababu tumewakabidhi na mnawaona jinsi wanavyofurahi," alisema.

Naye Asha Sheria alisema jumuiya hiyo imeguswa na wingi wa yatima waliopo katika eneo hilo kutokana na wazazi wao kufariki, hivyo wanawaomba Watanzania wengine kuiga mfano wao kwa kuwasaidia.

Mkurugenzi wa kituo hicho, Ustadh Abubakari Ally, aliiomba serikali, taasisi binafsi na za umma kukisaidia kituo hicho kilichopo Kizota, ili kiweze kupata majengo ya kuwalelea kutokana na watoto wa mitaani na yatima kuwa wengi.

"Huu ni msaada wa chakula na baadhi ya vitu, lakini watoto hawa hawaendi shule sababu ni kutokujua umuhimu wa shule, tunaiomba serikali itusaidie tupate majengo ili tuwe tunawakumbusha umuhimu wa shule, kituo chetu hapa hakina majengo ya kuweza kuwaweka," alisema.

Awali akisoma risala, Ramadhan Chivi alisema kwamba kituo hicho kina yatima 34, ambapo wakike ni 19 na wa kiume ni 15, na kwamba kinakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa madarasa mawili kwa ajili ya wanafunzi wa chekechea.

"Kituo chetu kina madarasa sita ofisi 3 kwa ajili ya walimu, tunahitaji madarasa mawili ili wanafunzi waweze kusoma vizuri," alisema.

Akitoa mada iliyowahusu yatima, Ustadh Abdulaziz Issa Dibo alisema kama serikali itawekeza kuwasaidia mayatima katika miaka ya baadaye itapata wataalamu bora katika sekta mbalimbali.

"Tunaiomba serikali iviangalie vituo kama hiki cha Rahim G kwani katika miaka ya baadaye itapata madaktari bora, mahakimu bora ambao hawatajishughulisha na rushwa sababu watakuwa wamepita kwenye sehemu sahihi za malezi," alisema.

# Wafanyabiashara sasa waitwa kuwekeza Dodoma

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAFANYABIASHARA ndani na nje ya nchi wametakiwa kujitokeza kwa wingi kuwekeza katika mkoa wa Dodoma ambao umekuwa na fursa nyingi hivi sasa, baada ya serikali kuhamishia makao yake makuu.

Rai hiyo ilitolea na Mwenyekiti wa Taasisi ya Sekta Binafsi Jiji la Dodoma, Ringo Iringo, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari juu ya maandalizi ya kongamano la fursa litakalofanyika Juni 27 na 28 mwaka huu, jijini hapa. Alisema wafanyabiashra na wawekezaji wote ndani na nje ya nchi wanaalikwa katika kuwekeza katika shughuli mbalimbali ikiwamo kilimo cha mazao ya biashara kama alizeti na zabibu.

"Zao la alizeti katika mkoa wa Dodoma linastawi sana na hivi sasa mkoa unashika nafasi ya pili katika uzalishaji wa zao hilo, lakini pia katika zabibu sisi tunafuata ukiitoa Afrika ya Kusini kwa kuzalishaji, hivyo basi watu wachangamkie fursa hizi," alisema Iringo.

Alisema pia kutokana na ongezeko la watu jijini Dodoma wanawaalika wafanyabiashara wa hoteli za kisasa kuja kuweza ili kutoa huduma zenye ubora kwa watu kama mabalozi watakapo hamia hapa mara baada ya ujio wa Rais Magufuli.

"Lakini pia tunahitaji wawekezaji wa shule za kimataifa, hospitali za kisasa ambazo zitaweza kumudu watu wanaoingia hivi sasa katika jiji letu na mtu atakaye wekeza katika mkoa huu hatapata shida katika jambo lolote," alisema Iringo.

Aliongeza kuwa kumekuwapo na changamoto ya upatikanaji wa mbegu, hivyo kuwataka watu kuja kuwekeza katika kilimo cha mbegu za mazao. "Dodoma ni fursa mpya nchini kwa wakati huu katika uwekezaji na hii ni sehemu ya watu kumuunga mkono Rais katika kujenga makao makuu ya nchi," alisema.



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, akiomba kupewa mabango ya kero za wananchi wa Kijiji cha Itundwi, Wilaya ya Kondoa mkoani Dodoma juzi, wakati wananchi hao waliposimamisha msafara wake kwa lengo la kufikisha kero yao ya umeme. **PICHA: IBRAHIM JOSEP**

# Serikali yatakiwa kutengea sekta kilimo bajeti ya 10%

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WADAU wa kilimo nchini wameitaka serikali kuongeza fedha kwenye bajeti ya kilimo hadi kufikia asilimia 10 ya bajeti kuu kama ilivyokubaliwa kwenye azimio la Malabo.

Akizungumza kwenye mkutano uliowakutanisha wadau wa kilimo nchini jijini Dodoma, Joram Wimo kutoka Shirika la Action Aid, alisema pamoja na kuwa Tanzania kusaini mkataba huo, lakini utekelezaji wake umekuwa ni wa kusuasua.


Alisema sekta ya kilimo ni muhimu nchini kwa kuwa inaajiri watu wengi, hivyo ikiongezewa fedha itaweza kuinua wananchi wake kiuchumi.

Alisema pamoja na sekta ya kilimo kutengewa fedha kiasi kidogo, pia hata utekelezwaji wa fedha hizo kwenye miradi ya maendeleo siyo wa kuridhisha.

"Kwa mfano kwenye ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka wa fedha 2016/17, inaonyesha kuwa fedha zilizotengwa kwenye miradi ya maendeleo ilikuwa ni asilimia tano tu, mwaka 2017/18 ilikuwa ni asilimia 16 na mwaka 2018/19 iliongezeka hadi asilimia 42, japo uhalisia wa bajeti hiyo bado ni changamoto."

Kwa upande wake Mkuu wa kitengo cha ushawishi kitaifa kutoka Shirika la Oxfam, Victoria Lihiru, alisema mkutano huo utawasaidia wadau wa sekta ya kilimo kujua ni namna gani bajeti ya serikali inavyoandaliwa ili wao waweze kufanya ushawishi wa masuala mbalimbali kuingia kwenye bajeti.

Mkutano huo pia uliwakutanisha wadau hao na Wizara ya Kilimo, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Fedha na Mipango, Tamisemi na Wizara ya Viwanda na Biashara.





Nuru Anuwar Abdallah, mke wa mmiliki wa kiwanja chenye mgogoro katika Mtaa wa Mlandege akionyesha ramani ya eneo lenye mgogoro, wakati akizungumza na waandishi wa habari mjini Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Washangaa agizo la waziri kupuuzwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

LICHA ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Haji Omar Kheri, kuliagiza Baraza la Manispaa Mjini kuwahamisha wafanyabiashara katika eneo la Mlandege ambalo lina mgogoro wa ardhi kwa muda mrefu, agizo hilo halijatekelezwa.

Wakizungumza na waandishi wa habari, wamiliki wa eneo hilo wamesikitishwa kutotekelezwa kwa agizo lililotolewa na waziri huyo mwenye mamlaka serikalini.

Anuwar Abdallah, mmiliki wa eneo la kiwanja plot namba 142 Mlandege, alisema siku 40 zilizotolewa na Baraza la Manispaa kutekeleza zoezi hilo baada ya kuwapa notisi wafanyabiashara waliopo katika eneo hilo kuondoka, inashangaza kuona siku zimepita, lakini hakuna hatua iliyochukuliwa, huku wafanyabiashara wakiendelea kufanya biashara kama kawaida.

Alielezea kinachoendelea ni uonevu na jambo lisilokubalika katika nchi inayoendeshwa kwa utawala wa kisheria na utawala bora.

"Tuna wasiwasi mkubwa kuwa kuna harufu ya rushwa katika utekelezaji wa zoezi hili, maana muda mrefu tunadai haki yetu, lakini bado inayumbishwa kila viongozi wanapotoa maagizo ya kuondoka kwa wafanyabiashara hao zoezi halifanyiki," alisema Anuwar. Aidha, Anuwar alimwomba Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, kuingilia kati suala hilo ili haki iweze kutendeka kwa kuwa ana vibali vyote vinavyomruhusu kumiliki na kufanya ujenzi katika eneo hilo. Aliongeza: "Tuna imani sana na Rais Shein, ni mtu mwadilifu na anayependa haki, lakini kuna baadhi ya watendaji wa umma katika serikali yake sio waadilifu na kushindwa kutenda haki pale inapostahiki."

Naye Anuwar Abdallah, alisema wameshahangaika sana kudai haki yao ambayo kwa miaka mingi imeshawasababishia hasara kubwa na kushindwa kufikia lengo.

"Tokea tulipopata vibali halali vya kujenga miaka 10 iliyopita hivi sasa gharama za ujenzi zimepanda, hivyo tunashindwa kufikia lengo ambapo wakati huo mfuko wa saruji ulikuwa Sh. 5,000 hivi sasa ni Sh. 15,000," alisema.

Takriban siku 40 zimepita tokea Waziri Haji Omar Kheir alipofanya ziara katika eneo hilo lenye mgogoro wa ardhi akiambatana na watendaji wakuu wa idara mbalimbali akiwamo Mkurugenzi wa Idara ya Mipango Miji, Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa Mjini, Mkurugenzi wa Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe na Mkuu wa Wilaya ya Mjini Unguja na kulitaka Baraza la Manispaa ya Mjini kuchukua hatua ya kuwaondoa wafanyabiashara hao.

Baada ya agizo hilo Baraza la Manispaa lilitoa notisi ya siku 40 kwa wafanyabiashara hao kuondoka kwa hiyari yao kabla ya hatua za kisheria hazijachukuliwa dhidi yao, lakini bado wanaendelea na bishara zao hadi sasa.

Wafanyabiashara hao wamejenga majengo ya kudumu katika eneo la uhifadhi wa barabara ambalo kisheria linatakiwa liwe wazi wakati wote bila ya kufanywa shughuli yoyote katika eneo hilo.

# Wahitimu watarajiwa sheria wafundwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Tume ya Kurekebisha Sheria, Jaji Mshibe Ali Bakari, amewataka wahitimu watarajiwa wa kitivo cha sheria katika Chuo Kikuu cha Zanzibar (SUZA) kuzingatia waliyojifunza.

Aliyasema hayo wakati wa sherehe maalumu ya usiku wa sheria ilioandaliwa na kitivo hicho chini ya ufadhili wa kampuni inayojihusisha na sheria (Stallion Attorneys).

Alisema ni lazima wanafunzi hao wafahamu kuwa elimu ya sheria inatokana na uwezo binafsi atakaokuwa nao mtu katika utendaji wake wa kazi.

Alisema bila ya kujituma katika elimu hiyo ya sheria, hutaweza kufanikiwa na kuwataka wahitimu hao kuongeza bidii watakapokuwa kazini.

Aliwashauri kuzingatia zaidi elimu ya kivitendo wakitambua kwamba taifa linawategemea katika upatikanaji wa haki pindi watakapoanza kazi kwenye maeneo mbalimbali ndani na nje ya Tanzania.

Aidha, Jaji Mshibe alitoa wito kwa wanafunzi hao watakapomaliza masomo yao kutambua kuwa wanawajibu mkubwa wa kuthamini wateja wao iwapo wataajiriwa kwenye kampuni au watajiajiri wenyewe kwa lengo la kuwatunza na kuwaenzi wateja wao.

Miongoni mwa wamiliki wa kampuni ya Stallion Attorneys, Shehzada Walii, alisema katika fani ya sheria zipo changamoto nyingi, lakini wahusika hawatakiwi kukata tamaa. Alisema wapo baadhi ya wanafunzi wengi hushindwa kufikia malengo yao kutokana na kukata tamaa kufuatia changamoto mbalimbali zinazowakabili.

Hata hivyo alisema uwepo wa changamoto hizo kwa wanafunzi zikiwamo za ajira hawapaswi kurudi nyuma badala yake wanatakiwa kuongeza bidii zaidi katika kuonyesha uwezo waliojifunza wakiwa darasani.

"Mimi binafsi wakati namaliza chuo kikuu ni mara kadhaa niliomba kujitolea sehemu mbalimbali, lakini nilikosa fursa, ila sikuwahi kukata tamaa ...nilihangaika kila leo ili nitimize ndoto zangu na hatimaye leo hii kwa kiasi fulani nimefanikiwa," alisema.

Naye Mkuu wa Kitivo cha Sheria wa SUZA, Dk. Makame Mohamed, alisema chuo hicho kitaendelea kuwajengea uwezo wanafunzi wanaosoma sheria kwa lengo la kuhakikisha wanauzika katika soko la ajira.

# Ataka wahusika ukatili wabanwe

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAOFISA watekelezaji wa sheria wameitaka jamii kutoa ushirikiano katika kesi za ukatili wa kijinsia kwa wahusika waliotenda vitendo hivyo kupewa adhabu wanazostahiki, ili iwe fundisho kwa wengine.

Maofisa hao waliyasema hayo kwa nyakati tofauti kwenye kamati za kupambana na ukatili wa kijinsia Wilaya ya Wete, Mkoa wa Kaskazini Pemba na Wilaya ya Mkoani, Mkoa wa Kusini Pemba.

Akizungumza wakati wa mkutano uliofanyika Wete, Pemba, Hakimu wa Mkoa wa Kaskazini ambaye pia ni Mkuu wa Mahakama ya Watoto, Abadalla Yahya Shamhun, alisema kuanzi Januari mwaka huu, hadi sasa amelazimika kufuta kesi 10 kutokana na kuletewa maombi na familia.

"Wakati kesi iko mahakamani imeshafikia nusu njia, familia huja na sababu za kuzuia kesi hiyo kuendelea na mara nyingine huletewa barua kutoka kwa mwendesha mashtaka kuwa wamefahamiana na pia wahusika wameoana, hivyo huwezi kuendelea tena na kesi," alisema.

Alieleza kuwa hata hivyo, Sheria ya Kumlinda Mtoto No. 6 ya mwaka 2011 na Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai namba saba ya mwaka 2018 zinasisitiza kuwa kutokutoa ushahidi ni kosa la jinai, hivyo hivi sasa Mahakama italazimika kuwaweka ndani wanaokataa kutoa ushahidi wakiwamo wanafamilia pamoja na waliotendewa makosa wenyewe.

Naye Kaimu Mkuu wa Polisi Wilaya ya Wete, Fakih Yussuf Mohammed, alisema moja ya changamoto zinazoikumba ofisi yake katika kupambana na vitendo hivi ni muhali wa wanafamilia pamoja na viongozi ambao mara nyingine hutoa maelekezo ya kuwa kesi nambari fulani isiendelezwe tena (ifutwe).

Fakih alishauri kuwekwa mwongozo maalum wa kufuatwa kwa viongozi, ambapo atakayekiuka pia abainishwe na kuchukuliwa hatua kwa vile wao Polisi hawawezi kupinga amri zinazotoka juu kuhusu kuzuiwa kuzipeleka kesi mahakamani.

Mwanasheria kutoka Ofisi ya Mwendesha Mashtaka, Juma Mussa Omar, alisema mwaka jana Wilaya ya Mkoani ilipokea kesi 142, lakini nyingi hazikuweza kusonga mbele kutokana na familia kutaka suluhu.

Alisema hata ofisini kwake kuna kesi 42 za Januari hadi Aprili mwaka huu, lakini tayari kuna mrundikano mkubwa wa barua ambazo zinaomba kesi hizo zifungwe.

Kamati hizo zote mbili za kitaifa zilikutana na timu ya Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), Zanzibar kwa kubadilishana mawazo juu ya hatua madhubuti za kufuata kwa ajili ya kukomesha vitendo hivyo viovu katika jamii.

Mkurugenzi wa TAMWA Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, aliitaka jamii kuwa mstari wa mbele kutoa ushahidi na pia vyombo vya sheria kuchukua hatua madhubuti dhidi ya watendaji wasiokuwa waaminifu.

# Kijiji chapewa msaada wa elimu wa mil. 300/-

Na Frank Monyo

KAMPUNI ya Pan African Energy Tanzania (PAET) imekabidhi madarasa sita, vyoo vitatu, ofisi mbili za walimu pamoja na madawati 138 vyenye thamani ya zaidi ya milioni 300 katika kijiji cha Migeregere kata ya Kikole wilayani Kilwa.

Katika makabidhiano hayo yaliofanyika mwishoni mwa wiki na Meneja Uwajibikija kwa jamii wa PAET, Andrew Kashangaki, alisema wameamua kujenga madarasa hayo baada ya kuguswa na hali iliyokuwapo kijijini hapo kwa wanafunzi kutembea umbali mrefu kufika shuleni.

"PAET tumeguswa na hali iliyokuwapo kijijini hapa ambapo wanafunzi wanatembea zaidi ya kilomita 10 ili kufika ilipo shule ya sasa ya Migeregere hali inayosababisha mahudhurio ya wanafunzi kuwa mabaya pamoja na usalama mdogo wa wanafunzi wakati wa kwenda na kurudi nyumbani," alisema Kashangaki.

Kwa upande wa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa, Renatus Mchau, ambaye alikuwa mgeni rasmi wakati wa makabidhiano hayo aliwataka wananchi wa wilaya yake kuzingatia elimu kama njia pekee na ya kisayansi inayoweza kuwasaidia kujikwamua katika lindi la umaskini.

"Mimi nawaomba mzingatie sana elimu kwa watoto wenu na pia kulinda majengo haya. Haya madarasa ni yenu na hii shule ni ya kwenu, hivyo ulinzi wa shule hii inawategemea ninyi kwa kiasi kikubwa," alisema Mchau.

Aliongeza kuwa shule hiyo iliyojengwa na PAET katika Kitongoji cha Mbeta, kijiji cha Migerege kata ya Kikole ni kati ya shule maalum zinazoitwa shule shikizi (Satelite school) ambayo itatumika kwa ajili ya wanafunzi wa madarasa ya awali hadi darasa la pili na kisha kuhamishiwa katika shule mama ya Migeregere ambapo kwa sasa wanafunzi wanaotoka katika kitongoji hicho kwenda Shule ya Migeregere wapo 54 kuanzia darasa la awali hadi la saba.

Katika hatua ya kuunga mkono mchango huo PAET wa kukuza elimu wilayani humo, Mchau aliahidi kuleta walimu katika shule hiyo ili huduma iliyokusudiwa iweze kuanza kutolewa mara moja.

Naye Diwani wa Kikole, Musa Kinjokwile, aliishukuru kampuni hiyo kwa kuwajengea shule jambo ambalo lilionekana kama ndoto kwao kwani watoto wanaozaliwa katika kijiji hicho wengi wao hawaendi shule kutokana na umbali uliopo unasababisha mwanafunzi kutembea zaidi ya kilomita 20 kwa siku kufuata elimu jambo ambalo limekuwa changamoto katika kijiji hicho kwa miaka mingi.



Washiriki wa shughuli ya kufanya usafi katika fukwe ya Andy- Mbezi Beach B jijini Dar es Salaam, wakifanya usafi katika eneo la fukwe hiyo jana, ikiwa ni sehemu ya kuadhimisha Wiki ya Utumishi wa Umma. **MPIGAPICHA WETU**

# NEMC yahamasisha usafi maeneo ya fukwe

Na Mwandishi Wetu

BARAZA la Taifa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kwa kushirikiana na asasi za kiraia zimefanya usafi katika fukwe ya Andy-Mbezi B jijini Dar es Salaam, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma na kutoa wito kwa wananchi kuendelea kutunza mazingira kwa kufanya usafi.

Asasi hizo za kiraia zilizoshirikiana bega kwa bega katika zoezi zima la kusafisha fukwe ni pamoja na Nipe Fagio, Aspect, Green Waste Pro.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa zoezi la kufanya usafi katika fukwe hiyo, Kaimu Meneja wa Kanda ya Mashariki wa NEMC, Mhandisi Benjamin Mchwampaka, alisema ni muhimu wananchi wakajenga mazoea ya kusafisha fukwe kwani ni eneo linalojumuisha jamii mzima.

"Fukwe hii ya Andy imekuwa na uchafu mwingi kutokana na kutofanyiwa usafi kwa muda mrefu, hivyo kwa kufanya zoezi hili kutahamasisha wakazi wa maeneo haya kujitoa katika kufanya usafi mara kwa mara ili kufanya mazingira ya fukwe kuwa salama," alisema Mhandisi Mchwampaka.

Alisema katika zoezi la kufanya usafi wamebaini chupa za plastiki ambazo hazijarejelezwa zinazofungashiwa vinywaji mbalimbali ndio zimekidhi katika maeneo mengi ya fukwe na kupelekea mazingira kutokuwa salama kutokana na kukithiri kwa uchafu.

"Tumefanya kuchambua taka katika makundi mbalimbali ili kutupa urahisi wa kubaini aina za taka husani chupa za rangi na kufuatilia mzalishaji ili tusaidiane nae katika kutafuta suluhu la kufanya urejereshaji wa chupa hizo ili kuondoa tatizo hilo," alisema.

Alisema kuna vijana wamejiajiri kukusanya chupa nyeupe na kujipatia kipato kwa kurudisha kwa mzalishaji kwa ajili ya kuzirejereza, hivyo kwa kutumia njia hii iliyoondoa chupa za maji kuzagaa mitaani ndiyo itakayotumika ili kuondoa chupa za rangi.

"Kwa asilimia kubwa taka za plastiki ni janga kutokana na ukweli kwamba kwenye mazingira zinapoingia ardhini zinaweza kukaa muda mrefu bila kuoza na pia kama vinaingia baharini zinakwenda kuharibu ikolojia na kupelekea viumbe wa baharini kupotea," alisema.

Mhandisi Mchwampaka alisema serikali imepiga hatua kubwa katika kulinda mazingira kwa kukataza matumizi ya mifuko ya plastiki ambayo ilikuwa ikiendelea kuharibu taswira ya nchi kimazingira na kusababisha maeneo mengi kuathirika.

Aliongezea kuwa Shirika la Viwango Tanzania (TBS) limewataka watengenezaji na waagizaji wa vifungashio na vibebeo vilivyoruhusiwa kisheria wawasiliane nao ili kuwapata maelekezo stahiki juu ya viwango vilivyopitishwa kutengeneza na kutumika hapa nchini.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Mbezi Beach B, Fatuma Ramadhan, aliishukuru serikali na wadau wa mazingira kwa kufanya zoezi hilo kwani limezidi kuwapa nguvu wananchi katika kujitoa kwenye shughuli za kijamii kama hizi ambazo manufaa yake ni endelevu.

Naye Ofisa Mhamasishaji Jamii kutoka Asasi ya Nipe Fagio, Abdalah Mikulu, alisema ushirikiano kati ya wadau wa mazingira, wananchi na serikali kutasaidia kuondoa tatizo la taka nchini na kupelekea mazingira yakawa salama kwa kizazi cha sasa na baadaye.

## Jamii yahimizwa kutumia intaneti

Elizabeth Zaya

CHAMA cha Internet Tanzania (ISOC), kimesema kuwa kutokana na mabadiliko ya teknolojia katika mitandao ya jamii kunahitaji kuangalia namna ya kutumia mitandao hiyo katika manufaa ya kiuchumi.

Akizungumza katika warsha ya kuwajengea uwezo waandishi wa habari katika matumizi ya intaneti kupitia mitandao ya jamii, Mwenyikiti wa ISOC Tanzania, Abibu Ntahigiye, alisema waandishi ni daraja katika jamii kwa kupata taarifa mbalimbali zinazotokea ndani na nje ya nchi, hivyo ipo haja kutumia nafasi yao kuendelea kuielimisha jamii matimizi sahihi ya mitandao hiyo.

Alisema matumizi ya mitandao ya jamii inatumika vibaya kwa baadhi ya watu kwa kutuma vitu visivyo na maadili na manufaa kwa jamii na wakati mwingine kuharibu vijana ambao huiga vitu visivyo manufaa kwao.

Ntahigiye alisema ni vema matumizi ya mitandao ya jamii ifundishwe kuanzia shule za msingi, ili kuelewa maana ya matumizi hayo katika manufaa ya maendeleo ya nchi.

Alisema baadhi ya nchi zimeanza kufundisha wanafunzi namna ya kutumia mitandao kimanufaa zaidi badala ya kuitumia kinyume.

Alisema matumizi mabaya ya mitandao ya jamii yanachangia baadhi ya vijana kukosa sifa za kuajirika kutokana na matumizi mabaya ya mitandao kwa kutuma picha ambazo hazina maadili pamoja na kuandika vitu visivyofaa katika jamii inayowazunguka.

Katibu Mkuu wa Chama hicho, Nazarius Kirama, alisema malengo ya ISOC ni kutaka kuhakikisha jamii yote inafikiwa na mitandao ya jamii katika kupata habari za manufaa ya elimu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi inayojishughulisha na Uhamasishaji Makundi yaliyopembezoni (TIBA), Marcela Lungu, alisema kuwa baadhi ya picha chafu za wanawake zilizo katika mitandao ya jamii hazitumwi na wanawake pekee, bali zinatumwa pia na baadhi ya wanaume.

# HABARI KIMATAIFA




Rais wa Tume ya Umoja wa Ulaya, Jean-Claude Juncker (kushoto) na Rais wa Baraza hilo, Donald Tusk, wakiwa jijini Brussles. **PICHA: AFP**.

## Wakuu EU watoa onyo kwa mrithi wa May

**LONDON,** Uingereza

VIONGOZI wa Umoja wa Ulaya (EU), wametoa onyo kwa Waziri Mkuu ajaye wa Uingereza, kuwa asitegemee mabadiliko yoyote kwenye mkataba ulioafikiwa kuhusu nchi hiyo kujiondoa kwenye Umoja wa Ulaya.

Onyo hili limekuja wakati aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje wa Uingereza, Boris Johnson, akitarajiwa kuchuana na Waziri wa Mambo ya Nje wa sasa, Jeremy Hunt, kuongoza chama cha Conservative na baadaye kuwa waziri mkuu mpya.

Wawili hao wameweka wazi kuwa wanataka majadiliano mapya na EU kuhusu mkataba huo wa kujiondoa, ambao viongozi wa Umoja wa Ulaya, walikuwa wamekubaliana na Waziri Mkuu anayeondoka Theresa May.

Rais wa Baraza la Umoja wa Ulaya, Donald Tusk, alisema umoja huo hautabadilisha mkataba huo lakini, utaivumilia Uingereza katika mchakato wa kujiondoa.

Kuelekea Oktoba 31, siku ya mwisho ya Uingereza kujiondoa kwenye umoja huo, Tusk alisema kuwa viongozi wa EU wako tayari kufanya kazi na yeyote atakayekuwa waziri mkuu mpya wa Uingereza.

RFI

## Mkuu wa majeshi Ethiopia auawa kwa kupigwa risasi

**ADDIS ABABA,** Ethiopia

WAZIRI Mkuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed, amesema Mkuu wa Majeshi Seare Mekonen ameuawa kwa kupigwa risasi na mlinzi wake.

Ahmed amesema kuwa Mekonen alipigwa risasi baada ya kuzuka kwa ghasia Jumamosi jioni katika taifa hilo la pembe ya Afrika.

Kwa mujibu wa mwandishi wa shirika la habari la AFP, Abiy, alizungumza kupitia kwenye televisheni ya taifa akiwa amevaa mavazi rasmi ya kijeshi, baada ya kutokea jaribio la mapinduzi katika Jimbo la Amhara.

Hata hivyo hakuna maelezo zaidi yaliyotolewa kuhusiana na lengo la mashambulio hayo katika jimbo la pili lenye watu wengi zaidi nchini Ethiopia linaloongozwa na Rais wa kikanda Ambachew Mekonen.

Ubalozi wa Marekani ulitoa tahadhari baada ya kusikika milio ya bunduki katika Mji Mkuu wa Addis Ababa, na pia vurugu karibu na Mji Mkuu wa Jimbo la Amhara, Bahir Dar.

Serikali ya Ethiopia imesema jaribio hilo la kuipindua serikali ya kikanda kaskazini mwa nchi hiyo lilishindikana.

Ofisi ya Waziri Mkuu, Ahmed, imelaani jaribio hilo la mapinduzi katika ujumbe uliotoa katika mtandao wa kijamii wa Twitter Jumamosi jioni.

Wakazi katika mji mkuu wa nchi hiyo, Bahir Dar, walisema walisikia milio ya bunduki.

Nchini Ethiopia mivutano ya kikabila imekuwa ndio chanzo cha mapigano katika nchi hiyo ambayo kwa muda mrefu imetawaliwa kwa mkono wa chuma.

Tangu Abiy alipochukua mamlaka Aprili 2018, ameleta mageuzi, ikiwa ni pamoja na kuwaachia wafungwa wa kisiasa, mageuzi ya kiuchumi, ameruhusu makundi ya watu mbali mbali kurudi nchini, na aliahidi kupambana na vitendo vinavyokiuka haki za binadamu, na ameboresha uhuru wa vyombo vya habari.

Lakini anakabiliana na kuongezeka kwa mivutano kati ya makundi ya kikabila katika nchi hiyo ambayo kwa kawaida ni juu ya ardhi na rasilimali, mivutano hiyo inasababisha vurugu kubwa katika nchi yenye idadi ya watu zaidi ya milioni 100.

**DW**

## Marekani yashambulia mifumo ya kompyuta ya silaha za Iran

**TEHRAN,** Iran

MAREKANI imeanzisha mashambulizi ya mtandao kwenye mifumo ya silaha za Iran siku ya Alhamisi wakati Rais wa Marekani, Donald Trump alipoachana na mashambulizi ya anga, ripoti nchini Marekani zimeeleza.

Gazeti la Washington Post limeeleza kuwa mashambulizi hayo ya mtandaoni yameharibu mifumo ya kompyuta inayodhibiti roketi na mitambo ya kurushia makombora.

Gazeti la New York Times nalo limeeleza kuwa tukio hilo ni kulipiza kisasi baada ya kushambuliwa kwa ndege yake isiyo na rubani, mashambulizi dhidi ya meli za mafuta ambazo Iran imedaiwa na Marekani kuziteketeza.

Mbali na kufanya shambulizi hilo, Marekani pia imeweka vikwazo ambavyo Rais Trump ameeleza kuwa ni vikubwa.

Alisema vikwazo vilikuwa vinahitajika kuizuia Iran kutengeneza silaha za nyuklia na vikwazo vya kiuchumi vitaendelea mpaka pale Tehran itakapobadili uelekeo.

Mvutano baina ya nchi hizo mbili ulijitokeza tangu Marekani ilipojiondoa kwenye mkataba wa nyuklia wa mwaka 2015 kati ya Iran na mataifa yenye nguvu duniani na kuiwekea vikwazo vilivyotikisa uchumi wa taifa hilo.

Wiki iliyopita Iran ilisema itaongeza viwango vilivyowekwa kwenye mkataba huo kuhusu mradi wa nyuklia.

Rais Trump alisema hataki vita na Iran, lakini alionya kuwa nchi hiyo itakabiliwa na uharibifu ikiwa mzozo utatokea.

Mashambulizi yalipangwa kwa wiki kadhaa, vyanzo vimeviambia vyombo vya habari nchini Marekani ikaelezwa kuwa ni njia ya kulipa kisasi mashambulizi ya mabomu dhidi ya meli za mafuta kwenye Ghuba ya Oman.

Mashambulizi hayo yalilenga mifumo ya silaha zinazotumiwa na majeshi ya nchi hiyo, yaliyoshambulia ndege isiyo na rubani siku ya Alhamisi wiki iliyopita.

Kwa pamoja Washington Post na AP zimeeleza kuwa mashambulizi ya mtandao yaliyofanywa na Marekani yameharibu mifumo, wakati New York Times limesema ililenga kuzima mifumo hiyo kwa muda.

Siku ya Jumamosi duru za kiusalama za Marekani zilionya kuwa Iran ina mpango wa kufanya mashambulizi ya mtandaoni dhidi yake.

Mkurugenzi wa Shirika la Usalama na Miundombinu nchini Marekani, Christopher Krebs, alisema hila za mashambulizi zinaelekezwa na utawala wa Iran na mawakala wake dhidi ya viwanda vya Marekani na mashirika ya kiserikali.

Washington Post lilieleza kuwa Iran imekuwa ikijaribu kudukua mifumo ya meli za kijeshi za Marekani.

Vikwanzo hivyo ni vipi?

Ununuzi wa noti za Marekani unaofanywa na Iran. Biashara ya dhahabu na vyuma vingine, graphite, aluminium, chuma, mkaa na programu zinazotumiwa katika sekta ya viwanda.

Zingine ni ubadilishanaji wa fedha unaohusishwa na sarafu ya Iran, vitendo vinavyohusishwa na ulipaji madeni ya Iran, sekta ya magari ya Iran.

Vikwazo hivyo viliathiri uchumi wa nchi hiyo kwa sababu ililenga sekta zake kuu za mafuta na benki.

Vikwazo hivyo vilizuia kampuni ya Marekani kufanya biashara na Iran, lakini pia kampuni ya kigeni au nchi kufanya biashara na Iran.

**BBC**

# Bashiru: CCM haijawahi kuwa na vikosi vya jeshi

Na Gwamaka Alipipi

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Bashiru Ally, amesema chama hicho hakina wala hakijawahi kuwa na vikosi vya kijeshi, bali kina vikundi vya vijana ambao kazi yao ni kusimamia itifaki na hamasa.

Amesema vijana hao kazi yao ni kuhakikisha shughuli za chama zinakwenda vizuri, viongozi wa chama wanakuwa sehemu salama wakati wa mikutano na vikao.

Alitoa ufafanuzi huo jana jijini Dar es Salaam wakati akifungua semina ya mabalozi wa shina 1,487 wa Wilaya ya Kinondoni, iliyolenga kuwapa uelewa wa masuala ya uchaguzi, hususani uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika Oktoba, mwaka huu.

"Sheria ya Vyama vya Siasa imetueleza vyama visiwe na vikosi, na hatukuwahi kuwa na vikosi na hatuna vikosi hivyo. Tunavyo vikundi vya vijana ambao kazi yao ni kusimamia itifaki na hamasa katika shughuli za chama popote tutakapokuwa," alisema Dk. Bashiru na kuongeza:

"Niwapongeze vijana, kila ninapokwenda vikundi hivi vinajitokeza, ndivyo vilivyotuwezesha kuwa hapa. Ndiyo wanaopanga kwenye mikutano, mwenyekiti ukae upande gani, katibu ukae upande gani, na wapo humu wanaangalia mamluki, endeleeni kufanya kazi hiyo."

Dk. Bashiru alilazimika kutoa ufafanuzi huo baada ya watu kupitia mitandao ya kijamii kueleza CCM inamiliki vikosi vya kijeshi.

"Sisi vikosi vya kijeshi vya nini? Tuna Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) lililofundwa na kuandaliwa na Mwalimu Julius Nyerere ambalo linasimamia mipaka yetu ya nchi, tuna Jeshi la Magereza, tuna Jeshi la Polisi," alisema Dk. Bashiru.

Dk. Bashiru alisema watu hao wamekuwa wakifanya vikao usiku, wanafanya siasa kwenye mitandao na wanahabari wakitoa taarifa za uongo.

Pia, aliwataka mabalozi wa mashina kuwahamasisha wananchi ili wajitokeze kwa wingi kujiandikisha kwenye Daftari la Kudumu la Wapigakura, kwa kupita nyumba kwa nyumba.



Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, akiongea na waandishi wa habari (hawapo pichani) baada ya kufanya ziara ya kushtukiza katika Kituo cha Polisi Gogoni, Wilaya ya Kimara jana.. **PICHA: BEATRICE SHAYO**.

## Lugola ashangaa mahabusi kukaa miezi 6 kituo polisi

Na Beatrice Shayo

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, ameshangazwa kuona mahabusi 11 waliofutiwa kesi mahakamani kuwekwa katika Kituo cha Polisi Gogoni, Wilaya Kimara kwa zaidi ya miezi sita kinyume na sheria.

Lugola aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati alipofanya ziara ya kushtukiza katika kituo hicho kwa ajili ya kufuatilia utekelezaji wa maagizo aliyoyatoa.

Alisema kumekuwa na malalamiko kuwapo kwa baadhi ya vituo vya polisi vinavyokaa na watuhumiwa kwa muda mrefu bila kuwafikisha mahakamani.

"Katika kituo hiki cha Gogoni taarifa nilizokuwa nazo kinaongoza kwa kuwashikilia watuhumiwa na kukaa nao kwa muda mrefu," alisema na kuongeza:

"Baada ya kufika katika kituo hiki kweli nimekutana na mahabusi 32, nimewahoji mmoja baada ya mwingine nikakutana na hawa mahabusi 11 waliofutiwa kesi zao," alisema.

Lugola alisema watuhumiwa hao 11 wanahusika na kesi za mauaji, alivyowahoji wengine wamekaa gerezani miaka saba na baada ya muda huo sasa mahakama imewarudisha katika vituo vya polisi kufuata kesi zao.

"Nimewakuta Gogoni wana miezi sita hapa, mimi kama waziri, hii sio sawa nimeongea na uongozi wamenieleza kwanini wapo hapa, lakini kuna changamoto ya Idara ya Mahakama, Jeshi la Polisi na Mkurugenzi wa Mashtaka ya Jinai, kwamba wapo hapa muda wote huo majalada yao yalishapelekwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka nimelichukua kama waziri ili kutatua tatizo hilo kwa kuwa walishaanza kugoma hata kula, lakini nimewasihi nitalifanyia kazi," alisema.

Alisema ameshangazwa mahabusi hao kukaa miezi sita bila kupatiwa taarifa na kuitaka mahakama iwapeleke gerezani na sio kukalishwa kituoni hapo kwa miezi sita.

Aidha, alisema akiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi analazimika kupita katika vituo mbalimbali vya polisi vya nchini kukagua na kuona ufanisi wa Jeshi la Polisi linavyotoa huduma kwa wananchi.

Pia alisema anawasikiliza wananchi ambao anawakuta katika vituo vya polisi kujua changamoto wanazokutana nazo katika kupata huduma vituoni.

# THRDC yaainisha mambo 10 hatari kwa uhai wa Azaki

INATOKA UK. 3

na Mratibu wa Kitaifa wa THRDC, Onesmo Olengurumwa, hakuna anayejua dharura ya serikali imebeba dhamira gani kwa Azaki.

Alisema muswada unafuta tafsiri ya mashirika yasiyo ya kiserikali na kuweka ufafanuzi mpya ambao hautambui nyanja ya ulinzi na uendelezaji wa haki za binadamu.

Pia, haujumuishi kampuni zenye dhamana, makundi madogo ya uwekezaji (Vikoba kwa ujumla), mashirika ya dini, na kwamba hayawezi kuwa kampuni zisizofanya biashara na kwamba ni lazima wafanye biashara au uwekezaji ili usajiliwe kama kampuni yenye dhamana.

**Pili:** Kuondolewa usajili moja kwa moja; kwamba muswada umeongeza kifungu kinachofuta usajili wa NGO zilizosajiliwa chini ya sheria hiyo, ambayo hayajajumuishwa kwenye ufafanuzi mpya ndani ya miezi miwili baada ya muswada kupitishwa kuwa sheria.

Uchambuzi huo ulisema muswada huo maalum wa sheria zilizoandaliwa, marekebisho mchanganyiko ulipelekwa chini ya hati ya dharura bungeni Juni 19, mwaka huu na kuwanyima haki ya kushiriki mchakato wa utengenezaji wa muswada huo.

"Hatua hii inakiuka uhuru wa kujumuika, njia mbadala zitolewe kwa mashirika haya halali kuhamia katika upande unaowafaa na siyo kufutiwa usajili moja kwa moja," alisema Olengurumwa.

**Tatu:** NGO kusimamishwa kabla ya kusikilizwa; muswada huo umeongeza vipengele vinavyohusu kusimamishwa NGO wakati wanaongejea suluhu ya bodi, kitu ambacho ni kinyume na kanuni za haki, dhana ya kutokuwa na hatia mpaka ithibitishwe.

**Nne:** Mamlaka ya Msajili kufuatilia na kutathmini mashirika yasiyo ya kiserikali kila robo mwaka; kwamba imeongezwa kipengele kinachompa msajili mamlaka makubwa ikiwamo kufuatilia na kutathimini NGO kila baada ya robo mwaka .

"Mamlaka kama haya yanaweza kutumika kiholela na kwa kuonea, ni vigumu kutembelea mashirika yote nchini," alisema Mratibu huyo.

**Tano:** Mamlaka ya Msajili kufanya uchunguzi; kwamba muswada umempa uwezo msajili kuchunguza NGO kwa kushirikiana na vyombo vya dola, na kwamba yanahusishwa na udhibiti unaoangalia haki ya faragha na uhuru.

"Msajili wa NGO hapaswi kupewa mamlaka chini ya sheria nyingine kufanya uchunguzi wa uhalifu, wigo wa sheria yoyote iliyoandikwa haujulikani na hii inaweza kuvutia matumizi mabaya ya mamlaka na kusababisha kukamatwa kiholela na kuingiliwa," ilifafanua.

**Sita:** Kuondolewa kwa usajili wa kudumu, marekebisho hayo yanapendekeza NGO kujisajili tena baada ya miaka kumi, kupata upya hati zao baada ya miaka 10 na kwamba ni mzigo kiuchumi na kiutawala na ofisi ya msajili.

Aidha, Olengurumwa alisema utaratibu huo unaondoa uhuru wa mashirika yasiyo ya kiserikali na kujenga woga na udhibiti binafsi.

**Saba:** Mamlaka ya kutamka kuwa asasi ni hatari, marekebisho hayo yanampa mamlaka waziri kutamka kuwa asasi ni hatari kwa utawala bora nchini, na kwamba halitakuwa halali, kipengele ambacho kinaziacha NGO katika hatari ya matumizi mabaya ya mamlaka.

Nane: Kuzilazimisha NGO kuwa kibiashara, kwamba zitasajiliwa chini ya sheria za kampuni zenye dhamana ambazo hazikuomba hati ya ukubalifu yanatakiwa kukubaliana na Sheria ya Kampuni na kuwa mashirika ya kibiashara vinginevyo yatafutwa.

**Tisa:** NGO na Azaki yenye hati ya ukubalifu kusitishwa ndani ya miezi miwili; kwamba kampuni yenye dhamana iliyosajiliwa chini ya sheria ya kampuni yenye hati ya ukubalifu na chini ya Sheria ya NGO itachukuliwa kuwa imesajiliwa chini ya Sheria ya NGO na kuondolewa katika orodha ya kampuni ya Msajili wa kampuni.

**Kumi:** Asasi kuondolewa usajili ndani ya miezi mwili; kwamba asasi yoyote iliyosajiliwa chini ya sheria ya asasi ambayo haiendani na ufafanuzi au tafsiri iliyotolewa kwenye muswada litafutwa.

"Shirika lisilo la kifuasi, lisilo la kibiashara litaondolewa usajili moja kwa moja ndani ya miezi miwili baada ya muswada wa sheria kupita," alisema Olengurumwa.

## MATANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### MAGARI NA VIPURI

**CRANE FUSO FOR SALE,**

(1.) Fighter 2002, SAKAI_340,3 stages, New in TZ,
2. Magnum 1991, TADANO_290, 2 Stages, 3 years in TZ.

**"Dalali Hatakiwi" Simu 0692 469 669**

### NAFASI ZA KAZI

**TANGAZO LA KAZI ,** Mtu wa IT diploma anahitajika na Mesenger form four au six. Mawasiliano: **justinatemba22@gmail.com, 0715 885533**

### ELIMU/ MASOMO

**NAFASI ZA MASOMO,** Chuo cha Uuguzi na Ukunga MASSANA kilichopo dar es Salaam, Mbezi Beach Goba Road. Kinatangaza nafasi za masomo kwa ngazi ya Diploma na cheti yatakayoanza mwezi wa September 2019. Njoo tukujazie Form Kupitia Mtandao wa Nacte: 0713 321260/0769 666880

**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**


### KUPOTEA KWA CHETI



**Abdulhaman Ally Msabaha** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita chenye Index namba SO751-0551 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa mwaka 2018 katika shule ya Sekondari Luhuwiko. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi Taarifa: **DOD/DOD/RB/79160/2019.**

115290902

### KUPOTEA KWA VYETI



**Japhet Likinjiye Lukumay** anatangaza kupotea kwa veti vifuatavyo cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S0629-0151** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la taifa mwaka 2010 katika shule ya sekondari Edmund Rice Sinon, cheti cha Diploma chenye namba **0001746** kilichotolewa na chuo cha Arusha Technical College mwaka 2016 na cheti cha Kuzaliwa. Yeyote atakaeona vyeti hivi atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **CD/LR/IR/RB/307/2019**

215290502

### KADI YA GARI IMEPOTEA

**MUSSA JAFARI KIDELI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 248 DCR** Aina yake NOAH. Yeyote atakaeiona anaombwa atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **MOR/MOR/RB/79144/2019.**

115291002

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MARIAM MUHAMED FAKI** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T.544DCU** AINA YA SUZUKI CARRY RANGI NYEUPE. YEYOTE ATAKAEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI **MBE/RB/785882/2019.**

115291201

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SUNDAY MUHAMED FAKI** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T.707 CLD** AINA YA SUZUKI CARRY RANGI NYEUPE.YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU. TAARIFA YA POLISI **MBE/RB/78584/2019.**

115291102

### KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**KISHAN ENTERPRISES LTD** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya SANYA M/CYCLE yenye namba za usajili **T 545 CJK** Chassisnamba **LKIPC11KXD1018349.**Engi nenamba**.157PM14301177** 69. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOM/TR/RB/828/2019.**

***Uza,***

***Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza***

***Nasi Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0767 223 311***

**JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?**

**Nipashe**

NI JIBU LAKO NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO
KWA BEI NAFUU SANA

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz au piga simu: 0767 223 311**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# De Ligt achagua kutua Juventus



**TURIN,** Italia

BEKI wa kati wa Ajax, Mdachi Matthijs de Ligt, amefanya maamuzi ya kuichagua Juventus kuwa ndio timu atakayojiunga nayo kwenye dirisha hili la uhamisho wa majira ya joto.

Uamuzi wa De Ligt sasa unakuwa ni wazi kwamba amezitosa Barcelona, PSG na Manchester United zilizokuwa zinamwania kwa udi na uvumba.

Beki huyo ameripotiwa kuzipiga chini Man United na Barcelona na kuamua kujiunga na Juventus kwa mujibu wa taarifa kutoka Uholanzi.

Man United ilikuwa ikimsaka sana beki huyo, huku kukiwapo na taarifa kwamba angeenda Barcelona wakati huo huo kukiwa na ripoti nyingine zilizokuwa zikimhusisha na mpango wa kwenda kujiunga na Paris Saint-Germain.

Lakini, sasa kinachoelezwa ni kwamba Juventus wameonekana kushinda vita hiyo ambapo wamedaiwa watambeba De Ligt kwa dau la pauni milioni 62 na kumaliza utata wote wa beki huyo atakwenda wapi kwenye dirisha hili la majira ya kiangazi.

Hivi karibuni, kwenye fainali ya Ligi ya Mataifa ya Uefa baina ya Ureno na Uholanzi, kuliripotiwa kwamba, Cristiano Ronaldo, anayekipiga kwenye kikosi cha Juventus alimshauri beki huyo kinda kwenda kujiunga na wababe hao wa Italia, ambao kuanzia msimu ujao watakuwa chini ya kocha Maurizio Sarri.

De Ligt alikuwa kwenye kiwango bora kabisa msimu uliopita wakati alipoisaidia Ajax kufika nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, huku wakibeba mataji ya ligi za ndani huko Uholanzi, ikiwamo taji la Ligi Kuu.

# Brazil yatinga 16-bora fainali Copa Amerika



**SAO PAULO,** Brazil

BRAZIL imefuzu hatua ya mtoano ya michuano ya Copa America baada ya kuishushia kipigo kizito Peru cha mabao 5-0 kwenye dimba la Corinthians.

Casemiro alianza kuwaweka mbele wenyeji hao wa michuano hiyo kabla ya Roberto Firmino na Everton kuongeza bao moja moja kuelekea kipindi cha pili.

Nahodha, Dani Alves aliongeza bao la nne baada ya mapumziko, huku Willian ambaye alitokea benchi akifunga bao la tano, lakini Gabriel Jesus akakosa penalti dakika ya mwisho ya mchezo huo.

Ushindi huo umeihakikishia Brazil kumaliza hatua ya makundi ikiwa na pointi saba, baada ya ushindi wa 3-0 dhidi ya Bolivia na sare ya bila kufungana na Venezuela.

'Selecao' hao walionekana kuwa kwenye kiwango cha kuvutia zaidi tangu dakika ya mwanzo, wakati Casemiro alipoanza kuifungia.

Roberto Firmino ambaye ndiye alikuwa akiongoza mashambulizi mbele, aliweza kufunga bao la pili kwa kumalizia mpira uliokolewa na golikipa wa Peru, Pedro Gallese.

Everton, ambaye alifunga akitokea benchi kwenye mchezo dhidi ya Bolivia, akafunga bao la tatu kwa kutumbukiza mpira kwenye kona ya mbali kulia.

Baada ya hapo mchezo ulionekana kuwa mikononi mwa Brazil, kwani Peru walishindwa kabisa kuipenya ngome ya Wabrazil hao.

Alikuwa nahodha, Dani Alves ambaye alifunga bao la nne kabla Willian kuhitimisha ushindi huo kwa kufunga la tano.

# SANCHEZ: FURAHA TELE NINAPOICHEZEA CHILE



**SAO PAULO,** Brazil

ALEXIS Sanchez amebainisha kwamba mara zote anakuwa na furaha zaidi kuichezea nchi yake ya Chile, kitu ambacho kinaonekana kama dongo kwa Klabu yake Manchester United baada ya kuipa ushindi kwenye michuano ya Copa America dhidi ya Ecuador.

Akicheza akiwa na maumivu baada ya kuumia kipindi cha kwanza, Sanchez alifunga bao kipindi cha pili kuiwezesha Chile kuibuka na ushindi wa 2-1 na kufuzu hatua ya mtoano wa 16-bora kwenye michuano hiyo, Ijumaa.

Sanchez aliendelea na mchezo huo baada ya kupewa dawa za kutuliza maumivu na alifunga bao dakika ya 51 kwenye mchezo huo uliopigwa dimba la Fonte na kuwawezesha mabingwa hao watetezi kutinga hatua ya mtoano.

"Niliumia kifundo cha mguu. Niliendelea kucheza kwa sababu ya mapenzi yangu kwa timu ya taifa," alisema Sanchez baada ya mchezo huo akiwaambi waandishi wa habari.

"Ninapoichezea nchini yangu mara zote nakuwa na furaha kubwa," aliongeza kusema mchezaji huyo ambaye alikuwa na kiwango kibovu katika Klabu yake ya Man United msimu uliopita."

Hilo lilikuwa ni bao la pili kwa mshambuliaji huyo katika mashindano hayo, ambaye ametoka kuwa na msimu mgumu pale Manchester United.

Sanchez, ambaye analipwa mshahara wa pauni 500,000 kwa wiki pale Old Trafford, ni wazi kwamba msimu ujao hataweza kuendelea kucheza pale United kutokana na kiwango chake kutokuwa katika ubora uliotarajiwa kama alivyokuwa akicheza Arsenal wakati alipotua akitokea Barcelona.

# HABARI MICHEZO



## Barcelona yasajili mtoto wa wakala wa De Jong

**BARCELONA,** Hispania

KLABU ya Barcelona imethibitisha kwamba imemsajili beki wa Uholanzi, Mike van Beijnen, ambaye ni mtoto wa wakala wa Frenkie de Jong, Ali Dursun.

Van Beijnen mwenye umri wa miaka 20, amesaini mkataba wa miaka miwili na ataichezea Barca B kipindi cha maandalizi ya msimu. Na katika mkataba wake kuna kipengele cha kumuuza kwa euro milioni 100.

Alishawahi kuzichezea Klabu za NAC Breda, PSV Eindhoven na Willem II, ambako alicheza sambamba na De Jong kwenye timu ya vijana.

Barca iliizidi kete Paris Saint-Germain kumsajili kiungo wa Ajax, De Jong Januari mwaka huu baada ya mazungumzo na baba yake Van Beijnen.

Kiungo huyo wa Uholanzi De Jong atatambulishwa rasmi Julai Mosi baada ya Barca na Ajax kukubaliana ada ya awali ya euro milioni 75.

Wakati huo huo, Barca watacheza na washindi wa pili wa Kombe la Ligi ya Europa, Arsenal kwenye mchezo wa maandalizi ya msimu mpya katika Uwanja wa Camp Nou Agosti 4, mwaka huu.

Mchezo huo wa kila mwaka wa taji la Joan Gamper ni utamaduni wa Barca kumaliza msimu kabla ya kuanza kwa msimu mpya, lakini mechi hiyo ya mwaka huu itachukua nafasi katikati ya ziara yao ya Japan na Marekani.

Barca itacheza na washindi wa Kombe la Ligi ya Europa, Chelsea mjini Tokyo Julai 23 kabla ya kukutana na timu ya Andres Iniesta, Vissel Kobe Julai 27.

Baada ya kurudi, Barcelona itacheza na Arsenal, na pia watakuwa na michezo miwili dhidi ya Napoli Agosti 7 mjini Miami na mjini Michigan Agosti 10, mwaka huu.

## WACHEZAJI MAN UNITED WATAKA POGBA AONDOKE



**MANCHESTER,** England

NYOTA wa Manchester United wameripotiwa kwamba wanataka Paul Pogba kuondoka kipindi cha majira ya joto kwa manufaa mazuri ya klabu hiyo.

Kiungo huyo wa Ufaransa anataka kuondoka klabuni hapo baada ya kukaa kwa kipindi cha miaka mitatu ambapo alitua hapo kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni 89 akitokea Juventus na wiki iliyopita alibainisha kwamba anataka kwenda kupata changamoto mpya.

Real Madrid na Juventus zinaongoza kwenye mbio za kuwania kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, ambaye Man United imesisitiza kuwa hauzwi.

Pogba amebakia kuwa mchezji maarufu kwenye vyumba vya kubadilisha nguo, lakini sasa wachezaji wa United wanataka kuanza upya chini ya kocha, Ole Gunnar Solskjaer, kwa mujibu wa Gazeti la The Sun.

Hawataki mambo kuendelea kama yalivyo hivi sasa na wanaona ni wakati mwafaka kwa nyota huyo kuuzwa.

Gazeti la Daily Mail liliripoti wiki hii kwamba, United inatarajia Pogba atasafiri nao kwenye maandalizi ya msimu mpya, licha ya kiungo huyo kuweka wazi kwamba anataka kuondoka hapo kwenye dimba la Old Trafford.

United inasisitiza kwamba Pogba hauzwi na kama wakitaka kumuuza bei yake ni pauni milioni 150.

United wanapanga Pogba atakuwa sehemu ya kikosi chao kwenye ziara yao nchini Australia, China na Singapore ikiwa ni maandalizi ya msimu mpya wa Ligi Kuu.

## Sane agoma kutua Bayern



**MANCHESTER,** England

WINGA wa Manchester City, Leroy Sane, ameripotiwa kwamba amewaambia marafiki zake kwamba atakataa ofa ya kujiunga na Bayern Munich kipindi hiki cha majira ya joto.

Sane amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka Man City, huku Bayern ikionyesha nia kubwa ya kutaka huduma yake.

Hata hivyo, kwa mujibu wa Gazeti la The Sun, uwezekano wa mchezaji huyo kujiunga na timu hiyo ni mdogo kwani Sane amebainisha kwamba anataka kuendelea kuichezea Man City, ambayo kwa sasa yupo nayo kwenye mazungumzo ya kuongeza mkataba mpya.

Sane, ambaye alijiunga na Man City mwaka 2016, amebakiwa na miaka miwili kwenye mkataba wake wa sasa pale Etihad.

Msimu uliopita Sane alifunga mabao 16 na kutoa pasi za mwisho 18 katika mechi 47 alizocheza kwenye mashindano yote na aliisaidia Man City kutwaa mataji matatu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, hakuwa chaguo la kwanza kwenye kikosi cha City msimu uliopita na ana matumaini ya kuwa chaguo la kudumu la kocha Pep Guardiola kama atabakia klabuni hapo.

Ripoti inaonyesha kwamba, Sane ana mashaka juu ya kurudi Ujerumani, ambako anahisi kiwango chake hakitakuwa kwenye ubora zaidi.

Mapema mwezi huu, Sane alikuwa kwenye orodha ya wafungaji wa Ujerumani dhidi ya Belarus na Estonia, ikiwa ni baada ya kuachwa kwenye kikosi hicho katika michuano ya Kombe la Dunia mwaka jana nchini Urusi.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# DANI ALVES: NAONDOKA PSG

Leo ninakamilisha mzunguko mwingine katika maisha yangu, ningependa kuishukuru familia ya PSG kwa fursa...

**RIO,** Brazil

BEKI kisiki wa Brazil, Dani Alves ametangaza kuwa ataondoka Paris Saint-Germain baada ya kuwatumikia mabingwa hao wa Ufaransa kwa misimu miwili sasa.

Alves, 36, ameweka wazi mustakabali wake huo wa baadaye ikiwa ni saa chache baada ya kuiongoza Brazil akiwa amevaa kitambaa cha unahodha na kufunga bao la nne wakati wakishinda 5-0 kwenye mechi ya Copa America dhidi ya Peru juzi.

**Beki huyo wa pembeni, Alves, ambaye hivi karibuni aliichezea Sevilla, Barcelona na Juventus kabla ya kutua Ufaransa, sasa ni mchezaji huru na amekuwa akihusishwa na uwezekano wa kutua Ligi Kuu England, Premier League.**

"Leo ninakamilisha mzunguko mwingine katika maisha yangu, mzunguko wa ushindi, kujifunza na uzoefu," Alves aliandika katika ukurasa wake wa Instagram.

"Ningependa kuishukuru familia ya PSG kwa fursa niliyoipata ya kujenga ukurasa katika historia ya klabu hii.

"Napenda kuwashukuru wafanyakazi wote kwa upendo wao, heshima na ushirikiano kuanzia siku ya kwanza. Unafanya klabu hii kuwa maalum zaidi.

"Ilikuwa miaka miwili ya ujasiri na kuendelea kuwekeza ili kutimiza malengo yangu, lakini katika maisha kila kitu kina mwanzo, katikati na mwisho na sasa wakati umefika kuhitimisha hapa."

Alves, ambaye ameichezea Brazil mechi 107, alijiunga na PSG mwaka 2017 na kutwaa ubingwa wa Ligue 1 mara mbili na Kombe la Ufaransa mara moja wakati wa kipindi chake klabuni hapo.

Beki huyo ambaye alitua PSG mwaka mmoja na Mbrazil mwenza, Neymar, kuna uwezekano wakaondoka pamoja msimu huu kufuatia mshambuliaji huyo naye kueleza nia yake ya kutaka kurudi alipopaita "nyumbani", Barcelona.

Neymar ambaye amekuwa akiandamwa na majeraha, ameiambia PSG kuwa anataka kuondoka na klabu hiyo imeeleza ipo tayari kumuuza majira haya ya joto wakati huu Real Madrid nayo ikielezwa kuonyesha nia ya kupata huduma ya mshambuliaji huyo.

## KWA UFUPI

### WAN-BISSAKA AKARIBIA UNITED

Manchester United na Crystal Palace wamefanya mazungumzo kuhusu uwezekano wa kuipata saini ya Aaron Wan-Bissaka, jambo ambalo litashuhudiwa beki huyo Muingereza akitua Old Trafford kwa ada ya awali kiasi cha pauni milioni 42.5. (Mail)

### PSG YAONGOZA KWA COUTINHO

Paris St-Germain inaongoza mbio za kuinasa saini ya kiungo wa Barcelona na Brazil, Philippe Coutinho, 27. (Calciomercato)

### MBAPPE AWEKWA KIPORO MADRID

Real Madrid inataka kumfanya mshambuliaji wa Paris St-Germain na Ufaransa, Kylian Mbappe, 20, kuwa usajili wao mkubwa majira ya joto yajayo. (AS)

### ICARDI ATAKIWA KUMRITHI LUKAKU

Manchester United inavutiwa kuipata saini ya straika Muargentina Mauro Icardi, 26, kama sehemu ya kuruhusu kuondoka kwa mshambuliaji Mbelgiji Romelu Lukaku, 26, kwenda kujiunga na Inter Milan. (Express)

### ERIKSEN AGEUKIA UNITED, JUVE

KIUNGO wa Tottenham na Denmark, Christian Eriksen, 27, anatolea macho kutua Manchester United ama Juventus baada ya dili la kujiunga na Real Madrid kushindikana. (Mirror)

### ARSENAL YAMFUATA NKUNKU

Arsenal itapaswa kulipa pauni milioni 13.5 kwa Paris St-Germain ili kumpata mshambuliaji Christopher Nkunku, 21, wakati huu RB Leipzig pia ikivutiwa naye. (L'Equipe - in French)

### SANCHEZ ADODA SOKONI

MIPANGO ya Manchester United imekuwa ikikabiliwa na kizuizi kwa sababu ya kukosa mnunuzi wa mshambuliaji wa kimataifa wa Chile, Alexis Sanchez, 30. (Express)

### SANE KUGOMA KUTUA BAYERN

WINGA Mjerumani Leroy Sane, 23, atakataa kutua Bayern Munich na kutoa upendeleo wa kuendelea kubaki Manchester City. (Sun)

### BENITEZ KUSEPA WIKI HII

KOCHA wa Newcastle, Rafa Benitez anajiandaa kuondoka wakati mkataba wake utakapomalizika mwishoni mwa wiki hii, hiyo ikiwa ni kutokana na mabadiliko ya kiuhusiano na mmiliki mpya. (Mail)

### LAMPARD KUSHAWISHIWA DERBY

Derby inajiandaa kumpa ofa ya mkataba wenye thamani ya pauni milioni 10 kocha Frank Lampard ili kumshawishi kuachana na kutua Chelsea. (Star)

### DEMBELE AGOMA KUIACHA LYON

STRAIKA wa Lyon, Mfaransa Moussa Dembele, 22, ameweka kando uwezekano wa kuhama majira haya ya joto licha ya kuhusishwa na klabu kadhaa ikiwamo Manchester United. (Goal)

### LIVERPOOL SPURS KWA GBAMIN

Liverpool, Tottenham na Everton zote zinavutiwa kuipata saini ya kiungo wa Mainz na Ivory Coast, Jean-Philippe Gbamin, 23. (Fussballtransfers - in German)

### BEGOVIC AWANIWA KILA KONA

Watford, Stoke, Celtic, Fenerbache na Olympiakos zote zinavutiwa na huduma ya kipa wa Bournemouth, Asmir Begovic na Mbosnia huyo mwenye umri wa miaka 32, yupo tayari kucheza kikosi cha kwanza. (Star)

# RAIS FUFA AANIKA SIRI UGANDA KUICHAPA DRC

**Na Somoe Ng'itu,** MISRI

SIRI ya Timu ya Uganda (The Cranes) kufanya vizuri katika mechi yao ya kwanza ya Kombe la Mataifa Afrika (Afcon) 2019, imetokana na kufanya maandalizi mazuri, imeelezwa.

Uganda inaongoza Kundi A baada ya kupata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), ikifuatiwa na wenyeji Misri ambao walipata ushindi wa bao 1-0 ilipofungua mashindano haya dhidi ya Zimbabwe.

Akizungumza na gazeti hili jana, Rais wa Shirikisho la Soka Uganda (Fufa), Moses Magogo, alisema kikosi chao kilikuwa na maandalizi ya muda mrefu ambayo mwaka huu yameanza kuzaa matunda.

Magogo alisema kikosi hiki kinachoshiriki mashindano haya, kilianzia kwenye Timu ya Taifa ya Vijana ya umri chini ya miaka 17 na ndicho kilichoiwakilisha Uganda katika fainali zilizopita za Afcon ambazo zilifanyika mwaka juzi nchini Gabon.

"Haya ni matokeo ya kufanya maandalizi mazuri, maandalizi ya muda mrefu, na pia wachezaji wetu kuwa na uzoefu, walijifunza vitu vingi katika mashindano ya Gabon, kujituma kila wanapokuwa na mpira," alisema Magogo.

Rais huyo aliongeza kuwa pia wamejipanga kuhakikisha wanauwakilisha vema Ukanda wa Cecafa katika mashindano haya yanayoendelea nchini hapa, ambayo kwa mara ya kwanza yanashirikisha timu 24.

"Sisi ni wawakilishi wa Cecafa, tunajisikia furaha kuanza na ushindi, tuna timu nne (Uganda, Tanzania, Kenya na Burundi) mwaka huu, tunawaombea wenzetu Tanzania wafanye vizuri pia na Kenya, pole kwa Burundi," alisema kiongozi huyo kabla ya Stars na Kenya kushuka dimbani jana kuvaana na Senegal na Algeria kwenye mechi zao za Kundi C.

Uganda itashuka tena dimbani Jumatano Juni 26, kucheza mechi yake ya pili dhidi ya Zimbabwe na itamaliza hatua ya makundi Jumapili kwa kuwakabili wenyeji Misri.




Mkurugenzi wa Maendeleo ya Michezo Wizara ya Habari Utamaduni Sanaa na Michezo, Dk. Yusuf Singo (kushoto), akiwa na baadhi ya washindi wa Promosheni ya Soka la Afrika inayoendeshwa na Kampuni ya tiGO muda mfupi baada ya kuwakabidhi bendera ya Taifa kwa ajili ya kwenda kushuhudia michuano ya Mataifa ya Afrika (Afcon) 2019, inayoendelea nchini Misri. Wa kwanza kulia ni Ofisa Biashara Mkuu wa tiGO, Tarik Boudiaf. **PICHA: JOHN BADI**

# Mama Sitta afungukia Misri 'unazi' wake Simba

**Na Somoe Ng'itu, MISRI**

UKIONDOA shughuli za kisiasa na serikali ambazo amekuwa akizifanya kwa muda mrefu, mpira wa miguu umekuwa ni sehemu ya maisha ya kila siku ya Mbunge wa Urambo, Margareth Sitta, ameeleza.

Mbunge huyo ni mmoja kati ya wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao wamekuja nchini hapa kuishangilia Timu ya Taifa (Taifa Stars ) ambayo inashiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon) 2019.

Akizungumza na Nipashe jijini Cairo jana, Mama Sitta, alisema amekuwa akishiriki katika hatua mbalimbali za kufanikisha Simba inafanya vizuri katika Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano yote ambayo wanashiriki.

Mama Sitta alisema ushabiki wake kwa klabu hiyo umetokana na mapenzi ambayo mume wake (Spika wa zamani wa Bunge la Tanzania- Samweli Sitta), amekuwa nayo kwa muda mrefu.

Mbunge huyo alisema huwa anafurahi sana Simba inapofanya vema katika mechi zake, kwa sababu mbali na kutwaa mataji, lakini pia inawafanya Watanzania wanashirikiana zaidi na kusahau tofauti zao nyingine.

"Mimi ninaijua vizuri sana Simba, tangu zamani, nimefua jezi zao wakiwa wanajiandaa na mechi mbalimbali kipindi kile Rage (Ismail Aden) anacheza, najua vitu vingi vya klabu hiyo," alisema Mama Sitta.

Aliongeza kuwa ili klabu ziweze kufanya vema, ni lazima viongozi wake wawe na muda mrefu wa kufanya shughuli za klabu kutokana na ushindani na changamoto zilizoko katika soka kwa sasa.

"Ni ngumu kufanya vizuri sehemu zote, ni kama kipindi kile, Rage anaiongoza Simba na jimboni kwake wananchi wanamhitaji, wote ni muhimu, hutakiwi kufanya vibaya au kuegemea upande mmoja, mpira ni ushindani na anayetaka kuongoza awe amejiandaa," aliongeza mbunge huyo.

Alisema pia mpira wa sasa umebadilika na anawataka Watanzania wasaidiane kuhakikisha jina la nchi linatangazika vizuri kwenye mashindano mbalimbali kimataifa.

"Sisi tumekuja katika kundi la kwanza, tutawashangilia vijana wetu halafu tutarudi Dodoma kuendelea na bunge, kujitoa huku ni kwa ajili ya mapenzi na nchi yetu," Mama Sitta aliongeza.

Aliwataka mashabiki kutowakatisha tamaa wachezaji, na badala yake kuendelea kuwa karibu nao ili kuhakikisha wanafanya vizuri kwenye vita hii ya kuwania ubingwa wa Kombe la Afrika.

Stars jana usiku ilicheza mechi yake ya kwanza Afcon 2019 dhidi ya Senegal kabla ya Alhamisi kushuka tena dimbani kuwavaa majirani zao Kenya na kisha Jumatatu ijayo kuhitimisha mechi za makundi dhidi ya Algeria.

# Amunike: Stars itashangaza Afcon

**Na Mwandishi Wetu, MISRI**

HAKUNA mechi rahisi! Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Emmanuel Amunike, amesema anaamini kikosi chake kimejipanga kuwashangaza wapinzani wao katika mechi za fainali za Kombe la Afrika (Afcon) 2019 kwa kuwa kila timu inamhofia mpinzani wake.

Taifa Stars ambayo mara ya mwisho ilishiriki fainali hizi mwaka 1980 huko Lagos nchini Nigeria iko Kundi C lenye vigogo Algeria, Senegal na majirani zao Kenya maarufu Harambee Stars.

Akizungumza na gazeti hili jana kabla ya kuivaa Senegal, Amunike, alisema kikosi chake kiko tayari kwa mapambano na wanaamini wanayo nafasi ya kusonga mbele katika michuano hiyo inayofanyika kwa mara ya 13 hapa barani Afrika.

Amunike alisema amewaambia nyota wake wasiwe na hofu yoyote katika mechi zao mbili zilizobakia, na kuacha kufikiria matokeo yoyote ambayo wamepata kwenye michezo iliyopita.

"Haya ni mashindano makubwa, kwanza tulihitaji kufuzu na sasa tunatakiwa kuendelea pale tulipoachia, hakuna anayerudi nyuma, hakuna mechi rahisi, kila timu inamhofia mwenzake, kila siku tunajipanga kusahihisha makosa halafu tunaingia uwanjani kuonyesha tulichojifunza," alisema Amunike.

Aliongeza kwake anaamini kila timu ina nafasi ya kusonga mbele na tuache kuwaza ukubwa wa majina ya wachezaji au nchi wanazotoka.

Alisema kwamba uzoefu walioupata katika mechi za kufuzu, umewaimarisha wachezaji na sasa kila mmoja anajua anachotakiwa kukifanya kulingana na wakati uliopo.

"Hakuna mechi rahisi, hata wapinzani wetu pia wanatuhofia, kikubwa ni kuwa makini tunapokuwa na mpira na kufahamu tunachotakiwa kukifanya pale mpira unapokuwa kwa wenzetu, nidhamu ya mpira ndio hutengeneza nafasi," Amunike alisema.

Naye Mbunge wa Chemba (CCM), Juma Nkamia, alisema mbali na wachezaji wa Stars kupeperusha bendera ya Tanzania kwa heshima, vile vile hili ndilo daraja la wao kujiweka sokoni kimataifa, kutokana na idadi kubwa ya mawakala waliofika nchini hapa kufuatilia fainali hizi.

Stars itashuka tena uwanjani kucheza mechi yake ya pili Alhamisi Juni 27 kuvaana na Kenya na itamaliza hatua ya makundi kwa kupambana na Algeria Julai Mosi, mwaka huu.

# Michezo

Jumatatu Juni 24, 2019

Nipashe


## Dani Alves: Naondoka PSG



HABARI UK. 30

## Mo Salah sasa 'Mfalme' Misri

**Na Somoe Ng'itu, Misri**

MSHAMBULIAJI tegemeo wa Timu ya Taifa ya Misri (Mafarao), Mohammed Salah, amekuwa nyota na kipenzi cha mashabiki wa soka ndani na nje ya uwanja.

Salah ambaye anaichezea Liverpool ya England, ndiye mchezaji ambaye ana mashabiki wengi nchini hapa, na hali hiyo inamfanya aitwe "Mfalme".

Nyota huyo wa zamani wa Roma ya Italia, pia picha yake imekuwa ikionekana katika matangazo mbalimbali katika majiji yote ya hapa Misri.

Anapoonekana sura yake katika televisheni, hushangiliwa zaidi kuliko wachezaji wenzake na hata anaposhika mpira, mashabiki pia humshangilia.

"Tunampenda sana Salah, tunaipenda na Liverpool, tunajua ataisaidia Misri kuchukua Kombe la Afrika mwaka huu," alisema shabiki mmoja aliyejitambulisha kwa jina la Essam Abdelhamid.

Shabiki huyo alisema kuwa imekuwa ni kawaida ya mashabiki wa Misri kumpenda zaidi mchezaji mmoja na hiyo inatokana na uwezo wake anaouonyesha katika mechi za klabu na nchi yake.

"Hizi ni zama za Mo Salah, kila mtu anajua anachokifanya, ingawa tunajua wachezaji wote ni muhimu katika timu, lakini kwa sasa tunamkubali sana Mo Salah, wapo wengine wazuri kama Suleiman, Amri Warda na wengine," Abdelhamid alisema.

Hata hivyo, mashabiki wa Misri wamesema kuwa mashindano ya mwaka huu ni magumu kwa sababu wachezaji wanajuana.

"Mambo si rahisi, timu nyingi zinaijua Misri, ila tunaamini kombe litabaki nyumbani," alisema Morsi Abdallah.

Misri imepangwa Kundi A ikiwa na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Zimbabwe na Uganda (The Cranes).









Mshambuliaji wa Chile, Alexis Sanchez (kushoto), akiambaa na mpira dhidi ya beki wa Ecuador, Pedro Velasco, kwenye mechi ya michuano ya Copa America juzi, mechi ambayo aliifungia Chile bao la ushindi wakati wakishinda 2-1 na kufuzu robo fainali. **HABARI UK. 28**

# OKWI AIWEKA KIPORO SIMBA

## ●●● Ajipandisha thamani Afcon Misri, asema sasa anashikilia ofa kibao ila awatuliza mashabiki Msimbazi kwa kueleza kuwa...

**Na Somoe Ng'itu,** MISRI

BAADA ya kuifungia timu yake ya Taifa ya Uganda (The Cranes), bao la pili katika ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), mshambuliaji wa Simba, Emmanuel Okwi, amesema kuwa bado hajafanya uamuzi wa klabu gani ataitumikia kuelekea msimu ujao.

Okwi ni mchezaji huru baada ya kumaliza mkataba wake na mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba na sasa yuko huru kufanya mazungumzo na klabu yoyote inayohitaji huduma yake.

Akizungumza na Nipashe jijini Cairo jana, Okwi alisema kuwa ana ofa kutoka klabu mbalimbali za ndani na nje barani Afrika, lakini kwa sasa akili yake iko katika kulitumikia taifa lake kwenye fainali hizi za Afcon zinazoendelea nchini hapa.

Okwi alisema anahitaji kufanya uamuzi wa hatima yake kwa umakini kwa sababu mchezo wa mpira ndio unaendesha maisha yake na familia.

"Akili na mawazo yangu yako katika timu ya Taifa, kuhusu klabu gani nitasaini, kwa sasa sina la kusema," alisema kwa kifupi mshambuliaji huyo wa zamani wa SC Villa ya Uganda na Yanga ya Tanzania.

Aliongeza kuwa anafahamu kwamba klabu mbalimbali zinahitaji huduma yake, lakini kwa sasa zinatakiwa zisubiri mpaka atakapomaliza kuitumikia Uganda ambayo iko katika Kundi A pamoja na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Zimbabwe na wenyeji Misri.

Mmoja wa viongozi wa Simba walioko Cairo aliliambia gazeti hili kuwa amezungumza na Okwi na kumweleza kwamba amewataka mashabiki wa klabu hiyo kutokuwa na hofu kuhusu hatima yake.

"Okwi amesema tusiwe na wasiwasi, ameshafanya mazungumzo na sisi na yako katika hatua nzuri, Simba ni nyumbani kwake, ni klabu ambayo anaipa kipaumbele kwa kila kitu," alisema kiongozi huyo.

Taarifa za ndani kutoka Simba zinasema kuwa thamani ya Okwi itazidi kupanda baada ya kuonyesha kiwango cha juu katika mechezo wao wa kwanza dhidi ya DRC, ambapo alitangazwa kuwa mchezaji bora wa mechi.

Mganda huyo ambaye hakuanza vema msimu uliopita, alionyesha kiwango cha juu katika mechi za mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, huku akifunga bao pekee kwenye mechi dhidi ya TP Mazembe iliyomalizika kwa Simba kutolewa hatua ya robo fainali kwa kuchapwa mabao 4-1.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

770856 541002 >